

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Sita – Tarehe 9 Aprili, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):**

Taarifa za Matoleo y a gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo: -

1. Toleo Na. 06 la tarehe 05 Februari, 2021;
2. Toleo Na. 07 la tarehe 12 Februari, 2021;
3. Toleo Na. 08 la tarehe 19 Februari, 2021;
4. Toleo Na. 09 la tarehe 26 Februari, 2021;
5. Toleo Na. 10 la tarehe 05 Machi, 2021;
6. Toleo Na. 11 la tarehe 12 Machi, 2021;
7. Toleo Na. 12 la tarehe 19 Machi, 2021; na
8. Toleo Na. 13 la tarehe 26 Machi, 2021.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Upungufu wa Walimu Shule za Msingi na Sekondari
Maeneo ya Vijijini**

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kumaliza tatizo la upungufu wa Walimu nchini, hasa shule zilizopo maeneo ya vijijini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu katika shule za msingi na sekondari, kuanzia Disemba 2015 hadi Septemba 2020, Serikali imeajiri walimu 10,666 wa shule za msingi na walimu 7,515 wa shule za sekondari na kuwapanga kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa. Aidha, kuanzia mwezi Desemba 2015 hadi

Septemba 2020, Halmashauri ya Mji Njombe imeajiri walimu 21 wa shule za msingi na walimu 111 wa shule za sekondari.

Vilevile Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Utumishi na Utawala Bora na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaajiri walimu wapya 6,000 wa shule za msingi na sekondari ifikapo Juni 2021 ili kujaza nafasi zilizoachwa na walimu waliofariki ama kustaafu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kupitia ofisi za wakuu wa mikoa imekuwa ikifanya uhamisho wa ndani kwa kuwahamisha walimu waliozidi hasa kwenye maeneo ya mijini na kuwapanga kwenye shule zenye uhaba mkubwa wa walimu ambazo nyingi zipo maeneo ya vijiji. Serikali itaendelea kuajiri na kuwapanga walimu kwenye shule za msingi na sekondari hasa zenye mahitaji makubwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swalii nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swalii la msingi lakini niulize swalii la kwanza. Kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa maamuzi aliyojatoa siku ya Jumatatu ya kuruhusu kuajiriwa kwa walimu 6,000 kwa haraka, tunamshukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini ni ukweli kwamba walimu 6,000 wanaokwenda kuajiriwa bado wanakwenda kufanya *replacement*; mahitaji ya walimu katika shule bado ni makubwa sana. Maamuzi ya Serikali ya kutoa elimu bure kwa nia njema yamefanya kuwe na uhaba mkubwa sana wa walimu katika maeneo hasa ya vijiji. Kwa hiyo, pamoja na mipango ambayo imeelezewa lakini bado kuna tatizo kubwa na ninapenda kujua, je, Serikali inaweza

bado ikatoa *commitment* kwamba itaajiri walimu wa kutosha? Kwasababu hii namba iliyotajwa hapa bado haitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; naelewa kuna vigezo ambavyo vinatumika kwenye ugawaji wa walimu kwenye maeneo mbalimbali. Ni ukweli usiopingika kwamba kwa yale maeneo ambayo ni miji ambayo iko ndani ya halmashauri vigezo ambavyo vinatumika kwa kweli havina uhalisia kwasababu maeneo hayo unakuta yanaangaliwa sana kwasababu yana miji lakini vilevile yana maeneo mengi sana yenye shule nydingi sana ambayo wananchi wamejitoa wakajenga shule ambazo zipo katika maeneo ya vijijini. Wanapoangalia vigezo vya *reallocation* unakuta kwamba hawaangalii hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali; Je, Wizara itakuwa tayari kuititia upya vigezo vya ku-*allocate* walimu ili maeneo ya halmashauri za miji ambayo yana maeneo makubwa ya zaidi ya kilometra 25 yaweze kupata walimu ili elimu yetu iwe na tija? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri wazi kabisa kwamba alichozungumza Mheshimiwa Mbunge ya ubaha wa walimu nchini pamoja na *replacement* ya walimu 6,000 ambayo tunakwenda kuifanya hivi karibuni bado upo. Na Serikali imoji-*commit* hapa katika *statement* yangu ya awali kwamba tutaendelea kuajiri kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Na mpango huo upo na ni endelevu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ondoa wasiwasi kwenye hilo kwa sababu Serikali iko makini, na Serikali ya Rais wa Sita, mama Samia Hassan Suluhu, imejipanga kuhakikisha tunaondoa kabisa tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, amezungumzia kuhusu Wizara kama tutakuwa tayari kuititia vigezo vya

ugawaji wa walimu upya. Nikubali kabisa hilo tumelipokea, moja, ni kama ushauri, lakini pili, tutaendelea kulizingatia kuhakikisha kabisa ugawanyaaji wa walimu wote nchini unafuata usawa na haki katika maeneo yote. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Tatizo ambalo linaikumba Njombe Mjini la uhaba wa walimu, ndilo tatizo hilohilo ambalo linaikumba Wilaya ya Chunya kwa uhaba wa walimu. Ajira mara ya mwisho iliyopita Wilaya ya Chunya tulipata takribani walimu 26 tu ambaao ni idadi ndogo ukilinganisha na ukubwa wa Wilaya ya Chunya.

Je, Serikali inatuhakikishia vipi kwamba kwenye awamu hii ya ajira itakayokuja tutapata walimu wa kutosha, hasa maeneo ya vijijini, ili kuweza kukidhi mahitaji ya watu wa Wilaya ya Chunya? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, moja, nikubaliane na yeye kwamba kweli hata Chunya nakufahamu vizuri. Eneo ni kubwa na kuna idadi ndogo sana ya walimu. Lakini kwa sababu ameleta hapa ombi na sisi kama Serikali kuititia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumelipokea hilo ombi na katika mgawanyo wa walimu 6,000 totalizingatia hilo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, taratibu zile za Bunge la Bajeti zimeshaanza, kwa hiyo, ntakuwa nakata mtu ye yeyote anayeuliza swali kwa kuchangia. Maswali yawe mafupi muda wetu wa maswali ni mfupi. Kwa hiyo, ukipewa fursa uliza swali, usianze kutoa mchango mrefu, ikiwa ni pamoja na wale wenye maswali yao ya msingi, uliza swali ulilojiandaa nalo.

Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na tatizo kubwa la walimu katika nchi nzima, na kuna walimu ambao wanajitolea kufanya kazi za kufundisha katika maeneo mbalimbali nchini, zinapojitokeza ajira walimu hawa hawapewi nafasi; je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha walimu wanaojitolea wanapewa kipaumbele pale nafasi zinapotoka? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vigezo ambavyo sasa hivi Serikali imekuwa ikitumia katika kuajiri walimu ni pamoja na kuzingatia walimu wote ambao wamejitolea kwa muda mrefu katika shule wanazofundisha. Kwa hiyo, hata katika hizi nafasi 6,000 ambazo tunakwenda kuzijaza zitazingatia vigezo hivyo. Na tumetoa maelekezo kwa maafisa elimu wote ngazi za wilaya kuleta taarifa za walimu wote wanaojitolea katika shule zao ili tuweze kuwazingatia katika ajira mpya. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yako ya msingi ameonesha kabisa changamoto ya walimu pamoja na kuajiri hawa waliopo bado changamoto itakuwepo, hasa kwenye walimu wetu wa sayansi. Na *technology* inakua, hasa matumizi yetu ya simu. Sasa kama Serikali, mna mkakati gani wa kuhakikisha sasa tuna-*link*, hasa zile shle zilizopo vijiini tukatumia hii mitandao ili wakawa na *access* ya wale walimu wanaofundisha wenzao mjini wapate elimu sawa na kule vijiini? Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba kwenye masuala haya ya TEHAMA bado kuna changamoto kubwa sana hususan vijijiini, na hata kwenye mitandao ya simu sisi wote ni mashuhuda kabisa kwamba *networking* ya mjini na vijijiini ni tofauti kabisa. Lakini sasa hivi Serikali tuna mitandao, tuna mfumo ambaa unawezesha walimu wa vijijiini na mijini kuwa na *access* iliyo sawa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba ameleta kama moja ya mapendekezo ama maoni na ushauri, basi sisi tutalipokea na moja ya kazi kubwa tutakazozifanya ni kuboresha mifumo iliyopo ili kuondoa hii changamoto ambayo ipo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi.

Na. 39

Upotevu wa Mapato Kwenye Zahanati

MHE. KENNETH E. NOLLO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mfumo wa ukusanyaji mapato wa *GoTHOMIS* kwenye zahanati kama ilivyo kwenye vituo vya afya ili kuondoa mwanya wa upotevu wa mapato?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Jimbo la Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Kieletroniki wa Uendeshaji wa Huduma za Afya (*Government of Tanzania Health Operations Management Information System - (GoTHOMIS)*) ni mfumo wa usimamizi wa uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya, ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa za wagonjwa na magonjwa, taarifa za malipo ya matibabu, taarifa za madawa na vifaa tiba na taarifa za huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu ulianzishwa mwaka 2016 na kuanza kusimikwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote. Mfumo umeboreshwa na kuunganishwa na mifumo mingine kama Mfumo wa Malipo ya Serikali (*GePG*), mfumo wa *NHIF* kwa ajili ya usimamizi wa madai na mfumo wa Kuomba Madawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (*ELMIS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Februari 2021, Mfumo wa *GoTHOMIS* umesimikwa katika vituo vya kutolea huduma 921, ikiwa ni hospitali 21 za mikoa, hospitali 82 za halmashauri, hospitali teule za wilaya 22, vituo vya afya 385 na zahanati 411. Kazi ya kusimika mfumo huu katika vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote nchini inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zimekuwa zikitumia vyanzo vyake vya ndani kusimika mtandao kiwambo na kununua vifaa vingine zikiwemo kompyuta na wataalam wa halmashauri kushirikiana na wataalam wa mikoa katika kusimika mifumo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya vituo vilivyofungiwa Mfumo wa *GoTHOMIS* na ambavyo vina miundombinu wezeshi kama mawasiliano ya *internet* vinatumia moja kwa moja Mfumo wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (*GePG*) na hivyo kuwezesha wapewa huduma kulipa moja kwa moja benki au kupitia

mitandao ya simu na hivyo kuwezesha makusanyo ya vituo kuongezeka na kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufungaji wa mifumo huu utaendelea kutekelezwa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, swali langu la msingi lilikuwa ni kwamba mfumo huu umeshafika kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kwenye zahanati 400, lakini tunajua nchi hii ina vijiji takribani 12,000, kwa maana hiyo na zahanati hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu la msingi ni kwamba zahanati nydingi sasa hawawezi kukusanya kwa kutumia ule mfumo na kinachotokea ni kwamba kunakuwa na upotevu wa mapato. Sasa swali langu la msingi ni je, Serikali haioni kwamba tutumie mfumo wa kawaida wa makusanyo ya kawaida (*POS*) ili tutoke kwenye upotevu ambao unaendelea sasa hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa dawa, hasa kwa watu wanaotumia *CHF*, kichecheo kikubwa imekuwa fedha za papo kwa papo, na hiyo inatokana na hii ya kwamba kuna upotevu wa fedha ambazo sasa mtu anakuwa analipa lakini fedha hazionekani.

Kwa hiyo, swali langu liko hapo, kwamba ni namna gani Serikali sasa inakuja kwamba ikiwezekana sisi tutumie *POS* kwa ajili ya kukusanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine...

NAIBU SPIKA: Umeshauliza maswali mawili Mheshimiwa.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Naibu Spika, *connection* kidogo, mfumo huu unatumia milioni 14 ku-install...

NAIBU SPIKA: Umeshauliza maswali mawili ya nyongeza, na ndiyo yanayoruhusiwa.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato, matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi lakini pia takwimu za huduma za afya katika vituo vyetu kwa kufunga mifumo ya *GoTHOMIS*. Na ni kweli kwamba bado kuna zahanati na vituo vya afya ambavyo bado havijafungwa mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Nollo kwamba kazi hii ya kufunga mifumo katika zahanati zetu ni endelevu. Kama ambavyo tunafahamu, hatujamaliza kujenga zahanati kwenye vijiji vyetu, na wala hatujamaliza kujenga vituo vya afya katika kata zetu lakini pia Hospitali za Halmashauri katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo *automatically* tutaendelea kutekeleza ufungaji wa mfumo huu katika vituo vipyambavyo vinaendelea kujengwa lakini pia katika vile vituo ambavyo bado havijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutumia mfumo wa *POS* halitatuwezesha kuboresha huduma za afya, kwa sababu lengo la mfumo wa *GOT-HOMIS* ni kuwa na taarifa za uhakika za magonjwa, matumizi ya dawa, aina ya matibabu yanayotolewa katika vituo. Kwa utaratibu huo hatuwezi kupata taarifa hizo kwa kutumia mashine za *POS*. Kwa hiyo naomba nimuhakikishie kwamba kama niliviotangulia kusema tumeshafunga katika vituo 921 nchini kote, na kila mwaka wa fedha tunaendelea kufunga mifumo

hii na tutaendelea kufunga ili viendelee kutoa huduma bora zaidi za afya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swalii pili, changamoto ya upatikanaji wa dawa kwa baadhi ya vituo. Ni kweli Serikali imeendelea sana kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vyetu vya huduma. Ukiilinganisha hali ya upatikanaji wa dawa mwaka 2015 na 2020/2021 tumepanda kutoka wastani wa asilimia 75 kwa dawa muhimu mpaka wastani wa asilimia 80 hadi asilimia 85 kwa dawa muhimu. Lengo la Serikali ni kufika angalau asilimia 95 kuelekea asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge; kwamba sisi ni sehemu ya Madiwani katika Halmashauri zetu, sisi ni wawakilishi wa wananchi katika Halmashauri zetu. Tuendelee kushirikiana na Serikali kusimamia ukusanyaji wa mapato ya uchangiaji wa huduma za afya katika vituo vyetu na kuhakikisha dawa zile kama ambavyo Serikali tunasimamia kwa karibu zinatumika na kuwafikia wananchi wote wakiwepo wanachama wa CHF. Kwa hiyo naomba nimuhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili litaendelea kuboreshwa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Changamoto ya upatikanaji wa dawa haiko kwenye zahanati na vituo vya afya peke yake bali hata katika Hospitali za Rufaa. Hospitali ya Rufaa ya Kitete Mkao wa Tabora ni miongoni mwa Hospitali ambazo zinachangamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa; na hii inatoka na...

NAIBU SPIKA: Swalii, swalii!

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:...je? Serikali ina mpango gani wa kuongeza kiwango cha dawa katika Hospitali ya Rufaa ili iweze kuwapatia wananchi wa Tabora huduma iliyobora ya dawa? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Dkt. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Hawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tunafahamu kwamba pamoja na uboreshaji wa upatikanaji wa dawa katika vituo vyetu katika Hospitali za Halmashauri na Hospitali za Rufaa za Mikoa ikiwepo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora kwa maana ya Kitete bado tunachangamoto ya upungufu wa dawa baadhi ya vituo. Ndio maana Serikali imeendelea kwanza kuongeza bajeti ya dawa, vitendanishi na vifaa tiba kila mwaka. Kwa mfano kwa miaka mitano iliyopita tulikuwa na billioni 30 sasa tuna billioni takribani 270. Pili, tumeendelea kuboresha sana ukusanyaji wa mapato ya fedha za uchangiaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba kwanza tunapunguza utegemezi wa vituo vyetu kwa bajeti ya Serikali Kuu kwa kuvipezesha kukusanya vizuri mapato ya uchangiaji lakini pia kununua dawa na vitendanishi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Hawa kwamba jambo hili Serikali tunalichukua, na tumeweka mpango mkakati wa kwenda kuboresha upatikanaji wa dawa katika vituo vyetu, zikiwezo Hospitali za Rufaa, ikiwepo Hospitali ya Kitete. Nimhakikishie kwamba tutahakikisha kadri ya bajeti na taratibu ambazo zimepangwa tunaboresha sana upatikanaji wa dawa kwa wananchi wa Tabora na katika Hospitali ya Kitete na nchini kote kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 40

Kuhuisha Miundo ya Utumishi kwa Kada Mbalimbali

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaendelea kuhuisha miundo ya utumishi kwa kada mbalimbali kwa kuwa utaratibu wa kuajiri na kupandisha vyeo ndani ya Utumishi umekuwa ukibadilika kulingana na majukumu ya kiutendaji na maendeleo ya kiuchumi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishina Utawala Bora Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa majibu. Mheshimiwa Mchengerwa pokea kwanza hayo makofi. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, yanamtosha nayapokea kwa niaba yake. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nimesimama hapa mara nyingi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kipindi cha tatu sasa cha uenyekiti wangu. Nanze kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonayo kwangu. Nimuahidi tu kwamba nitakwenda kuchapa kazi kwelikweli, kwenda kupunguza au kumaliza kabisa kero za watumishi wa umma wanyonge ambao ndio msingi wa Taifa letu hili. (*makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pili baada ya kumshukuru Mheshimiwa Rais, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rufiji, kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakiniamini wakati wote waliponichagua mwaka 2015, Iakini pia mwaka 2020 nilishinda kwa kishindo kwa kura ambazo hazipata kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Pwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mujibu wa Kanuni D. 6(2) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, Watumishi wa Umma huajiriwa na kupandishwa vyeo kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Kada husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mabadiliko ya kiutendaji pamoja na maendeleo ya kiteknolojia na kiuchumi Wizara mbalimbali zimekuwa zikihuisha miundo ya maendeleo ya kiutumishi ya kada mbalimbali zilizo chini yake kwa kuongeza sifa za kielimu, vigezo vya kuajiri na kupandisha vyeo watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kutambua mabadiliko ya kiutendaji na maendeleo ya kiteknolojia na kiuchumi, kuanzia mwaka 2014 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imekuwa ikiziwezesha Wizara Taasisi na Wakala za Serikali kuhuisha miundo yake ya maendeleo ya kiutumishi kadri ya mahitaji mapya yanavyojitokeza. Kwa mfano katika kipindi hicho miundo iliyoishwa ni pamoja na ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni, pamoja na Taasisi za Umma na Wakala wa Serikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt Alice Kaijage, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ili muundo fulani wa utumishi wa kada fulani uhuishwe lazima kwanza kada husika maombi yapelekwe Serikalini ndipo ifanyiwe kazi, kwa hiyo kama ikikwama kwenye meza fulani ya kamishna ina maana huo uhuishwaji unakwama. Kwa kuzingatia hivyo, je, Serikali haionti vema sasa kuwa na utaratibu wa kuwa na kipindi maalum cha kufanya uhakiki wa kada zote za Utumishi wa Umma na pia kufanya uhakiki wa Utumishi wa Umma pamoja na takwimu za Utumishi, hii yote kuleta usawa katika Utumishi wa Umma na pia kuboresha na kupandisha morale ya kazi ya watumishi? Mfano mzuri ni kada ya uhuishaji wa muundo wa kada ya maafisa kazi hawa *Labour Officers*.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa stahiki, stahili kwa watumishi pamoja na mafao yao hukokotolewa kuzingatia kiwango cha mshahara anacholipwa mtumishi. Kwa kuona umuhimu huu, je, Serikali sasa italipa kipaumbele suala zima la kuhakiki kada za kiutumishi kwa wakati? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kweye swalii la msingi kwamba Serikali itaendelea kuhuishaa miundo ya maendeleo ya utumishi kwa kadri ambavyo inaletwa kwenye Wizara yetu. Nitoe kumbukumbu tu kwa Mheshimiwa Mbunge aweze kufahamu kwamba kuanzia mwaka 2011 Serikali imekuwa ikuhishaa miundo ya maendeleo ya utumishi hasa kwa kada hii ya ualimu, ambapo ilifanya nyongeza ya madaraja kutokana na nafasi zao za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mwaka 2014 Wizara iliendelea kufanya namna hiyo na mwaka 2015 Wizara ya Fedha pia Wizara yetu iliendelea kuhuishaa miundo hasa kwenye kada mbalimbali ikizingatiwa baadhi ya watendaji kwenye kada hizo maafisa mipango, manunuzi, maaafisa

ugavi, wahasibu na wakaguzi. Nitoe rai tu kwa Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba Wizara yetu itaendelea kuhuisha miundo mbalimbali ya maendeleo ya utumishi kwa kadri itakavyoona inafaa. Kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba asiwe na hofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa swali la pili, kuhusu stahiki za mafao za watumishi kama ambavyo nimeulizwa. Katika utumishi wa umma stahiki na stahili za utumishi zimeanisha katika miongozo na nyaraka mbalimbali zinazotolewa kuhuisha mara kwa mara na Serikali. Nyaraka hizo huainisha makundi mbalimbali ya utumishi na stahiki wanazotakiwa kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, kwa mujibu wa kanuni ile ile Kanuni D. 6(2) za Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Kanuni hili iliwhahi kutolewa mwaka 2009; watumishi wa Umma kuajiriwa na kupandishwa vyeo na kubadilishwa kada (*Recategorization*) kwa kuzingatia sifa walizonazo na zinazooneshwa katika Miundo ya Maendeleo ya Utumishi katika kada mbalimbali zilizoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miundo ya Maendeleo ya Utumishi wa kada mbalimbali katika Utumishi wa Umma imeainisha ngazi za mishahara, kuanzia cheo cha kuingilia katika Utumishi wa Umma (*entry point*) hadi cheo cha mwisho kwa kila kada kulingana na kiwango cha elimu na kwa kuzingatia uzito wa majukumu ya kada husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako hili Tukufu kuwa Serikali itaendelea kuhuisha stahiki na stahili mbalimbali za watumishi wa umma pamoja na viwango vya mishahara ya kada mbalimbali kwa kuzingatia sera za kibajeti na uzito wa majukumu ya kada husika ili viweze kutumika kukokotoa mafao mbalimbali ya umma. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: ahsante sana. Mheshimiwa Janejelly James Ntate swali la nyongeza.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, lakini kumekuwa na nyaraka zitolewazo na miongozo na Menejimenti ya Utumishi wa Umma zinazokinzana kabisa na Sheria mama ya Utumishi wa Umma. Je, lini hizi nyaraka na miongozo vitafutwa ili sheria mama za kiutumishi zitumike?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi swali hili liko mahsus i kwa nyaraka fulani ambazo Mheshimiwa Mbunge hajazitaja ni zipi na zinakinzana na sheria zipi, kwa hivyo utakuwa na uhuru wa kutaka kujibu ama nikupe fursa Mbunge akaandae swali la msingi ili nyaraka tuzijue ni zipi zinazokinzana na sheria. Uko na uhuru kama unayo majibu karibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri kwamba tunapokuwa na nyaraka basi sheria ndiyo hufuata mkondo wake. Tunapokuwa na sheria ambayo inayokinzana na Katiba ni dhahiri Katiba inakuwa juu ya ile sheria, lakini tunapokuwa na nyaraka inakinzana na sheria basi sheria ndiyo inafuata mkondo wake.

Kwa kupitia swali lako kama ulivyoliuza nitapata fursa ya kukaa na watendaji na kuangalia zile nyaraka zote ambazo zinakinzana na sheria iliyopo na tutafanya maamuzi kutokana na namna. Lakini pia ikikupendeza nitaomba nipaye nyaraka hizo ili niweze kuzipitia na kushaurina na watendaji katika Wizara yangu. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Sawa, kwa hivyo Mheshimiwa Mbunge unaouhuru wa kuleta swali mahsus au kuzipeleka kwa Mheshimiwa Waziri hizo nyaraka ili zikapitiwe.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 41

HitajI la Umeme Kata za Handa, Lalta, Sanzawa na Mpendo

MHE. KUNTI Y. MAJALA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasambaza umeme katika Kata za Handa, Lalta, Sanzawa na Mpendo?

NAIBU SPIKA: Hizi kwa niaba huwa zinaleta changamoto sana, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swalI la Mheshimiwa Kunti Yussuf Majala, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo havijapata umeme katika Wilaya ya Chemba vikiwemo vijiji nya Kata za Handa, Lalta, Sanzawa na Mpendo vitapatiwa umeme kupitia mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili ulioanza kutekelezwa mwezi Machi, 2021 na utekelezaji wa mradi huu utakamilika ifikapo Desemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi kwa Wilaya ya Chemba zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 681.4, msongo wa kilovoti 0.4 umbali wa kilomita 50, ufungaji wa transfoma 50 za 50kVA, pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 1,100 kwa gharama ya takriban Shilingi Bilioni 27.3.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Yussuf Majala swalI la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kunipatia niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata hizi ilikuwa zipatiwe umeme *REA* awamu ya pili, lakini mpaka tunamaliza *REA* awamu ya pili kata hizo hazijapatiwa umeme. Je, Serikali inawahakikishiaje watanzania wa Wilaya ya Chemba kwenye kata hizi nilizozitaja, kwamba kwenye awamu hii ya *REA* awamu ya tatu iliyoanza Machi, 2021 kwamba vijiji hivi na kata zake hazitakwenda kukosa umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini swalı langu la pili, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya ukatikaji wa umeme kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Chemba na kwenda kusababisha uharibifu wa mali za watumiaji wa umeme. Je, Serikali sasa haion ni wakati wa kuanza kulipa fidia kutokana na tatizo la ukatikaji wa umeme bila taarifa? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tamko la Serikali kwa niaba ya Serikali, kwamba tunawahakikishia wananchi wote wa Tanzania kwamba vijiji vyote ambavyo vilikuwa havijapata umeme vilivyoko katika kata pamoja na hivyo alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge kwamba vitapelekewa umeme katika awamu ya pili ya mzunguko wa tatu wa *REA*, bila kuacha kijiji hata kimoja. Hiyo ni *commitment* ya Serikali na tayari mradi umeanza na vijiji vyote vilivyokuwa vimebakia takriban 1,900 vimechukuliwa katika mradi huu na vitapatiwa umeme.

Mheshimiwa naibu Spika, timekuwepo changamoto kadhaa katika awamu zilizotangulia na zile baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa yamebaki katika awamu hii ya tatu mzunguko wa pili hakuna hata kimoja kitakachobaki; na hiyo ni *commitment* ya Serikali. Kwa hiyo Mheshimiwa namuhakikishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Chemba Mheshimiwa Monni amekuwa naye mstari wa mbele katika kufuatilia umeme wa wananchi wake; na sisi kama Wizara na Serikali tutahakikisha kwamba tunapeleka umeme katika mazingira hayo kwa kushirikiana na Wabunge wa maeneo yote. Ndio maana sasa swali liloulizwa limejibowi lakini pia na wengine wanaendelea kufuatilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika swali la pili alizungumiza kuhusu kukatika kwa umeme na nizungumzie katika eneo la Chemba. Yapo matatizo ambayo yanapelekea umeme kukatika; na kwa eneo la Dodoma tunalo tatizo moja kubwa sana. Udongo wa Mkoa wetu wa Dodoma ni udongo tepetepe inaponyesha mvua, kwa hiyo nguzo zimekuwa zikianguka na kulala panapokuwa panatokea hali ya hewa yenye mvua nyingi na udongo kuwa tepetepe. Na katika kulitatu hilo tumehakikisha basi tumeanza kuweka vitu vinavyoitwa *concrete poles* ambazo ni nguzo za zege zinaweza kwenda chini zaidi na zitahimili mzingo kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa Jimbo la Chemba umeme unaokwenda Chemba unaenda katika *sub-station* yetu ya Babati unapita Kondoa, unakwenda Chemba, unakwenda Kiteto, unakwenda mpaka Kilindi, kwa hiyo ni parefu sana. Kwa Mkoa wa Dodoma imeamuriwa kwamba zijengwe *sub-station* nne zinazoitwa *ring circuit* ambazo zitakuwa zikiuzunguka mji wa Dodoma na zitapunguza mahitaji ya umeme kwenye msururu mrefu. Kwa mfano kutoka Kondoa kwenda Chemba kuna kilometra kama 30. Sasa ile Kiteto na Kilindi zitaondolewa kwenye mstari huu ili umeme unaokwenda Chemba uwe wa uhakika na uuhudimie wale wananchi walioko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumekuwa tukiwaelekeza wenzetu waendelee kutoa taarifa kwa wananchi wao ili wawze kupata taarifa kwamba umeme utakatika na wajiandae kwa mazingira kama hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita Waziri wa Nishati alitembelea Kituo cha Afya cha Makorongo na kwa sababu ya umuhimu wa Kituo kile cha Afya alielekeza umeme uwekwe. Kituo kile kinahudumia Kata tano lakini mpaka leo hii kituo kile hakijapata umeme. Naomba sasa kujua, ni lini Wizara itatekeleza agizo lile la Waziri wa Nishati na Madini? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, Mbunge Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Waziri yalitakiwa yatekelezwe na kwa vyovyote vile yatakuwa katika hatua za utekelezaji kwa sababu uunganishaji wa umeme siyo jambo la siku moja. Naomba tulichukue na tukalifanyie kazi na kuhakikisha katika muda mfupi umeme unawashwa katika Kituo hicho cha Afya kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata 29 za Wilaya ya Mbozi, Kata tatu za Bara, Kilimpindi na Nyimbili bado hazijapelekewa umeme. Naomba kufahamu ni lini Serikali itapeleka umeme katika kata hizo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shonza kuhusu kupeleka umeme katika kata alizozitaja katika Jimbo la Mbozi. Katika Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili wa *REA* ilioanza Machi tutahakikisha tunapeleka umeme maeneo yote ambayo yalikuwa hayajapata umeme. Hivyo na yeye atakuwa mmojawapo katika wale watakaopata umeme katika awamu hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tunduru Kusini lina matatizo makubwa sana ya umeme hasa vijiji vyake zaidi ya asilimia 70 bado havijapata umeme. Je, ni lini Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu B utaanza katika Jimbo la Tunduru Kusini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru kwa kusema ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili inazo jumla ya *Lot 37* za kupelekeza umeme katika maeneo yetu ya vijiji. Katika hiso *Lot 37*, ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tayari maeneo yote yaliyotakiwa kupelekewa umeme ambayo hayakuwa na umeme yamechukuliwa katika hiso *Lot 37* na tayari tumeshazindua kuanzia Machi 15, pale Manonga na tunaendelea kuwatuma wakandarasi kuripoti katika maeneo yetu husika.

Mheshimiwa Natibu Spika, nikumbushie tu, agizo ambalo tumeshalitoa kwamba wakandarasi wote wanaenda kupeleka umeme katika maeneo hayo pamoja na maeneo mengine watakayopiga ripoti. Wapige ripoti kwa Waheshimiwa Wabunge ili kuwaonesha maeneo ambayo yanahitaji umeme kwa haraka na kwa ufasaha zaidi ili kuweza kushirikiana kwa pamoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, itapunguza yale maswali ambayo tunaulizwa kwa sababu Waheshimiwa Wabunge watakuwa wamepata uhakika kwamba katika eneo lake mkandarasi anafika. Kwa hiyo, niwasisitiza wakandarasi wafike katika maeneo ya Waheshimiwa Wabunge na kutoa taarifa ili Waheshimiwa Wabunge wapate hiyo taarifa na sasa kazi iweze kuendelea vizuri.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Swali Na. 42, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, Sasa aulize swali lake.

Na. 42

Tatizo la Umeme katika Jimbo la Mbagala

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza transforma ya 100 MVA katika *substation* ya Mbagala ili kuondoa tatizo la kukatika umeme katika Jimbo la Mbagala?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge Wa Mbagala, kama Ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mbagala msongo wa kilovoti 132/33 chenyé uwezo wa *MVA* 50 ulikamilika na kuanza kufanya kazi rasmi tarehe 25 Februari 2018, kupitia utekelezaji wa mradi wa *TEDAP* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Baada ya kituo hiki kuanza kufanya kazi, hali ya upatikanaji umeme katika eneo la Mbagala uliimarika ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho cha kupoza umeme, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza mradi wa kuboresha vituo vya kupoza umeme vya Kinyerezi na Mbagala kwa kufunga transfoma zenye uwezo wa *MVA* 50 kwa kila kituo pamoja na kuongeza uwezo wa njia ya kusafirisha umeme ya kilovoti 132 kutoka Kinyerezi hadi Mbagala kupitia Gongo la Mboto. Mradi huu unatarajia kutekelezwa kwa kipindi cha mlezi kumi kuanzia Juni, 2021 na kukamilika Aprili, 2022. Gharama ya mradi huu ni takriban Dola za Marekani milioni 9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huu, kutaboresha hali ya upatikanaji umeme katika maeneo ya Mbagala na maeneo mengine ya jirani yanayopatiwa umeme kutoka katika kituo hicho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chaurembo swalii la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa umeme unaozalishwa katika *Sub-station* ya Mbagala ni chini ya asilimia 20 tu unaotumika Mbagala na asilimia zaidi ya 80 unaenda kutumika Mkuranga. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga *sub-station* kule Mkuranga ili kuwapoza watu wa Mbagala waendelee kutumia umeme wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa Jimbo la Mbagala ndio Jimbo ambalo lina watumiaji wengi wa umeme ukilinganisha na mikoa mingine ya Ki-*TANESCO*, je,

Serikali ina mpango gani wa kulifanya Jimbo la Mbagala kuwa mkoa wa Ki-TANESCO?

NAIBU SPIKA: Mheshiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mbagala tunayo *Sub-station* inayozalisha *Megawatts* 48 na *Megawatts* 40 zinakwenda Mkuranga kama alivyosema kwa sababu kuna viwanda vingi sana pale zinabaki *Megawatts* 8 tu. Tunapata umeme wa Mbagala kutoka Ubungo kuititia Gongolamboto lakini tunapata umeme mwингine kutoka Kurasini. Pale Kurasini tunapata *Megawatts* kama 26 hivi, zinazoenda kujazia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba umeme unapungua katika eneo la Mbagala kwa sababu mahitaji yamekuwa makubwa. Hata hivyo, kama tulivyosema kwenye swalii la msingi, tunaongeza uwezo wa kituo hicho cha Mbagala kwa kuweka *MVA* 50 lakini pia cha Kinyerezi ambacho pia kitaleta umeme pale Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii hilohilo ni kwamba tayari Serikali inafanya *feasibility study* ya kujenga *sub-station* nyingine kumi na kuziboresha nyingine kadhaa katika maeneo yetu ya Tanzania. Mkuranga kwa sababu ya umuhimu wake wa kuwa na viwanda vingi sana ni eneo mojawapo ambalo litapelekewa *sub-station* katika siku za hivi karibuni ili kupunguza mzigoto mkubwa ambao vituo vyetu vya Mbagala na Kinyerezi vinaupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii la pili, Mkoa wa Dar es Salaam mpaka sasa unayo mikoa ya ki-TANESCO minne na hivi karibuni yamekuja maombi ya Kigamboni kuwa ni Mkoa wa ki-TANESCO na bado yanafanyiwa kazi. Niombe kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amelisema,

tutaenda kuangalia vigezo kwa sababu kuna kuangalia idadi ya wateja, makusanyo, *line* ya umeme mkubwa na mdogo katika eneo husika, vigezo vikikidhi basi, mamlaka husika zitaamua na huduma zitapelekwa karibu zaidi na wananchi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji – Bonde la
Mto Mkomazi**

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya muda mrefu ya Mhe. Rais ya ujenzi wa Bwawa la umwagiliaji kwenye Bonde la Mto Mkomazi?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein M. Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali Mheshimiwa Timetheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Mkomazi ipo katika Kijiji cha Manga Mikocheni, Kata ya Mkomazi, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe. Skimu hiyo ina jumla ya hekta 5,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ambapo kati ya hizo, hekta 200 zimeendelezwa kwa kujengewa miundombinu ambazo zilifadhiliwa kutokana na fedha za ndani za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Ofisi ya Tume ya Umwagiliaji ilifanya mapitio ya upembuzi yakinifu ya awali na kubaini hitaji la Sh.3,379,000,000 ili kuendeleza

bonde hilo. Kati ya fedha hizo Sh.4,041,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na Sh.2,337,999,000 ni za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Ujenzi wa Skimu ya Mkomazi pamoja na bwawa lake upo katika Mpango wa Umwagiliaji wa mwaka 2018 (*National Irrigation Master Plan*). Mkakati mpana wa Serikali ni kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili ifikapo mwaka 2025 tuwe na uwezo wa kumwagilia hekta milioni 1.2 ambapo Skimu ya Mkomazi ni mojawapo ya skimu zitakazotekeliza katika mkakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji wenye lengo kufanya matengenezo ya miundombinu na kujenga miradi mpya. Pia Wizara imeelekeza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuanzia sasa kujenga miradi kwa kutumia wataalam wa ndani kwa utaratibu wa *force account* kwa Mfumo wa Usanifu na Ujenzi (*Design and Build*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake lakini nina nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ahadi ya ujenzi wa bwawa na miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo hili ni ya muda mrefu tangu wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliuhibsha ahadi hiyo wakati wa kampeni zake za mwaka 2020. Eneo hili lina maji mengi ambayo yanaleta mafuriko kwenye Kata zaidi ya tano. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye majibu yake ni sehemu ya mpango kabambe, swali langu nataka kujua, ni lini ahadi hii itatekelezwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wilaya ya Korogwe inaongoza kwa fursa na mazingira mazuri ya kilimo cha umwagiliaji. Serikali haioni sasa ni wakati sahihi kuboresha skimu zilizopo kwenye Tarafa za Magoma na Mombo ikiwemo Skimu ya Kwamkumbo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri

waliitolea ahadi wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Februari, 2021?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini tutaijenga Skimu ya Mkomazi, *commitment*ya Wizara na Serikali ni kwamba katika kipindi cha miaka hii mitano kwa maana ya *plan* ya 2025, Skimu ya Mkomazi ni moja kati skimu ambazo Serikali itazijenga. Nataka nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni moja kati ya skimu tutakayoipa *priority* kwa sababu kila mwaka maafa yanayotokea na upotevu wa maji katika eneo hilo ni makubwa sana kuna *potential* kubwa ambayo na sisi tunafikiri kwamba ni muhimu tukaifanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi tulioitoa tukiwa katika ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu ipo palepale. Tuliahidi kwamba baada ya mvua hizi wataalam wetu wa Wizara ya Kilimo kwa maana ya wataalam wa Tume ya Umwagiliaji watapeleka vifaa kwa ajili ya kwenda ku-repair ile skimu ambayo ilikuwa imeathirika. Ahadi ile ipo palepale, naomba avumilie, *Inshaallah*, hivi karibu wataalam wetu watakwenda.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Katika Jimbo la Manyoni Mashariki tuna bwawa la umwagiliaji linalojulikana kama Mbwasa *Irrigation scheme*. Tayari ilishafanyika upembuzi yakinifu yaani *feasibility study* zaidi ya miaka 10, tulisaidiwa na watu wa JICA na iligharimu shilingi milioni 200. Napenda kujua sasa *commitment* ya Serikali ni lini sasa ujenzi wa bwawa hili la umwagiliaji ambalo litasaidia wakulima katika kata zaidi ya

tano wa kilimo cha mpunga litaanza kujengwa na Serikali? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA : Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tathmini ya mabwawa na maeneo *potential* mengi ambayo yamefanyiwa usanifu na upembuzi yakinifu kama Wizara sasa hivi tunayafanyia *auditing* kwa sababu maeneo mengi ukiangalia gharama ambazo zilisanifiwa na hali halisi ya mahitaji ya fedha inayohitajika hazina uwiano.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba watupe nafasi katika bajeti tutakapokuja mwaka huu tutatoa mwelekeo wetu wa umwagiliaji *clearly* ambao kama Serikali tumeamua kwenda nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya eneo ambalo tunalolipa kipaumbele ni kufanya *audit* kuangalia kweli gharama zinazohitajika katika eneo hili ni halisi na kweli tutapata *value for money* katika eneo hilo. Njia nyngine ni kwamba miradi mingi ya umwagiliaji tutakayofanya sasa hivi tutatumia *force account* na katika bajeti itakayokuja mtaona tutatenga fedha kutokana na Mfuko wa Maendeleo wa Umwagiliaji ambao utakuwa ni chanzo chetu wenyewe kama Wizara bila kutegemea fedha kutoka Hazina katika Mfuko Mkuu. Fedha hizi tutazielekeza katika kununua vifaa ili Tume yetu ya Umwangiliaji iwe na *capacity* ya kwenda kujenga mabwawa bila kutumia wakandarasi na tutatumia *force account* kwa kuishirikisha halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wasubiri, baada ya bajeti tutakuwa tuna mwelekeo sahihi wa sekta yetu ya umwagiliaji.

NAIBU SPIKA : Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Skimu ya Pawaga, Ruaha Mbuyuni na Mlalo kule Lushoto tuliahidiwa kwamba zingetengewa fedha baada ya kuharibiwa na mafuriko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mpaka sasa ninavyozungumza wenzetu wa Pawaga na Ruaha Mbuyuni wameshapewa fedha lakini sisi milioni 30 ambazo zimeahidiwa na Tume ya Umwagilajiji mpaka sasa hazijafika katika Halmashauri ya Lushoto kwa ajili ya Skimu ya Mlalo. Je, Serikali inatoa *commitment* gani kwa pesa hizi kwenda katika Skimu hii ya Mlalo?

NAIBU SPIKA : Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Skimu za Mnaro, Pawaga na Ruaha zilikuwa zimeathirika kwa kiwango kikubwa na mvua za mwaka jana na mvua zilizoendelea mwaka huu. Kama Wizara tuliamua kwamba badala ya kupeleka fedha tutumie *equipment* tulizonazo wenyewe za Tume ya Umwagilajiji na kutupunguzia gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Skimu za Pawaga na Ruaha zimeshafanyiwa kazi, Skimu inayofuatia kupeleka vifaa ni ya Mlalo ambayo anatoka Mheshimiwa Shangazi na naamini kwamba kabla ya msimu ujao wa mvua tutakuwa tumeshairekebisha na tutatumia vifaa vyetu na Tume watapeleka vifaa wenye kwenda kufanya hiyo kazi badala ya kupeleka fedha. Kwa sababu tukitumia *force account* tutatumia nusu ya bajeti iliyokuwa imeletwa na halmshari yake.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na Wizara ya Maji, niwatangaze wageni wa Mheshimiwa Spika halafu tutaendelea na utaratibu wetu.

Waheshimiwa Wabunge, leo Mheshimiwa Spika anao wageni wambao wako jukwaa la Spika, nao ni wageni sita ambao ni Wabunge wa Bunge la Uganda na Wajumbe wa Bunge la Afrika yaani Pan African Parliament wakiongozwa na Mheshimiwa Jacquiline Amongin, karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jacquiline Amongin ameongozana na Mheshimiwa Bangirana Anifa Kwooya, karibu sana. Yupo pia Mheshimiwa Felix Okot Ogong, karibu sana.

Yupo pia Mheshimiwa Elijah Okupa, karibu sana. Yupo pia Mr. James Bamuwamye, huyu ni Afisa Itifaki, karibu sana. Yupo pia Ms. Peruth Lilian Najjuma ambaye ni Katibu wa Msafara. (*Makofi*)

Karibuni sana wageni wetu kutoka Bunge la Uganda. Sasa mtakuwa huru kwenda kuonana na Mheshimiwa Spika. Naamini sasa mnakifahamu Kiswahili kwa sababu imeshakuwa lugha rasmi ya Afrika Mashariki, kwa hiyo, sina haja ya kuongea Kiingereza. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu sasa aulize swali lake.

Na. 44

Ujenzi wa Bwawa Kata ya Mikangaula – Nanyumbu

MHE. YAHYA A. MHATA aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ya ujenzi wa bwawa la maji katika Kata ya Mikangaula Wilayani Nanyumbu itatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji,
Engineer Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali iliahidi kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Nanyumbu kwa kujenga mabwawa katika Vijiji vya Mikangaula, Mchiga, Maratani, Chilunda na Nangova.

Katika kutekeleza ahadi hiyo, Serikali imeanza ujenzi wa bwawa katika Kijiji cha Maratani ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 95 na utakamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2021. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa tuta, *spill-way*, chemba za kutolea maji na kupokea maji, birika la kunyweshea mifugo na kituo kimoja cha kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, *RUVASA* Wilaya ya Nanyumbu imepanga kuanza kazi za ujenzi wa mabwawa ya Mikangaula na Chilunda.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, swalii la nyongeza.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na andiko la huu mradi pamoja na kujenga bwawa, ni kuhakikisha kunakuwa na mtandao wa maji kutoka kwenye bwawa kuelekea Vijiji vya Lipupu, Maratani, Mchangani A na Malema na baadhi ya Vijiji vya Kata ya Mnjanje:-

Swali je, ni lini utekelezaji wa uwekaji wa miundombinu ya maji utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili. Ahadi hii ya kujenga bwawa katika Kata ya Mikangaula ilitolewa tarehe 28/07/2011 na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Mrisho Jakaya Kikwete. Swalii langu; ni miaka 11 ndiyo mradi huu unatakiwa kutekelezwa:-

Je, Wizara haioni wakati umefika ahadi ya viongozi wa juu hasa Marais wetu ikachukuliwa kama ni agizo na ikatekelezwa haraka iwezekanavyo, badala ya kusubiri miaka 11 ndiyo itekelezwe? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mtandao wa maji tunaelekea sasa kwenda kuutekeleza. Katika kutengeneza mabwawa, tunaanza kuhakikisha uhakika wa chanzo cha maji ambapo sasa bwawa limeshafika asilimia 95 na sasa hivi kazi zitakazofuata ni kuukamilisha. Hii 5% iliyobaki kufikia mwisho wa mwezi wa Tano au kabla ya kumaliza mwaka huu wa fedha ni kuona kwamba tunakwenda kusambaza mitandao ya mabomba kuelekea kwa watumiaji wetu wote wa Nanyumbu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swalii lake la pili, amesema mradi umeanza tarehe 28/07/2011. Kama wote tunavyokumbuka, miradi hii kwa kipindi hicho ilikuwa chini ya Halmashauri zetu za Wilaya. Kwa hiyo, wale wenzetu kidogo walishindwa kumaliza miradi hii na ndiyo maana RUWASA ikaanzishwa. Sote tunafahamu RUWASA sasa hivi ina mwaka mmoja na miradi korofii yote kama huu imekuwa ikifanikiwa kwa kuweza kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge napenda tu kukuhakikishia kwamba tunakwenda kutimiza ahadi hii kwa kutumia RUWASA na wote tunafahamu namna RUWASA ambavyo wamekuwa wakamilisha miradi chechefu, kwa hiyo, na mabwawa haya pia yanakwenda kukamilika. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Uhaji wa Huduma ya Zimamoto Mji
Mdogo wa Katoro**

MHE. TUMAINI B. MAGESSA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya Zimamoto katika Mji Mdogo wa Katoro ili kupunguza hatari ya moto iwapo utatokea ikizingatiwa kwamba kuna ongezeko kubwa la wafanyabiashara katika Mji huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatoa huduma za uzimaji moto na uokoaji katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Kutokana na ufinyu wa bajeti na upungufu wa rasilimali watu na vifaa, Mji Mdogo wa Katoro utaendelea kupata huduma za zimamoto na uokoaji kutoka katika Kituo cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kilichopo Geita Mjini mpaka hapo Jeshi litakapopata rasilimali za kutosha kuweza kuwa na Kituo katika Mji Mdogo wa Katoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa Elimu ya Kinga na Tahadhari ya Moto katika Mji Mdogo wa Katoro ili kupunguza majanga ya moto yanayoweza kutokea katika mji huo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa vile sasa Kituo cha Geita sasa kitakuwa kinahudumia mkoa mzima, nami ninachojua ni kwamba pale Geita hata gari la zimamoto halipo: Je, ni lini Geita itapata gari la Zimamoto ili iweze kuhudumia mkoa mzima kutoka kwenye *center* moja ya Geita? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa vile kutoka Geita ni mbali na Katoro, ni lini sasa Kituo cha Polisi cha Geita kitapewa gari la Polisi ili liweze kuwashudumia wananchi wakati wakisubiri huduma ya gari la zimamoto kutoka Geita ili mali zao zisiporwe wala kuharibika baada ya moto kutokea? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Geita kuna jumla ya magari manne ya zimamoto. Magari haya ni mazima na yanafanya kazi katika mkoa huo. Kwa bahati nzuri, pia sasa Serikali imeshafikiria kupeleka gari la zimamoto katika mji mdogo wa Katoro. Kitu cha msingi ambacho namwomba Mheshimiwa Mbunge, aendelee kustahimili kidogo, Serikali tumo mbioni kupeleka gari la zimamoto katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba wakati wao wanaendelea kustahimili, zipo njia mbadala ambazo tunazitumia kuhakikisha kwamba itakapotokea majanga hasa ya moto na mengine, wananchi hawa wanaweza kupata msaada wa haraka. Hivi karibuni tulifunga mkataba ama makubaliano na wale skauti, kwamba watusaidie

kuendelea kutoa taaluma, washirikiane na Jeshi la Zimamoto ili kuhakikisha kwamba taaluma inaenea na majanga yanapotokea wanaweza kupata msaada wa haraka. Sisi kama Serikali kupiditia Jeshi la Zimamoto pia tunaendelea kutoa taaluma. Kikubwa ambacho tumesisitiza hasa kwa Jeshi la Zimamoto, waweze kuwahi kwenye matukio kwa haraka panapotokea majanga haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la Mheshimiwa, ni lini sasa tutapata gari la Polisi ambalo litakwenda angalau kuweza kutoa huduma? Katika Mji Mdogo wa Katoro, Kituo cha Polisi cha Katoro tayari gari la Polisi lipo, ipo gari ya *One Ten*, ambayo inatumika, sema tu, kwa kweli gari ni ya muda mrefu, limechakaa. Tunachowapongeza Jeshi la Polisi, Geita wameshaomba magari katika Jeshi la Polisi ili waweze kupelekewa magari hayo yaweze kuwasaidia katika harakati mbalimbali za *ku-serve maisha ya jamii*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Mikakati ya Kuanzisha Viwanda vya Dawa na
Vifaa Tiba Nchini**

MHE. MUSSA R. SIMA aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuanzisha viwanda vya dawa na vifaa tiba hapa nchini ili kuacha na kuagiza vifaa hivyo nje ya nchi?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba ina jumla ya viwanda 14 ambapo viwanda 12 vinatengeneza dawa za binadamu viwanda viwili dawa za mifugo; na kiwanda kimoja kinatengeneza Vifaa Tiba. Wizara imeendelea kuchukua hatua za makusudi ili kuhakikisha Sekta hiyo inaongeza uwekezaji kwenye Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo inakwenda sambamba na kuongeza ufanisi wa viwanda vilivyopo ili kufikia asilimia 60 ya uwezo wa uzalishaji wa dawa na vifaa tiba nchini ifikapo mwaka 2025. Hatua hizo ni pamoja na kuunda Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba (*National Pharmaceutical Coordination Committee - NPCC*); na kuweka vivutio vya uwekezaji kwa lengo la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na Nje ya Nchi ili kuwekeza katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lli kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo, Serikali imeondoa VAT kwenye vifungashio vya dawa zinazozalishwa nje na ndani ya nchi; imeshusha kodi ya mapato kwa asilimia 30 ambayo imesaidia kuhamasisha uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda kwa muda wa miaka miwili kwa miradi mpya ya viwanda vya dawa na kuweka upendeleo maalum kwa ununuzi wa dawa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kuitia *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kufuatilia uwekezaji na ambapo sasa hivi kuna viwanda 11 vinavyoendelea na ujenzi wa Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba na ujenzi umefikia katika hatua mbalimbali. Lengo la Serikali ni kuokoa fedha zinazotumika kuagiza dawa na vifaa tiba hivyo kutoka nje ya nchi kwa kuzalisha na kuwezesha upatikanaji wa uhakika wa dawa hizo nchini na hivyo kuendelea kutengeneza ajira hapa nchini. Aidha, lengo hilo linakusudia kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa ni suala la kipaumbele wakati wowote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, swali la nyongeza.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na uwepo wa viwanda hivyo 14 alivyovitaja, lakini bado Serikali inaagiza dawa na vifaa tiba kwa asilimia 80 kutoka nje. Je, tatizo ni ubora wa dawa zinazotolewa nchini ama ushindani wa kibiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali imesema ifikapo mwaka 2025 itafikia asilimia 60, napenda kujua tu, sasa hivi tuko asilimia ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Tanzania bado hatujajitosheleza katika uzalishaji wa dawa kwa maana ya kuwa na viwanda vichache ambavyo vinazalisha dawa na vifaa tiba kwa ajili ya matumizi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala siyo ubora, ni uwezo wetu ambao bado haujakidhi mahitaji ya ndani. Suala la ushindani ni suala lingine kwa sababu ushindani upo hata katika bidhaa ambazo tumejjitosheleza, lakini *specifically* kwenye hili bado uwezo wetu wa kuzalisha ndani ni mdogo, ndiyo maana tumelenga kuhamasisha kuititia vivutio mbalimbali ili tuwe na wawekezaji wengi zaidi wanaowekeza katika viwanda vyatengeneza dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiasi ambacho kinaagizwa sasa, ni kweli hatujafikia uwezo wa kutengeneza asilimia zote za dawa kwa maana ya asilimia 100, bado tunaagiza zaidi ya asilimia 80 kutoka nje. Kwa hiyo, bado

lengo letu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kufikia asilimia ya uzalishaji ifikapo mwaka 2025.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa naomba kuuliza; je, Serikali ina mpango gani ya kufufua Kiwanda cha *Machine Tools*, kiwanda ambacho kinatengeneza vipuri kwa ajili ya viwanda vingine na pia vinatengeneza na kuunda mashine za kusaidia viwanda vingine vidogo na vikubwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo mnajua, Serikali sasa ina mpango wa kuendeleza uchumi wa viwanda. Kiwanda cha (*Kilimanjaro Machine Tools – KMTC*) ni moja ya viwanda muhimu sana kwa maana ya *basic industries* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaamua kufufua kiwanda hicho. Katika bajeti ya mwaka huu tumetenga zaidi ya shilingi billioni 1.6 kwa ajili ya kujenga kinu cha kuyeyushia chuma (*foundry*).

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwamba kiwanda hicho sasa kinaenda kufanya kazi kwa sababu tutakuwa na uwezo wa kuyeyusha chuma na kuzalisha vipuri ambavyo vinahitajika katika viwanda vingine kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Viwanda hapa nchini. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya*, Mbunge wa Nyasa, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Nape Nnauye.

Na. 47

Gharama za Kuhamisha Umiliki wa Ardhi

MHE. NAPE M. NNAUYE K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha gharama za kuhamisha umiliki wa ardhi ambazo siyo rafiki hasa kwa wanyonge na kusababisha wengi kuwa na miliki bubu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swalii hili naomba uniruhusu nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa fursa ambayo amenipatia kuweza kuendelea kulitumikia Taifa hili, lakini zaidi sana nimshukuru Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini tena na kutuamini Wizara yetu na kuendelea kutuweka pale ili tuendelee kuitumikia Serikali hii. Namshukuru sana kwa imani hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba sasa nijibu swalii la Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya*, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamishaji wa milki za ardhi huzingatia Sheria ya Ardhi (Sura Na. 113), Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura Na. 334), Sheria ya Ushuru wa Stempu (Sura Na. 189) na Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura Na. 332) ambayo inahusika na Kodi ya Ongezeko la Mtaji. Kwa mantiki hiyo, Wizara yangu inasimamia gharama za Ada ya Uthamini, Ada ya Upekuzi katika Daftari la Msajili, Ada ya Maombi ya Uhamisho wa Milki na Ada ya Usajili ambazo ni gharama nafuu na wananchi wa kawaida wanaweza kuzimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika nyakati tofauti imekuwa ikiboresha gharama za uhamishaji na umilikishaji wa ardhi. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/2019 gharama za tozo za mbele yaani (*premium*) ilipunguzwa kutoka 7.5% kwenda 1% ya thamani ya ardhi ambayo hutozwa mara moja tu wakati wa umilikishaji kwa maeneo ya urasimishaji mijini na hadi 2.5% kwa maeneo mengine. Aidha, Wizara pia imeboresha gharama za urasimishaji kwa kupunguza kutoka shilingi 250,000/= hadi shilingi 150,000/= na katika Halmashauri nyingine wanatoza shilingi 50,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazotekelezwa na Serikali zinalenga kuboresha gharama za umilikishaji na uhamishaji wa milki kuwa rafiki hususan kwa wanyonge. Aidha, kwa kuhakikisha kuwa ada na tozo zinakuwa rafiki na zinazingatia maoni ya wananchi, Serikali sikivu ya Awamu ya Tano kuititia Kamati Maalum (*Task Force on Tax Reform*) kila mwaka inapitia sheria za kodi ili kufanya maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Serikali iko tayari kupokea maoni na ushauri wa wadau kuhusu viwango vya tozo zinazohusu uhamisho wa milki za ardhi na tozo nyingine zinazohusu Sekta ya Ardhi kwa ujumla ili kuboresha huduma kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nape Nnauye, swalii la nyongeza.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza, kwa kuwa umilikaji halali wa ardhi utaisaidia Serikali katika kukusanya mapato kwa sababu wamiliki halali watalipa kodi vizuri na kwa kuwa kwa uzoefu uliooneshwa kutokana na shida ya uhamishaji wa umiliki unaonesha kwamba wananchi wa kawaida wanashindwa kumudu gharama. Je, Serikali iko tayari ikiwezekana kufuta kabisa gharama za kuhamisha umiliki ili wamiliki waweze kumiliki na kulipa kodi kwa Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swal i la pili, Serikali ya Awamu ya Tano kuitia Rais hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa maombi ya wananchi wa Mtama walifuta umiliki wa shamba la Maumbika lilioko Jimboni Mtama na kulikabidhi kwetu, lakini tukiwa katika utaratibu wa kuligawa kwa wananchi, Serikali hiyo ili-reverse uamuzi wake. Je, Serikali iko tayari sasa kutumilikisha shamba hili ili wananchi waweze kulitumia kwa sababu limetelekezwa kwa muda mrefu na mmiliki wa shamba hili? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nape, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka tu nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ni sikivu na kila mara wananchi wanapotoa kilio chao, Serikali hukaa na kuanza kuangalia upya kuweza kuona ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia. Kwa hiyo katika suala zima la kusema kwamba pengine gharama ya uhamishaji miliki iweze kufutwa ili watu waweze kumiliki wengi bila tatizo lolote, naomba niseme tu Serikali hii inaendeshwa kwa kodi za wananchi. Sasa ukishaanza kuzifuta kodi ambazo pengine ni ndogo na ni *token* ukiziangalia, mwisho wa siku utakuta Serikali haina njia nydingine yoyote ya kupata mapato na kujikuta kwamba tunakwama. Tunachofanya kama Serikali ni kuendelea kupunguza zile kodi ambazo pengine zina kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nikizungumzia suala la muuliza swal ambaye aliuliza swal la msingi, Mheshimiwa Stella Manyanya kwenye eneo lake hata zile tozo wanazotoza katika masuala mazima ya ardhi ziko chini sana. Ukiangalia kwenye makazi walikuwa wanatozwa shilingi 15 lakini sasa hivi wanatozwa shilingi 11 ambazo ni kidogo sana. Kwenye maeneo ya biashara ilikuwa shilingi 30, sasa hivi wanatozwa shilingi 21, hata shilingi 100 hajifika. Ni ndogo ndogo ambazo wananchi wakiweza kulipa kwa hiari ni pesa

ambazo unaweza ukazikusanya na zikafanya kazi kubwa katika Taifa hili. Kwa sababu wazo limetolewa, naomba tulipokee na sitaweza kulitolea maamuzi sasa hivi kwa sababu ni lazima mchakato uweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ameongelea suala la shamba la Maumbika kwamba Serikali ilifuta umiliki wake kwa kushindwa kulimiliki halafu baadaye pengine maamuzi yakabadili. Naomba niseme kwamba, wakati mwagine tunapotoa ilani kwa ajili ya kubatilisha milki za watu, tunaangalia hatua iliyofikiwa lakini halmashauri husika ndiyo inayoleta *notice* au maombi yake kwa Waziri kuomba shamba lile lifutwe kwa sababu wameshindwa kutimiza masharti lakini wakati huo wanakuwa wamempa *notice* ya siku 90 ili aweze pengine kujitetea kwamba kwa nini hakuweza kumudu au kufuata masharti yale yaliyowekwa. Kwa hiyo utetezi unapokuwa wakati mwagine una uhalali na mantiki ndani yake, Serikali pia huwa inabadili mtazamo wake na kuweza kumrudishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa suala hili la Maumbika ambalo amelizungumza lazima kuna kitu ambacho kilikuwa kimetokea katika hilo kwa sababu sikuweza kuliangalia kwa undani wake kuweza kujua ndiyo amelitoa sasa hivi. Basi kama lina maelezo ya ziada zaidi ya hizi taratibu za kisheria, niko tayari kumjibu baadaye. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ulenge*. Samahani kidogo, kwanza nimewonona Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana na ya uhakika ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka tu kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba nchi hii kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Na. 5 Ardhi ya Vijiji na Na. 4 Ardhi ya Jumla tunatoa hati mbili. Kuna hati ambayo ndiyo hiyo inayosababisha wanyonge wananchi wanamiliki, tuna hati ya kimila ambayo inatolewa kwa mujibu wa sheria ambayo zaidi ya asilimia 90 ya hao wanyonge wa nchi hii

wanapewa hati za kimila na ndizo zilizo nyingi kuliko hizi hati za mjini. Hawatozwi pesa ya kuanzia wala ada ya kila mwaka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka niwaambie kwamba Serikali kupitia Bunge hili mlitunga sheria nzuri sana inayowatambua wanyonge. Wanyonge wote wanaomilikishwa zile ardhi wanazozitumia kwa shughuli zao za uzalishaji wa kila siku hawatozwi lolote, hawana kodi ya uhamishajji wala hawana kodi ile la *land rent* ya kila mwaka na hawana ukomo. Ana miliki leo, hana miaka 33 wala miaka 99 kama hati za mjini. Kwa hiyo suala la wananchi maskini wametambuliwa kwa mujibu wa sheria na waendelee. Hivi sasa Bunge lako halijawahi kutunga tozo yoyote kwa wananchi maskini wanaomiliki ardhi kwa mujibu wa sheria hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la Maumbika, nali jua vizuri. Tulikuwa na makusudi ya kufuta na ni kweli yule mwekezaji ametelekeza lile shamba. Nataka uwaambie wananchi wa Jimbo lako la Mtama, leo nakupa ahadi, nitakapokuwa naosma bajeti hapa, nitakupa barua nataka lile shamba limilikiwe na Halmashauri ya Wilaya ya Mtama ili wananchi wa pale waliendeleze iwe sehemu ya mapato yao. Walime korosho kwa sababu lile shamba ni la korosho, mmiliki alilitekeza siku nyingi, tuko kwenye hatua za mwisho za kuliondoa, lakini kwa sasa ningeomba watu wa halmashauri waendelee kuliangalia angalia, kama kuna korosho humo waanze kuokotaokota. Barua kamili ya umiliki wa shamba lile kurudi halmashauri nitaitoa hapa wakati nitakapokuwa nawasilisha bajeti yangu. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza. Naomba kuuliza swali moja; Serikali imeweka mfumo wa kidigitali wa kulipa kodi za ardhi, lakini mfumo huo haumruhusu mwananchi kupata *control number* moja kwa moja, ni

mpaka afike kwenye ofisi za ardhi ili kuhamasisha ulipaji kodi kwa haraka na kumwepushia mwananchi kulipa faini zisizo za lazima, je, Serikali haioni haja ya kuboresha mfumo huu ili kumwezesha mwananchi kulijua deni lake moja kwa moja kama wanavyofanya Wizara ya Maji? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angeline Mabula, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Mwanaisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna changamoto katika suala zima la kuweza kupata zile *bill* kuititia mtandao, lakini bado kama Wizara tulirahisisha kwa kutumia simu zetu ukipiga *152*00# unafuata maelekezo kama ambavyo tunafanya katika masuala ya *M-Pesa* na mambo mengine. Suala la msingi unalotakiwa kujua wakati unatafuta kujua *bill* yako unatakiwa uwe unajua *plot number* yako ya kiwanja au namba ya hati yako kwa sababu itakuuliza na wakati huo itakuuliza kama kiwanja chako kiko Dar es Salaam au kiko mikoani. Kwa Dar es Salaam unaweka namba moja (1) lakini kwa mikoani unaweka namba mbili (2) halafu unafuata maelekezo. Kwa hiyo kuna wakati mwengine mitandao inasumbua, kweli inakuwa ni shida lakini ukiweza kupata mahali ambapo mfumo umekaa vizuri, bado unaweza ukapata *bill* yako, unaweza ukalipa kodi yako kwa kutumia simu yako hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kama Wizara pia tunajaribu kuboresha mifumo kwa sababu kuna wakati mwengine unadaiwa 500,000 una 300,000 unataka kulipa. Ule mfumo mara nyingi hauruhusu kulipa *part payment*, inhabidi uwasiliane na Afisa Ardhi ili aweze kukupa. Sasa hivi wataalam wetu wanafanya kazi hiyo ili uweze kulipa hata kama una sehemu ndogo ya kuweza kulipa basi utalipa *part payment* na nyingine utakuja kumalizia na mfumo utapokea na Wizara ndio kazi inayofanya sasa hivi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ulikuwa unasema Dar es Salaam namba moja halafu mikoani, sasa nilifikiri Dar es Salaam ni mkoa siku hizi, kwa hiyo umeubadilisha hadhi. *Anyway*sawa.

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swalii la Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Ally Hassan Omar King, Mbunge wa Jang'ombe, sasa aulize swalii lake.

Na. 48

**Wajibu wa Kumlipa Mteja Anayeibiwa Fedha
Kwenye Akaunti ya Benki**

MHE. ALI HASSAN OMAR KING aliuliza:-

Je, wizi unapotokea kwenye akaunti ya benki ya mteja uliofanywa na mtumishi wa benki ni nani mwenye wajibu wa kumlipa mteja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Engineer Masauni, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi unapotokea kwenye akaunti ya benki ya mteja, uchunguzi wa kina hufanywa na vyombo husika katika masuala ya upelevaze ikiwa ni pamoja na Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kadri hali na mazingira ya tukio yatakavyokuwa yametokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo ikibainika kuwa wizi huo umefanywa na mtumishi wa benki, hatua stahiki huchukuliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na mteja kulipwa kiasi cha fedha alichoiwiwa na

mhalifu kuchukuliwa hatua za kinidhamu pamoja na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Pia, Benki Kuu hutoa adhabu kwa benki husika pale inapobainika kwamba utaratibu uliowekwa na benki husika ulikuwa na kasoro zilizochangia kuibwa kwa fedha za mteja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, swali la nyongeza.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa jawabu hili zuri naipongeza sana Serikali kwa kuwa na utaratibu mzuri wa kuwajali wananchi wake dhidi ya vitendo hivi vya uhalifu vinavyotokeza katika mabenki ambavyo hufanywa na watumishi ambao sio waaminifu. Nimepata tamaa sasa na mimi. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itawalipa wateja 103 wa Tawi la *NBC* la Zanzibar Forodhani ambao fedha zao kiasi cha milioni 400 zillibwa na watumishi wa benki hii ya *NBC* Forodhani kule Zanzibar pamoja na kuichukulia hatua au adhabu hiyo benki ya *NBC* kwa kutowalipa wateja hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; ili kuhakikisha kwamba hawa wazee wanalipwa fedha zao hizi za kiihua mgongo ambao wengine tayari wameshafariki; je, Serikali iko tayari kufuatilia kwa haraka pamoja na mimi kuhakikisha kwamba haya waliyosema yanatokea?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Engineer Masauni, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Hassan King kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi nilieleza kwamba, kwanza nieleze kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwaka 2006 inaeleza kwamba moja ya majukumu ya Benki Kuu ni kusimamia ufanisi na usalama wa wateja, kusimamia na benki nyingine ili kuhakikisha usalama na ufanisi wa amana za

wateja katika benki. Hiyo ndiyo dhamana yake kubwa. Kwa hiyo ikiwa tukio hili ambalo limejitokeza katika Benki ya *National Bank of Commerce (NBC)* ya uhalifu ambao umetokezea sasa haijaaelezewa na muuliza swali kwamba uhalifu huu umesababishwa na nani. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge muuliza swali kwamba nitakapotoka hapa nitafuatilia suala hili tujue kwamba je, wizi huu ulivyofanyika, uchunguzi umeshafanyika kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi? Kama uchunguzi huu umefanyika ni nani ambaye amesababisha uhalifu huu? Kama suala hili limesababishwa na wafanyakazi watumishi wa benki, basi hatua zitachukuliwa. Kama suala hili limesababishwa na mifumo ya Benki, basi Benki Kuu ya Tanzania itachukua dhamana ya kuhakikisha kwamba fedha zile zinarudishwa na benki ile na zitachukuliwa hatua benki husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme kwa sababu suala lake sio suala ambalo ni mahsus, nahitaji kufahamu kwa undani hasa kujua hasa wizi huu uliojitokeza chanzo chake ni nini na kama uchunguzi umefanyika, umefikia katika hatua gani ili tuweze kutoa maelekezo ya jinsi gani hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kwamba tutakuwa tayari kufuatilia, ndiyo maana nikaeleza kwamba kwa sababu jambo hili ni jambo ambalo yeye Mheshimiwa Mbunge analifahamu zaidi tutakuwa tayari mimi na yeye tushirikiane tufuutilie ili tufahamu kabisa kwamba jambo hili limefika katika hatua gani na tuweze kuchukua hatua pale ambapo tumefikia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa huduma za fedha za Kibenki na huduma za fedha za mtandao zote ziko chini ya Sheria ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania, naomba kuuliza; je, Serikali ina mpango gani kukomesha na kudhibiti wizi wa

mitandao ambao imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wetu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wizi wa mtandao ni moja kati ya njia ambazo zinatumika kuweza kufanya uhalifu wa kibenki na pale ambapo inabainika wizi huo wa kimtandao umefanywa na watumishi wa benki husika, basi watumishi hao huchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nillivyozungumza awali kwamba Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*) inasimamia benki zingine kuhakikisha kwamba kwanza inaa jiri wataalam au wafanyakazi ambao wanakuwa ni wenye weledi na wenye maadili ili kuhakikisha kwamba inasimamia sera na rasilimali watu kwenye benki. Benki Kuu yenye ya Tanzania inafanya tathmini kila mwaka kuhakikisha kwamba Menejimenti ya benki zote nchini inasimamiwa na Mameneja au Wakurugenzi ambao watakuwa na uadilifu.

Tatu, kumekuwa kuna utaratibu wa kuwa na *registry* ya kuhakikisha kwamba kuna orodha ya watumishi wote ambao wanakuwa sio waaminifu na pale ambapo wanakuwa sio waaminifu orodha ile inatawanywa katika benki zote ili watumishi wale wasiweze kupata fursa ya ajira katika benki nyingine kupunguza uhalifu wa aina kama hiyo ambao unakuwa unasababishwa na baadhi ya wafanyakazi au mameneja wa benki husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inafanya jitihada kubwa sana kuona benki zetu nchini zinadhibiti uhalifu wa kimtandao usijitokeze hasa pale ambapo uhalifu huo unasababishwa na benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalifu wa mtandao mwingine ambao uko nje ya benki kama ambavyo unatokezea katika taasisi mbalimbali na wenyewe Serikali inashirikiana na vyombo vya dola ikiwemo Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi pale ambapo yanajitokeza matatizo kama hayo na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Nitaleta kwenu matangazo. Kwanza ni tangazo la wageni walioko hapa Bungeni:-

Wageni wa Mheshimiwa Spika tulishawatangaza. Mimi pia ninao wageni ambao ni wanafunzi wa mwaka wa tatu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Dkt. Saumu Ibrahim na Dkt. Johnstone Andrea ambao ni *coordinators*. Karibuni sana Bungeni. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na wageni watano wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni familia yake kutoka Buhongwa Mkoani Mwanza wakiongozwa na mama yake mzazi Bi. Chausiku Mtore na mke wake Bi. Jasmin Salum. Karibuni sana. Sasa hapa sijajua yupi ni mama, yupi ni mke, hebu mke wake ni yupi? Sawa, mmemwona wifi yetu? Mmemwona wifi yetu na wanapendana na mkwe wake, jambo jema kabisa hilo. (*Makofii/Kicheko*)

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni ndugu zake kutoka Dodoma na Singida wakiongozwa na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma ndugu Ramadhan Duma. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mwasi Damas Kamani ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi wanaosoma *hot culture* kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Mkoani Morogoro, Ndugu Abdon Theonest. Sijui amekaa upande gani karibu sana.

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Esther Nicholous Matiko ambao ni watoto wake na wadogo zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Stephen Byabato, ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati ambao ni familia yake wakiongozwa na mke wake Bi. Alicia Audat Byabato ambaye, ameambatana na watoto wake. Karibuni sana; hebu asimame wifi yetu, shemeji yetu, sawa karibu sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ni watumishi wa Hospitali ya Misheni Mbesa kutoka Tunduru, Mkoani Ruvuma, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Misheni Ndugu Helga Ambrasta. Haya, karibuni sana.

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Noah Lembris ambao ni watoto wake na katibu wake kutoka Arumeru Magharibi, Mkoani Arusha. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 29 wa Mheshimiwa Kenneth Nollo ambao ni Wenyeviti wa Kata wa CCM, Jimbo la Bahi kutoka Dodoma, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kata Ndugu Elias Chawenda. Karibuni sana; naona makofi mengi. Wabunge wanaelewa kazi yenu ilivyo ngumu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni mke wake ndugu Sarah Ramadhani na mtoto wake Salim Seif Gulamali, wao wanatoka Manonga Mkoani Tabora. Karibuni sana; hebu simama kidogo mke wa Mheshimiwa Gulamali, simama kidogo. Haya jamani, asanteni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao wanatoka Kishapu Mkoani Shinyanga wakiongozwa na mtoto wake Ndugu Melkior Boniphace Butondo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Suma Fyandomo ambaao ni Ndugu Sayuni Ntulo na Ndugu Lilian Mwakitosi kutoka Mkoani Mbeya. Karibuni sana. (*Makof*)

Nimeletewa pia ujumbe hapa kwamba, Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijiini, anaye mgeni wake hapa ambaye ni mtoto wake anaitwa Bright Benaya. Karibu sana. (*Makof*)

Waheshimiwa wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo nao ni wageni 23 ambaao ni wanafunzi na walimu wa *Nazareth Sunday School*/kutoka Mkoani Dodoma. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge wanaweza kusema kwa nini mashemeji na mawifi wanasmamishwa-simamishwa humu. Ni muhimu hili jumulya hili ni vizuri kujua nani ana mke, nani hana, nani, eeh. Kwasababu, humu ndani humu huwa watu wanaruhusiwa kuoa na kuoana kwa hiyo, ni vizuri kujua nani ameshachukuliwa na nani bado. Kwa hiyo, ndio maana huwa tunasisitiza utambulisho. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge ninalo pia tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, ofisi imeweuka utaratibu unaolenga kulinda afya za Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi katika kipindi hiki cha Bunge la bajeti ambapo kwa kawaida huwa tunapokea wageni wengi na msongamano huwa ni mkubwa. Sasa utaratibu umewekwa ambaao lengo lake ni kudhibiti msongamano wa wageni Bungeni kama hatua mojawapo ya kukabiliana na huo msongamano usiwe mkubwa, lakini pia kwa ajili ya kulinda afya za Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge.

Kwa hivyo, kwa kuanzia, moja. Kuanzia sasa Waheshimiwa Wabunge wataruhusiwa kuleta wageni Bungeni wasiozidi watano kwa kibali maalum. Waheshimiwa Wabunge hawataruhusiwa kuleta wageni zaidi ya watano kwa wakati mmoja na lazima upate kibali maalum. Maana yake hapa Mheshimiwa Nollo yeye amefanya hili jambo

kabla ya tangazo kwa hiyo, Wenyeviti wamebahatika kuja wengi humu ndani. Kwa hivyo, hiki kibali kitakuwa kinatoka Ofisi ya Katibu kwa hiyo, utapeleka taarifa kule halafu wataangalia ni wageni wangapi ambao wameruhusiwa hiyo siku, halafu wageni wako utawataarifu kama watapata fursa ya kuingia humu ndani ama la. Sasa hatua hizi kama itatokea zitabadilika mtataarifiwa, ila kwa sasa taarifa ndio hiyo ya kuleta wageni si zaidi ya watano. (*Makofii*)

Jambo la pili. Wizara upande wa Serikali, Mheshimiwa Jenista Mhagama kama *Chief Whip*, lakini pia tunaye kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wizara zitaruhusiwa kuleta watendaji wasiozidi 15 ili kusaidia wakati huu wa Bunge la bajeti. Wizara zitaruhusiwa kuleta watendaji wasiozidi 15 na kipindi inacholeta hawa 15 ni kipindi kile ambacho Wizara husika bajeti yake inajadiliwa hapa ndani. Kwa hiyo, wataalamu mtakaokuwa mnawaleta ama watendaji mnaowaleta hawatakiwi 15, wanaweza kuja pungufu ya hapo.

Tatu. Ziara za mafunzo kwa wanafunzi na makundi mengine ya kijamii zimesitishwa hadi hapo mtakapotangaziwa tena. Ziara za mafunzo zote zimefutwa kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnatarajiwa kutoa ushirikiano hapa na ninadhani mtu wa kwanza kutoa ushirikiano inabidi niwe mimi maana huwa nina wageni wengi sana humu ndani kwa hiyo, nadhani linaanza na mimi hili.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo pia kutoka kwa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, ambaye ni Mwenyekiti wa Wabunge wanawake. Kwanza ni tangazo la viongozi ambao uchaguzi ulifanyika siku ya tarehe 04 Februari, 2021 na kupata viongozi mbalimbali. Ni muhimu viongozi Waheshimiwa Wabunge mkawatambua viongozi hawa; kwanza ni Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ambaye ni Mwenyekiti wa *TWPG*. Kwa hiyo, wanawake wote humu ndani tunaongozwa na Mheshimiwa Shally Raymond. (*Makofii*)

Mheshimiwa Sofia Hebron Mwakagenda ndiye Makamu Mwenyekiti wa wanawake, lakini pia Mheshimiwa

Agness Elias Hokororo yeye ni Katibu Mkoo wa wanawake. Yupo pia Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso yeye ni Naibu Katibu Mkoo. Yupo pia Mheshimiwa Esther Nicholous Matiko yeye ni mweka hazina, mkiona amebeba mabegi makubwa makubwa mjue humo kutakuwa na hela. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya yeye ni Naibu Mwekahazina. Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Matembe yeye ni Mjumbe wa Kamati Tendaji, Mheshimiwa Latifah Khamis Juakali yeye ni Mjumbe Kamati Tendaji, Mheshimiwa Riziki Said Lulida Mjumbe Kamati Tendaji. Mheshimiwa Kunti Yusuf Majala ni Mjumbe wa Kamati Tendaji. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo la kutoka tena kwa Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Shally Raymond. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanawake wote mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge, saa 07.00 mchana, kutakuwa na kikao cha Wabunge wanawake wote katika ukumbi wa Habari uliopo nyuma ya jengo la utawala. Ukiingia pale utawala unaingia kulia kwako, huko ndio kuna ukumbi wa Habari.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndio matangazo tuliyonayo. Tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2021/2022 – 2025/2026

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Na tutaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi. Mheshimiwa Humphrey Polepole ajiandae.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwamba, Mheshimiwa Shangazi

ambaye atakuwa wa pili baada ya mimi amenipatia dakika tano zake kwa sababu, anadhani naweza kuwapa mambo mengi mazuri. Halafu... (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa sasa changamoto ni kwamba, kipindi hiki unachangia tu dakika kumi. Kwa hiyo, zile za kwake inabidi labda umgawie mtu ambaye hayupo kabisa na achangie hizo tano peke yake kwa hiyo, muda wako utaanza sasahivi wa hizo dakika kumi.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, haya. Ombi lingine ni kwamba, dakika kumi nikijadili tu la Liganga/Mchuchuma hazinitoshi kwa hiyo, kama Bunge mnataka kusikiliza ya Liganga/Mchuchuma mniombee dakika tano badaye. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Waheshimiwa Wabunge naomba nichangie na kutoa ushauri huu. Ni kwamba, mpango tulionao makusudio makubwa kwanza ni suala la ukuaji wa uchumi uende zaidi ya asilimia 8, mbili ajira, tatu ustawi wa jamii na maendeleo, yote yameelezwa humo, ila mimi ninaboresha na kuongezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu unahitaji kuhudumia watu, sasa hivi tuko watu karibu milioni 61 mwaka 2025 tutakuwa takribani watu milioni 70 kwa hiyo, huu mpango lazima uwahudumie hawa watu. *GDP per capita* yetu iliyoitungiza kwenye nchi za kipato cha chini (*lower middle income*) ni dola 1080. Maoteo ni kwamba, tukifika mwaka 2025 *GDP per capita* yetu itakuwa ni dola 1400. Hizo bado ni fedha kidogo ndugu zangu, inamaanisha mwaka 2025 kipato cha Mtanzania kila mwezi kitakuwa dola 117.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikaja na hesabu angalao tufike dola 150 maana yake kwamba, *GDP per capita* yetu itakuwa dola 1800 tukifika mwaka 2025 ambayo wenzenetu wa Kenya tayari wanayo. Sasa kinachohitajika hapa na ugomvi mwingi wa kodi, *task force*, nionavyo ni kwamba, hata kodi zetu tufanyeje tatizo bidhaa ni hizohizo na walipa

kodi ni haohao. Na huu uchumi tukitaka ukue kwa zaidi ya asilimia 8 ni lazima tutafute bidhaa mpya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye bidhaa mpya naomba mnisikilize kwa makini. Tumefanya utafiti kutoka miaka mingi karibu miongo mitatu, tumeangalia nchi zilizokuwa na mafanikio makubwa ambazo uchumi ulikuwa kwa zaidi ya asilimia 10 kwa mwaka tumegundua kwamba, uwekezaji wao mkubwa namba moja ulikuwa kwenye utafiti. Ninaomba huu mpango tulionao uweke mkazo kwenye utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Jirani yangu hapa alivyosema tumeshakubaliana nchi za kiafrika *1% of the GDP iende* kwenye *research and development*. Kwa hiyo, mpango huu tunaomba utoe fedha nydingi kwa ajili ya utafiti, lakini kwa hali ya sasa tuliyonayo, *COSTECH* tuliyonayo haiwezi kufanya hiyo kazi kwasababu muundo wake ni kama idara ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya kazi na ma-*funding agencies* mengi sana duniani, lakini hayana muundo kama wa *COSTECH*. Bajeti ya *COSTECH* ni ndogo, ukichukua *1%* ya *50 billion US Dollars* ya mwaka, sasa hivi nadhani *GDP* yetu karibu iko kwenye *around 60 billion* uchukue *1%* hiyo, mnajua hesabu, uipatie *COSTECH*, *COSTECH* haiwezi *ku-manage* hizo fedha kwa ajili ya muundo na haiwezi kufanya utafiti. Kwa hiyo, cha kwanza kabisa kwenye mpango wetu turudi kwenye utafiti. Kilimo ni utafiti, maji ni utafiti, ujenzi ni utafiti, hatuwei kulikwepa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye bidhaa mpya ambazo zitaleta *8%* au *10%*. Cha kwanza kabisa nadhani msemaji mmoja jana alisema kwenye sekta ya madini lazima tubadilike ndio maana nilisema ya Liganga siwezi kuongelea mambo ya *iron*. Dunia inabadilika kuna madini yanatakiwa sasa hivi duniani kwa hiyo, kwenye ripoti zetu kuwa tunaongelea kila siku dhahabu, *tanzanite*, ni kama tunapitwa na wakati kidogo lazima tulete madini mapya ambayo ndio yatafanya uchumi ukue kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, na haya madini mapya yanahitajika kwenye *fourth industrial revolution*, mabadiliko, hata kama sisi hatuhusiki tutachukuliwa tu kama *mapassenger, passive passengers in the fourth industrial revolution* ndio sisi, lakini tunayo hayo madini. Kwa hiyo, mpango wetu badala ya uongelee vizuri dhahabu, ongelea *tanzanite*, lakini hiyo ni *monotony*, madini yanayohitajika sasa hivi naomba niyasome; *lithium* kwa ajili ya mabetri, *cobalt, nickel, platinum, chrome, manganese, copper*. Hayo yote nchini yapo, lakini hatuna mgodi hata mmoja, badala ya kila siku kufukuzana na dhahabu tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na niwasaidie tena. Dhahabu sasahivi imepanda bei kutoka kwenye dola 1700 mpaka dola 2000 kwa *ounce*, lakini nyuma ilikuwa chini yad ola 1400. Kwa hiyo, hesabu zetu mtu akisema sekta inafanya vizuri anasahau kwamba, bei kule imepanda ndio maana tumepata fedha nyangi, lakini haijamaanisha sekta inafanya vizuri migodi ni ileile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna madini ambayo ni muhimu sana. Wote wenye *iphone* hapa, kama kuna mtu ana *iphone*, madini yaliyomo humo *rea earth elements* ni manane, *specific eight*. Madini haya yako 17 na haya ndio madini yanahitajika sasa hivi duniani zaidi kuliko chuma kwa hiyo, tuwekeze huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado dakika tano?

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa nyininge ambayo inabidi kutuletea hizo fedha ni nishati. Nishati tutumie nyumbani, nishati tuiuze. Tumeshajenga *transmission lines* kwenda Kenya, *transmission lines* kwenda Zambia yaani kwenye soko la SADC na kwenye soko la *East African community* kwa hiyo, umeme tulionao ni mdogo. Kila siku nasikia mnaimba *hydro*, ukweli ni kwamba, anayejua mambo ya umeme *hydro* kukupatia faida umewekeza hela nyangi unahitaji miaka u-re-crop ile faida ndio umeme uwe wa bei ya chini wa maji. Sio tu kwamba, leo nikimaliza bwawa

hapohapo bei ni ndogo, labda kama hutaki kurudisha fedha zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu tulitengeneza *energy mix*. Na *projections* ni kwamba, Bara la Afrika litakuwa na ukame tutakuwa tunapoteza kati ya *GDP 1% to 2% zitapotea*. Je, mabwawa yetu yakikumbwa na ukame nini kitatokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana tunataka *energy mix, hydro, natural gas, coal*. Tunaenda *renewables, wind, solar, geothermal, biomass, tides and waves*. Umeme huu tunahitaji na tulishapanga zaidi ya *megawatts* 10,000 ndio *target*. Kwa hiyo, huu mpango lazima ujielekeze kuzalisha zaidi ya *megawatt* elfu kumi kwa miaka mitano ijayo; hii mingine yote haitoshi, tuzalishe tuuze, bidhaa hiyo nyingine mpya hiyo. Na tukipata bidhaa hizi tukauza tukapata fedha nyingi hata tutapunguza hizi kodi tunazopigana kila siku kwa sababu ni bidhaa zilezile ni watu walewale, sasa tulete bidhaa mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzalishe tuuze bidhaa bidhaa hiyo nyingine mpya hiyo, na tukipata bidhaa hizi tukauza tukapata fedha nyingi hata tutapunguza hizi kodi tunazopigana kila siku kwasababu ni bidhaa zile zile ni watu wale wale sasa tulete bidhaa mpya. Bidhaa mpya nyingine ni ya gesi tumesimama *LNG* yetu uwekezaji ndio ungelikuwa mkubwa kwa historia ya nchi hii, ni *thirty billion*, sisi ni *thirty billion*. Msumbiji vita yao huku *Cabo Delgado* ikitulia uwekezaji wao unatuzidi, wao wako kwenye *sixty billion* tumechelewa kwasababu hatujafanya maamuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *LNG* ndugu zangu, *natural gas* ni bidhaa mpya ambayo nchi kama *Qatar* ina *GDP per capital* ya zaidi ya *sixty thousand USD per person per annum*, na sisi tulipokuwa tumepanga kufika Dola elfu *3,000 per Person per annum* tutafikia kwa kutumia uchumi wa gesi. Kwa hiyo huo mpango kama tunataka kufanikiwa mimi sioni kwanini tuisirudi kwenye mipango yetu ya uchumi wa gesi, bila hivyo ndugu zangu hatuwezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine bidhaa mpya nimekuja nayo ambayo tunabidi kuifanyia kazi ni gesi ya *helium* ambayo inatakiwa duniani. Wote huwa mnaenda kwenye *MRI Scanner*. Unajua *scanners* zote za dunia nzima zinatumia *helium*, simu zote tulizonazo kuna *helium*. Kwa hiyo nimechukua bidhaa ambazo zinatumika duniani kwa watu wengi ndio bidhaa mpya. Kwa hiyo ndugu zangu na hiyo nayo tuiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ya mwisho hii niliongea wakati ule kwamba *agriculture* yetu ichukue mazao manne ambayo yanatumiwa zaidi ya nusu ya wakazi wa dunia hii. Sasa hivi tupo watu bilioni 7.8, tukifika mwaka 2025 tutakuwa takriban kwenye bilion tisa. Hawa watu wote hayo madini niliyokwambia wana simu, wana *laptop*, wanaenda kwenye *electric cars* na kwa hiyo watatumia hivyo vitu; ndiyo bidhaa mpya ya kufanya uchumi wetu ukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho ni kilimo kwa kuwa kinaajiri wengi. tulime na tufuate ile Maputo Declaration. Mwaka 2006 nchi za Kiafrika zilipokuwa Maputo zilikubaliana kwamba angalau asilimia 10 ya pato la Serikali iende kwenye bajeti za kilimo, lakini sisi bado tuko kwenye asilimia tatu hadi nne. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kilimo, hiyo *irrigation* mliyokuwa mnaongea jana itafanyiwa kazi, utafiti utafanyiwa kazi, tuzalishe haya manne; yaani Mahindi, Mpunga, Ngano na Mihogo, hayo ndiyo mazao ambayo zaidi ya 50 percent of the world population wanafanya consumption.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili la Liganga; muda umekwisha au bado upo?

MBUNGE FULANI: Bado.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Haya, kumbe nimeenda kasi, kumbe nimeenda vizuri. Sasa ndugu zangu Liganga ni hivi ...!!!

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Profesa naambiwa kengele ya pili imegonga.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, bado wanataka ya Liganga kidogo Mama Mheshimiwa.

NAIBU SPIKA: Dakika mbili malizia.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, haya dakika mbili, jamani ya Liganga Historia yake ni kwamba utafiti ulianza tangu miaka ya 70. Miaka ya 80 Profesa Marehemu Nicas Mahinda alifanya *Ph.D* yake kuhusu Liganga. Wakati wa miaka ya 80 watu kwenye hiyo Liganga walikuwa wanataka chuma peke yake, lakini ndani yake kuna *titanium* na *vanadium*. Kwa hiyo *discussion* ilikuwa tutatoaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana huu mradi nadhani sijui kama tulifanya vizuri kumpatia mtu mmoja miradi yote miwili; sidhani. Lakini wakati ule mawazo ilikuwa lazima tumpe anahitaji umeme mwingu ili atenganiche *Iron* kutoka kwenye *Titanium* na *vanadium*, zile zilionekana ni madini yasiyotakiwa wakati ule; lakini tekinolojia ya sasa tunayahitaji mno, *titanium* na *vanadium* tunayahitaji sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi pendekozo langu kwenye huu mradi, huyu tumempatia vyote, na Makaa na Mawe ya Mchukuma yalikuwa yatalishe *six hundred megawatts*, *megawatts* 250 azitumie kwenye mambo ya *plant* yake *megawatt* 350 apeleke kwenye *national grid*. Sasa sijui, kosa tuliolifanya yeye kama huku haweze kuzalisha umeme inamaanisha hata huku kwenye chuma hata zalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa nashauri, *NDC* haina uwezo wa kuendesha huu mradi kwasababu imekaa nao tangu miaka ya 80, lazima tufanya

maamuzi huu mradi upelekwe kwa watu wenye ujuzi, wanaoyajua hayo madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *NDC* wamepewa *soda ash* kule Engaluka, hawawezi na wenyewe watolewe hii miradi hao *NDC* ipelekwe chini ya Ofisi ya Rais kwamba kila Waziri pale anaitwa au Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini *NDC* ikibaki viwanda na Biashara kama imeshindwa kuendeleza huu mradi kwa miaka zaidi ya 40 sidhani kwamba wana uwezo huo, na hawana uwezo huo ukweli ndio huo. Sasa ambacho mimi nilikuwa nimemuomba yule mwekezaji ni wa kutoka China; na mimi napokea ripoti zote za mambo ya madini takriban ya dunia nzima. Nikampendekezea kwamba wewe mimi nadhani mtaji wako na teknolojia yako inaweza ikakufanya huu mradi usiutekeleze. Nnikamuomba balozi wa wakati huu tukakaa, mimi na balozi na yule. Nikasema kwakuwa huyu ameshawekeza hela zake sisi tutafute kampuni nyingine kubwa ya China ishirikiane nae,

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ndugu zangu China ni miongoni mwa wazalishaji wa chuma wakubwa na watumiaji wa chuma wakubwa yaani na wao wataenda kwa *speed yao*. Kwa mfano mpaka Ijumaa iliyopita walikuwa na tani zaidi ya milioni 100 kwenye bandari zao 43; wanaita *stock pile*, sasa kama mtu ana stock pile ya tani zaidi ya 110 kwenye Bandari 45 za China je, atakuwa na moto wa kuja kuchimba chuma yetu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Umesema unapata taarifa za madini dunia nzima naona umeamu kugawagawa madini mengine humu ndani hayo.

Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ili nami niweze kuchangia mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niseme kwamba tumepata somo zuri kutoka kwa Profesa, amezidi kutufundisha kwamba kuna maeneo ambayo sisi kama Taifa ni lazima tuongeze umakini na tuyafanyie kazi kwa uharaka ili tuweze kwenda kufanana na wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nikianzia pale alipoishia alipokuwa anazungumzia uwezo wa *NDC* kuweza kuendesha mradi mkubwa kama ule ya kule Liganga na Mchuchuma. Ni kweli wasiwasi huo si yeye tu anao lakini naamini Wabunge wengi hasa wanaotoka maeneo hayo wanajiridhisha hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo mchango wangu ulikuwa ujikite sana kwenye suala zima la sera, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipata kusema kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne. Tunahitaji ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Hapa kwenye siasa safi ndipo ambapo tunapata zile sera (*policy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taifa letu katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali iliyopita tumefanya mabadiliko mengi sana ya sheria mbalimbali, na nyingine pia kuziboresha kupitia *Miscellaneous Amendments* lakini hatukugusa kwenye sera; na ili tuwe na sheria tunaanza kwenye sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wote hapa wa sekta hakuna hata mmoja ambaye sera yake ni ya wakati tuliokuwa nao, sera nyingi Serikalini zimepitwa na wakati sera nyingi zimekuwa kuukuu kiasi kwamba hata mipango mizuri tunayoipanga kwa sera zilizopo bado itakuwa ni vigumu kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano tu kwenye eneo hilo la viwanda na biashara Sera ya Maendeleo Endelevu ya viwanda (*Sustainable Industry Development Policy*) 1996 hadi 2000. Leo tuko mwaka wa 2021, miaka 21 hakuna sera wala hakuna mabadiliko yoyote yanayofanyika huko, ama wamelikalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (*Small and Medium Enterprises Development Policy 2003*), hii Wizara imeikalia tangu 2011 wameanza mchakato mpaka tunavyozungumza mchakato bado unaendelea, kwa hiyo hilo ni tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukienda kwenye Sera ya Taifa ya Biashara (*National Trade Policy – NTP 2003*) nayo ni hivyo hivyo, mchakato unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwa bahati mbaya sana sheria iliyoanzisha viwanda ni ya mwaka 1967 tukiwa katika ujamaa mkongwe kabisa. Sasa hivi tupo katika angalau utandawazi hata sekta za viwanda inashikiliwa zaidi na sekta binafsi siyo viwanda vile ya umma ambapo wakati huo mashirika kama *TIRDO*kama *SIDONa* halikadhalika ndiyo yalikuwa yanaweza ku-back up. Kwa hiyo utaona kabisa kwamba ndiyo maana hata eneo la viwanda na biashara kipindi hiki hatufanyi vizuri, kwasababu sera bado imepitwa na wakati lakini sheria yenyewe iliyoanzisha, Sheria ya Viwanda pia imepitwa na wakati sana, ya 1967.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa sana na eneo hili nadhani ni Ofisi ya Waziri Mkuu ndio wanaosimamia sera, ebu tuwape hawa Mawaziri wa Kisekta muda kabisa wa kuhakikisha kwamba sera hizi zinaenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nimefurahi sana, juzi Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan alipotoa angalau muda wa miezi mitatu kwa Waziri wa Uwekezaji kwenda kutengeneza Wizara, hilo ni jambo zuri, kwamba ni lazima tuwape muda. Tusiishie tu kwamba Waziri amepewa nanii anaondoka bila kumpa muda kwamba tunataka kipindi fulani tuwe tumeona sera ambayo imekamilika ili mambo yetu yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Ajira ni ya mwaka 2008. Hivi tunavyozungumza tunataka ajira milioni nane, ziko katika llani ya Chama cha Mapinduzi, lakini Sera ni ya mwaka

2008 inawezekana kabisa kuna mpishano kubwa kati ya Sera na mipango yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima tuone kwamba mipango tunayoiweka na sera tuliyokuwa nayo ni kwa kiasi gani vinashabihiana ili kuweza kuzalisha zile ajira 2008. Sera ya Vijana ni ya mwaka 1998 Sera ya Michezo ya mwaka 1995. Sanaa ya Michezo ambayo sasa hivi tunaona kwamba eneo hili linachangia pato, nadhani ni la pili baada ya utalii, lakini sera yake ni ya mwaka 1995 ndiyo maana tunaona hata wasanii au kwenye michezo wanajientesha wenyewe wenyewe hakuna mpango ambaao Taifa kama Taifa tunaweza tukaona kama katika eneo la Michezo tunakwenda kwa mwelekeo upi. Kwa hiyo ni lazima Mheshimiwa Bashungwa fanyia kazi eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana hata *Club* ya Simba inapata taabu katika kuingia kwenye uwekezaji kwasababu michezo bado inaonekana ipo katika ridhaa, ilhali sasa hivi michezo ni sehemu ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Mambo ya Nje, diplomasia ya uchumi haijaandikwa popote, tunazungumza tu. Tupo katika diplomasia ya uchumi, lakini hakuna mahali popote kwamba kuna sera inaelekeza hivi, tutakuwa na waambata wa kibiashara katika balozi zetu tutakuwa na hiki, hakuna! Tunaizungumza mdomoni lakini lakini kwenye Makabrasha hakuna (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili nalo ni eneo muhimu sana, tulitazame, hasa katika eneo hili la Kilimo ambapo tunatamani kuona kwamba mazao ya wakulima wetu yanavuka mipaka na kwenda kushindana na maeneo mengine. Sasa ni lazima sera hizi zisimamiwe na tuwape muda tuhakikishe kwamba tunakuwa na sera madhubuti zinazoweza kusimamia mpango wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye elimu huku nako kuna *double standard*. Kuna wakati Waziri anatumia sera ya mwaka 1995, kuna wakati anatumia 2004,

inategemea tu umembana katika *angle* gani, kwa hiyo anatafuta upenyo kwa kupitia sera. Kwa hiyo ni lazima tuwe *specific*, kwamba kwa elimu yetu tunatumia sera ya mwaka gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ya 2004 ndiyo ilituelekeza kwamba elimu ya Msingi iishie darasa la Sita, lakini hata Mtaala wa elimu ukaelekeza hivyo ndiyo maana miaka miwilli mitatu huko nyuma hakukuwa na vitabu vyataga la saba. Baada ya kuanza kuhoji hili jambo nadhani wamenyofoka katika maeneo fulani fulani wametengeneza Mtaala wa Darasa la Saba; lakini kimsingi ilikuwa kwamba elimu ya msingi iishie darasa la saba katika kuboresha suala zima la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana kwamba eneo hili Serikali tunaomba kwamba tuboreshe sera zetu katika sekta zote ili ziweze kuendana na mipango hii mizuri ambayo tunaiweka ili ziweze kusaidia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nadhani Waheshimiwa Mawaziri hapa watakuwa pia walifuatilia mchango wa jana wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani. Kama Taifa tukiwa na mwelekeo mmoja tukiwa na agenda ya Kitaifa, basi sera nazo zitajelekeza kwenye kuhakikisha mpango huo wa Taifa unaenda vizuri.

Mheshimiwa Humphrey Polepole atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi naomba kuungana na Wabunge wenzangu kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa mwaka 2021/2022 na 2025/2026 na nitapenda kujikita katika maeneo manne kwa ufupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni ukweli usiopingika ya kwamba ulimwenguni biashara ndogo ndogo, biashara ndogo na biashara za kati ndizo zinachukua asilimia kubwa ya uchumi ulimwenguni. Kwa lugha ya Kiingereza *Micro small and medium enterprises* ndizo ambazo zina-constitute most of the economies Ulimwenguni, na neno biashara, ukisema enterprises kama ni biashara, lakini nikisema enterprises inaweza kuwa kampuni ndogo enterprises inaweza kuwa mradi fulani wa uzalishaji enterprises inaweza kuwa shughuli ambayo mtu anaifanya kujiletea kipato. Nitatumia neno enterprises nikimaanisha kwa maana ya tafsiri hiyo pana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wote waliofanikiwa ulimwenguni ma-bilionea ma-trilionea kwa mtindo huo wote walianza kama *micro entrepreneurs* ama unasema *small entrepreneurs*. Mimi ushauri wangu kwenye mpango, tujikite sana kwenye kuwezesha *micro-small and medium enterprises* kwasababu hawa ndio injini ya uchumi wowote na ikiwepo hapa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu za tangu mwaka 2010 *micro small medium enterprises* zilikuwa kama 2,700,000, kwa maana ya wale ambao wamezianzisha; lakini kwa sera yetu hapa Tanzania ukitazama tafsiri wanasema *micro enterprises* ni zile ambazo zinawamiliki chini ya watano halafu wale wanaokuwa *small* wanakuwa watano mpaka hapo mbele kumi, halafu wale wakubwa wanaanza kumi na kuendelea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Tanzania watu wengi wanaosimama katikati ya ama mazao ya shambani na bidhaa inayokwenda kutumika nje ni hawa watu wa *Micro small and Medium Enterprises*. Iwapo tukiwawezesha vya kutosha hili ni eneo lingine kubwa sana la kikodi ambalo linaweza kuchangia vikubwa sana katika Pato letu la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa kufanyika, kwanza, ni kuwatambua watu hawa. Watu wengi katika eneo hili bado siyo rasmi wanasema ni *informal sector* lakini kimsingi

ajira karibia zote, kwa takwimu za mwaka 2010 *Micro, Small and Medium Enterprises* peke yao walikuwa wana-constitute kwa zaidi ya 31% ya ajira zote hapa Tanzania na hawa ni watu milioni 2,700,000 peke yake. Kama tungekuwa tumewafanya wawe mara mbili maana yake wakawa kama milioni 6 hivi wale waanzishaji wa biashara, nazungumzia biashara hizi zote kwa maana kuanzia *Micro, Small and Medium* ni wale wenye kipato kisichozi bilioni 1 basi tungeweza kuona ajira zaidi ya 70% zinatoka katika eneo hili la biashara hizi ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali tuwapatie uwezeshaji bila mizengwe, milolongo mirefu na *bureaucracy*. Utaratibu ambao tayari Serikali imeanza kuufanya kazi ni mzuri sana na umekuwa na matunda ni kuwatambua Watanzania. Sasa hivi asilimia kubwa ya Watanzania wana vitambulisho vya *NIDA*. Kitambulisho cha *NIDA* unawea ukamfahamu mtu jina lake ukiacha taarifa zile za msingi lakini unawea kufahamu anatoka wapi, ana shughuli gani na tukiendelea kuboresha tunaweza hata kupata taarifa za kifedha na za kibenki za kila Mtanzania; benki yake ni wapi, anashughulika na jambo gani. Kwa hiyo, tutakuwa tumewaondoa watu hawa wengi kwenye *Micro, Small and Medium Enterprises* kwenye kigingi kikubwa cha kupata uwezeshaji wa kifedha kwa msingi wa *collateral/ama wanasema dhamana*.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kila Mtanzania atakuwa na hati ya nyumba rasmi ya kwenda kupata mkopo lakini siku hizi kwenye masoko ya kileo ya mikopo tumeanza kuzungumza kuhusu mbadala wa *collateral* kwa maana ya dhamana ile ya kidesturi kama hati ya nyumba kwa kuanza kutoa ama mikopo midogo midogo ama kutumia utambulisho ambao hauna shaka. Sasa hivi ukitumia kile kitambulisho chako cha *NIDA* na tukiweka vizuri zaidi watu wetu wa TEHAMA Serikalini, inawezekana kujua mwenye kitambulisho hiki cha *NIDA* amekopa mkopo benki kwenye eneo fulani na hajalipa au mwenye kitambulisho hiki cha *NIDA* ana *perform* mkopo wake mahali fulani vizuri zaidi. Kwa hiyo, unapokwenda kwa mkopeshaji yejote rasmi kwa maana ya

Taasisi kwa kitambulisho tu kile kinaweza kukupatia uhalali wa wewe kupata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia wanaoingia kwenye soko la ajira ni zaidi ya watu milioni 1 kila mwisho wa mwaka, hawa watu wanaoingia huku ni vijana na hawa vijana hawana hati za nyumba. Kama tukiweka utaratibu mzuri wa kuwatambua wakapata vitambulisho na tukapata wanasesma *guaranteeskutoka* kwa ndugu wa karibu na ndivyo ambavyo wenzetu wa Mashariki ya Mbali, Thailand wamefanikiwa kuwakopesha watu wengi sana na kufanikiwa ni kwa sababu ya kutumia utaratibu kama huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili litatoa ajira nyingi sana. Hawa ndiyo ambaa baada ya kiwanda kutoa bidhaa wao ndiyo watachakata, watasambaza kidogo kidogo; hawa ndiyo ambaa mgodi ukianza ndiyo watakaokwenda kuchukua madini yatakayotolewa na kuyauza kidogo kidogo. Ushahidi upo kwenye eneo la madini hizi bilioni nyingi zimetokea ni kwa sababu tumewarasimisha wachimba madini wadogo wadogo kwa kuwawekea masoko ya madini na tumeona pesa nyingi sana imepatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ilikuwa ni kuhusu uchumi. Ni muhimu sana tukafahamu kwamba uchumi wetu umekuwa madhubuti kwa sababu tumewekeza katika ujenzi kama eneo moja kubwa na ni kigezo cha ukuaji wa kiuchumi. Ujenzi huu umesambaa nchi nzima; barabara, miundombinu ya reli, tumetengeneza meli maeneo mengi kabisa na sasa tuna Bwana la Mwalimu Nyerere na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia amesema lazima mambo haya yaendelee na Watanzania wanafahamu hivyo. Ujenzi mkubwa ni kigezo kikubwa sana cha ukuaji wa kiuchumi na uchumi ukikua ndiyo tutapata fedha, watu watapata ajira nyingi za muda mfupi na muda wa kati na hatimaye mwisho wa siku watu watapata kipato na wataweza kumudu maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali, ziko fikra kadhaa lakini napenda kusisitiza kwamba ni muhimu tukaendelea kusimamia nidhamu ya kusimamia uchumi wetu. Tumefanikiwa sana kuufanya mfumuko wa bei kwua *single digit* na kuna fikra nyingi kwenye eneo hili lakini fikra moja ni bayana ni kwamba mfumuko wa bei unapokuwa chini mnufaika ni mwananchi wa kawaida na hasa mnyonge. Ndiye ambaye mkate utaendelea kuwa bei ileile ndani ya muda mrefu, ataongeza kipato lakini bei ya mkate itabaki palepale. Pia wale wakubwa wakiiza mikate mingi kwa sababu wananchi wote wanaweza kununua na wao hatimaye wanaweza kutengeneza faida kwa maana hiyo. Kwa hiyo, kuendelea kuweka nidhamu ya usimamiaji wa uchumi na hasa kuhakikisha kwamba *inflation* haiongezeki katika kiwango ambacho tume-*maintain* ni muhimu sana kwa ukuaji wetu wa kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni masoko. Hapa Tanzania hatuna tatizo la uzalishaji, wakulima wanalima mazao kila mwaka. Kinachotakiwa sasa hivi ni kutumia mageuzi makubwa ya ki-TEHAMA kumuunganisha mkulima moja kwa moja na soko na kuondoa ukiritimba wa madalali. Wakulima wengi hawafahamiani na mnunuaji wa mwisho lakini kama hapa tungkuja na private sector wakatengeneza mifumo ya ki-TEHAMA ambayo inaweza kumwezesha mkulima akasema nina magunia 100 ya mahindi nika-post hapa kwenye application fulani halafu mtu fulani akasema nataka magunia 50 ya mahindi akaingia kwenye application hiyo wataonana kama ambavyo mifumo hii duniani ipo. Ali Baba alianza kidogo hivi mwaka 1999 yeye na mkewe na anakubaliana na hiki tunachokisema kwamba biashara ndogo sana na za kat i wanaanza watu wachache. Hapa Tanzania kwa takwimu ni 2.9% tu ya biashara hizi zote za kat i na hizi ndogo zaidi ndiyo zina watu zaidi ya watu watano mahali kwingine kote ni watu wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu utawala bora na uwajibikaji. Mimi napenda kusema kwamba wakati wa msiba wa Hayati Magufuli wale watu walikuwa wanalia siyo kwa sababu Rais Magufuli ametangulia mbele ya haki,

mimi nasema hapana. Wale watu walikuwa wanalia kwa sababu Rais Magufuli na Mama Samia walikuwa wana jambo lao na wananchi wale. Wale wananchi walikuwa wanalia wakionyesha *concern* ya kama yale ambayo Rais Magufuli na Mama Samia waliwaahidi hayo ndiyo yatakayoendelea hata wakati Magufuli hayupo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Samia ameeleza msimamo, amesema kazi iendelee. Rai yangu kwa Serikali, usimamizi mzuri wa rasilimali za Taifa letu unatokana na nidhamu nzuri ya viongozi wetu. Vita dhidi ya rushwa, ujisadi, matumizi mabaya ya rasilimali za umma; mambo hayo hatutakiwi kurudi nyuma kamwe, asilani! Kinyume na hapo, Watanzania wale walilia watalia na baadhi yetu humu muda si mrefu kwa sababu watasema tumewageuka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu tumsaldie Mheshimiwa mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili ile ndoto ambayo walituletea yeeye na Mzee Magufuli, tukawaamini na tukawapenda ikatimie chini ya uongozi wake katika kipindi hiki na kwa kadri ambavyo Mungu itampendeza na yeeye mwenyewe kwa maana hiyo na Chama chetu cha Mapinduzi. Umuhimu sana kuliko yote, nimefurahia sana Mheshimiwa Rais amesema kukumbuka kuzingatia haki za watu wetu na hasa wanyonge. Ni muhimu sana viongozi wakaendelea kusimamia hilo wakati wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa katika kuhakikisha kwamba Serikali yetu inaendelea kufanya kazi za maendeleo

na kuendelea kukuza uchumi kwa Taifa letu lakini kuendelea kukuza ajira na kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pole kwa Watanzania kwa msiba mzito ambao umetupata pamoja na Waheshimiwa Wabunge nawapa pole sana kwa sababu tulizoea kufanya kazi na ndugu yetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Tumeona namna ambavyo ameweza kusimamia na kuendesha Serikali yetu kwa kipindi cha miaka mitano na ameweza kusimamia maendeleo makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mama yetu Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu kwa uteuzi wake. Nina hakika kwamba ana uwezo mkubwa wa kusimamia Taifa letu na kuendesha yale mazuri yote ambayo alianza kufanya kazi na Mheshimiwa ndugu yetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba naanza kwa kuunga mkono hoja. Ukiangalia Mpango wetu hata ukiangalia mipango yote iliyopita tumeona kwamba kuna hoja ya Miradi ya Magadi Soda Engaruka, Mchuchuma na Liganga na *LNG*. Miradi hii mikubwa kila mwaka tunaiona ipo katika Mpango wetu wa Maendeleo wa Taifa lakini naona kwamba Serikali haijawa tayari kusimamia miradi hii kuhakikisha kwamba tunakwenda sasa kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Mradi wa Mchuchuma na Liganga soko la makaa ya mawe yapo ndani ya nchi na nje ya nchi lakini Serikali hatujakuwa tayari kuwekeza ili kuhakikisha kwamba uzalishaji huu unaendelea kuleta tija na manufaa kwa Taifa letu. Kwa hiyo, naiomba Serikali kusimamia ili kuhakikisha kwamba mradi huu unakwenda vizuri na unaleta tija na unaongeza mapato kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinis tuna Mradi huu wa *LNG*, kwanza niishukuru Serikali kwa hatua ambayo imefikia kuhakikisha kwamba imetoa fedha ya kulipa fidia kwa

wanaopisha mradi pale Lindi katika eneo la Likongo. Hata hivyo, naiomba Serikali kuharakisha mradi huu ili sasa utekelezaji uweze kuanza na kuhakikisha kwamba tunakwenda nao vizuri kwa sababu mradi huu utatuletea manufaa makubwa na utaingiza mapato makubwa katika Taifa letu. Si kwamba tutakaofaidika ni wana Lindi lakini Tanzania nzima tutafaidika na mradi huu wa *LNG*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali sasa kuharakisha mazungumzo ya mwisho yaliyobaki kuhakikisha kwamba sasa mradi huu tunakwenda katika utekelezaji. Nina hakika kwamba Mama yetu Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu atausimamia vizuri kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye utekelezaji. Pia naomba wafidiwa walibaki kulipwa fidia zao basi Serikali iharakishe kutoa malipo ili wananchi wale tuweze kuwaondoa na waweze kupisha mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la afya. Katika Sera ya Afya tumeweza kutekeleza vizuri na Mpango wa Taifa wa Pili ilitumia trilioni 3.15. Ilifanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba imewekeza katika sekta ya elimu. Naomba Mpango wa Tatwa Maendeleo ya Taifa kwa maono ya Mheshimiwa aliyekuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wa kujenga Shule ya Sekondari ya Wasichana kila Mkoa kwa mchepuo wa sayansi uzingatie kuhakikisha kwamba tunakwenda

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano iliwekeza katika kuboresha sekta ya elimu na ilitumia trilioni 3.15. Ilifanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba imewekeza katika sekta ya elimu. Naomba Mpango wa Tatwa Maendeleo ya Taifa kwa maono ya Mheshimiwa aliyekuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wa kujenga Shule ya Sekondari ya Wasichana kila Mkoa kwa mchepuo wa sayansi uzingatie kuhakikisha kwamba tunakwenda

kuendeleza maono haya ili watoto wetu wa kike waendelee kupata elimu ya masomo ya sayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunazo shule kongwe, najua mpango wa Serikali wa kujenga na kukarabati shule kongwe unaendelea kwa shule za sekondari pamoja na vyuo lakini bado hatujaangalia katika shule zetu za msingi. Kuna shule za msingi ambazo ni chakavu mno, ukiangalia kwa macho hazipendezi na hazikaliki madarasani na hazipo rafiki kabisa wanafunzi kukaa madarasani. Kwa hiyo, naomba Serikali sasa kupitia Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa uziangalie zile shule za msingi kongwe ziendelee kuingizwa katika Mpango maalum na Serikali iweze kuzikarabati ili tuwe na shule bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sera ya barabara, tunazo barabara kuu za kiuchumi zinazounganisha mkoa na bandari lakini zinazounganisha bandari na nchi Jirani. Tuna barabara inayotoka Dar es Salaam - Pwani - Lindi - Mtwara; tuna barabara inayotoka Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma - Mwanza, lakini tuna barabara zinazokwenda nchi za jirani maana yake zinaunganisha uchumi wa nchi yetu na uchumi wa nchi Jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zetu zimekuwa dhaifu sana hata kama tunazikarabati utakuta barabara imekarabatiwa imetumika miezi sita tu tayari imeingia kwenye uchakavu. Kwa hiyo, Serikali yetu inaendelea kutumia fedha nyingi kukarabati kila mara barabara hizi lakini bado zinaonekana zipo chini ya kiwango. Kwa hiyo, naomba Serikali sasa kuhakikisha kwamba sera yake inakuwa wazi namna bora ya kuzikarabati na kuzijenga barabara hizi kwenye kiwango cha hali ya juu ili ziendelee kutumika katika kukuza uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala zima la *TARURA*. *TARURA* wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana lakini ukiangalia hata ofisi hawana, baadhi ya maeneo ofisi za *TARURA* hazipo tunatumia majengo ya kukodi lakini majengo yenye ni madogo hayana nafasi kubwa, pia

bado hawana vifaa na magari na kuna upungufu mkubwa wa watumishi. Kwa hiyo, naomba sasa Serikali kuangalia namna bora ya kuwaboresha hawa ndugu zetu *TARURA* ili tuende nao vizuri na waweze kufanya kazi zao vizuri na sisi tuweze kufaidika na *TARURA* katika kuhakikisha kwamba wanaendelea kufanya kazi katika mazingira rafiki na tunategemea kwamba waweze kusimamia barabara zetu za kule kwenye Halmashauri zetu ziweze kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Mpango wa Tatu wa Taifa katika uwekezaji wa uchumi wa bahari. Nimeona kwamba sasa tunakwenda kuwekeza katika sekta hii ya uvuvi na kuhakikisha kwamba Serikali yetu sasa inaingia katika uwekezaji huu wa bahari. Ni jambo jema sana lakini nafahamu kwamba sekta hii ya uvuvi inatoa ajira za kudumu zaidi ya laki mbili, lakini inatoa ajira za muda mfupi zaidi ya millioni 4. Kwa hiyo, ni jambo jema sasa kuingiza katika uwekezaji huu na sisi tutaendelea kufaidika na Serikali yetu itaendelea kuingiza mapato ya kutosha. Nashauri tu tuwekeze katika rasilimali watu kwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na wataalamu wenye ujuzi mkubwa wa kusimamia sekta hii ya uwekezaji huu wa uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Tatu wa Taifa pia umeonesha namna bora ya kusaidia ndugu zetu wa *SIDO*. *SIDO* wanafanyakazi nzuri sana na tukiwatumbia ndugu zetu wa *SIDO*...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili Mheshimiwa.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, tuwekeze kuwasaidia na kuwapa nguvu ndugu zetu wa *SIDO* ili watusaidie kutoa elimu ya mafunzo stadi lakini tutakuwa na uwekezaji mkubwa wa viwanda vidogo vidogo kwa sababu wao wanasmamia shughuli hizi. Kwa hiyo, naomba tuwaunge mkono ndugu zetu wa *SIDO* ili kuharakisha maendeleo ya wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache kuhusu Mpango wa Tatu wa Maendeleo ambayo ni hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango hii inatengenezwa na inapangwa na mara nydingi kila mwaka tunakaa hapa tunaijadili na baadaye tunaitafsiri katika pesa, tunaipangia bajeti. Kwa hiyo, tunasubiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine mipango hii haitekelezwi jinsi inavyotakiwa. Nami napenda niungane na Kamati ya Bajeti. Kamati hii imetoa mapendekezo kwamba kuna haja kubwa ya kuwa na mfumo mzuri katika ufuatiliaji na usimamizi wa mipango yetu, yaani ile tunaita *monitoring and evaluation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa LAAC karibu miaka mitano, kwa hiyo, tunapata nafasi nzuri ya kukagua miradi ya maendeleo. Miradi ilio mingi haitekelezeki na nydingine inachukua muda mrefu kwa sababu au Serikali haipeleki pesa au hakukuwa na uhalisia wa miradi hiyo. Kwa hiyo, nashauri kwamba tunapopanga mipango kwanza, miradi iwe ya uhalisia ambayo inaendana na bajeti yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia miradi hii isimamiwe; kuwepo na sera. Serikali ilete sera. Kamati ya Bajeti mimi jana nimeisikiliza sana, nimeona hili ni jambo la msingi sana, kwamba watuletee sera na sheria ili tuweze kuwa na kitengo kizuri ambacho kinafanya ufuatiliaji. Sijasema kitengo hakipo, kipo lakini hakina tija kwa sababu hakuna sheria yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Serikali haitakubali kuleta hii sera kwa sababu Serikali haipendi kufuatiliwa. Nakumbuka wakati tunaanzisha Kamati ya Bajeti, Spika na Naibu walismama. Kwa hiyo, naomba nikutume, msimamie jambo hili, pale ambapo Serikali itakataa, wale waliokuwa kwenye Bunge wanakumbuka ilivyokuwa mbinde kutengeneza Kamati ya Bajeti; Serikali ilikuwa haitaki na inawezekana katika hili pia haitaki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri Bunge lisimame, mlete sheria. Wakati ule iliposhindikana Bunge lilitunga sheria na Serikali ikashituka ikaleta sheria, kwa hiyo, tukaweza kuunda Kamati ya Bajeti. Bila kuwa na Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, hii miradi ambayo tunakaa hapa tunapanga haitatekelezeka ipasavyo. Kwa hiyo, hiyo ni hoja yangu ambayo nimeona ni ya msingi ili hata tukiaa hapa tukaandaa mambo, tukapanga na baadaye tukapeleka pesa katika miradi hii, kama hakuna ufatiliaji na usimamizi; na ifike mahali kama ikibidi tuwe na kamati ndani ya Bunge ambayo kazi yake itakuwa ni kufuatilia kuona kama je, kuna *discipline* katika bajeti?

Je, Serikali inatimiza tunavyowaelekeza au hakuna *discipline* kila mtu anafanya anavyotaka? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kushauri kwamba kama Serikali ikishindwa kuleta, basi naomba Bunge lisimame kabisa liweze kuhakikisha kwamba hiki kitu kinatekelezeka kwa sababu tumekishauri kwa muda mrefu na bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa niende katika mipango hii na bajeti zetu kuchochea maendeleo ya watu. Unapowaeleza Watanzania kwamba uchumi ni wa kati au uchumi ni mzuri, una maana gani? Kwa sababu Watanzania wetu hawa ambao tunawaita wanyonge; na hili neno "mnyonge" mimi linaniudhi sana. Kwa sababu gani? Ina maana tunataka kuwaambia Watanzania wakubali unyonge na umasikini, yaani waubebe mgongoni, wauwekee na mbeleko kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania sio wanyonge, Watanzania wakipangiwa mipango mizuri, wakaelekezwa, wanaweza wakafanya kazi yao vizuri na nchi yetu ikapata maendeleo. Kwa hiyo, hayo mambo ya kuita Watanzania wanyonge, kwa kweli inanikera sana. Watanzania sio wanyonge, ni watu amba wana uwezo mkubwa sana kuweza kufanya kazi zao; wakielekezwa vizuri wakawekewa sera nzuri, wanaweza kuendeleza maisha yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposema uchumi kwa mtu wa kawaida anapata maana gani? Maana tuna vijana wasomi hapa wapo wengi, ambao kazi yao ni kutuandikia *ma-book* hayo. Hayo *ma-book* yapo, ni yawasomi, lakini Watanzania wa kawaida wanachohitaji ni maisha yao ya kila siku. Wanahitaji mahitaji yao, wanataka kupewa nguvu ya manunuzi kwanza, waweze kuwa na uwezo wa kuendesha maisha yao ya kila siku. Unapomwambia mtu uchumi umekua nyumbani kwake, anaangalia tangu asubuhi anaweza kumudu maisha yake!

Kwa hiyo, hapo uchumi tuuchukulie katika kuhakikisha watu wetu wanakuwa na uwezo wa kumudu maisha yao ya kila siku. Pia mipango hii na uchumi iendeleze maisha yao na huduma za kijamii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nilitegemea kwamba mipango ya mwaka huu itaangalia maji. Upo ukosefu mkubwa wa maji katika nchi hii. Maswali ya maji yakiulizwa hapa wewe mwenyewe ukiwa hapo unaona watu wanavyonyonyuka, kila mtu anaongelea maji katika jimbo lake. Kwa hiyo, nilitegemea kwamba mpango huu ungeweza kufikiria namna nzuri ya kuweza kuhakikisha kwamba tunaondokana na adha ya ukosefu wa maji katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka mwaka 2020 tulikuja na pendekezo hapa kwamba Serikali ifikirie namna ya kupata pesa kidogo kutoka kwenye mafuta, tufanye *re-investment* kama tulivyofanya kwenye *REA* ili kupunguza matatizo makubwa sana yaliyopo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niligombea Jimbo Bukoba Vijijiini huko tulikuwa tunapambana na Mheshimiwa Rweikiza, lakini Jimbo la Bukoba Vijijiini lina matatizo makubwa sana ya maji.

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Itakuwa kengele ya kwanza hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa ya maji katika jimbo lile; ukiliangalia lina Kata 29, lakini *almost* asilimia 55 watu hawana maji. Kwa hiyo, wanapotupa takwimu kwamba kuna maji ya kutosha watu milioni 25, mimi sikubali, kwa sababu ukienda Mkoa wa Kagera kwa mfano, tuna mradi wa maji pale Bukoba Manispaa, ndio mzuri. Nenda Kyerwa, Karagwe, Bukoba Vijijiini, Ngara, Biharamulo na kusema ukweli Mkoa wetu wa Kagera hata haukutokea katika mpango. Nimesoma kuona kama kuna Kagera imeandikwa mahali popote pale, hakuna, labda kama itakuja kwenye bajeti ya kisekta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaangalia matatizo makubwa. Ukosefu wa maji unasababisha magonjwa. Wanawake wanalalamika. Badala ya kujenga uchumi wao, wanashinda kwenye mahospitali. Maji yanaleta magonjwa mengi: *Typhoid, Amoeba* sijui na vitu gani na vitu vingine vinaitwa *UTI*. Kwa hiyo, unakuta watu wanahangaika, badala ya kufanya shughuli za uchumi, wanakwenda kwenye matibabu. Kwa hiyo, tunaomba hoja ya maji iwekwe kipaumbele ili tuhakikishe tunasaidia wanawake kuwatua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo kuhusu kilimo. Pamoja na mambo mengi, lakini nimegundua kwamba hakuna hata wataalam wakusaidia kilimo. Kwa sababu unapolima; na binadamu sisi tuna tabia ya kufundishwa na kukumbushwa kila wakati. Kwa hiyo, hakuna wataalam, hakuna *extension officers* wa kilimo na hata wa mifugo. Unaweza kwenda kwenye Wilaya moja; kwa mfano Wilaya

ya Muleba; mimi natoka Wilaya ya Muleba. Unaweza kukuta kuna mtu mmoja tu ambaye ni Afisa Mifugo na watu wanafuga; wana ng'ombe wa maziwa, lakini wale *extension officers* hawapo. Tunaomba Serikali ichukue hatua ya kuajiri *extension Officers* ili wakulima pamoja na kilimo chao lakini wapate utaalama wa kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niongee kuhusu ushirika. Tunapoongea kilimo ni lazima tuangalie na namna ya kusaidia ushirika. Ushirika unasaidia wakulima. Huko nyuma ushirika ulikuwa unasaidia hata kutafuta pembejeo; mbegu, lakini pia ushirika ulikuwa unasaidia katika malipo ya wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakulima wa kahawa kwa mfano Mkoa wa Kagera wamepata shida sana sana ya malipo. Mtu anauza kahawa zake, anakaa miezi sita hajapewa fedha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Vuma Holle ajiandae.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuchangia, naomba nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi ya kugombea katika Jimbo la Meatu. Kubwa pia, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Meatu kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao, nami

nawaahidi sitawaangusha na ninamwomba Mwenyezi Mungu anisaidie. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Hebu subiri kidogo Mheshimiwa. Subiri subiri, nimezima *microphones* zote, kwa sababu sielewi kelele inatoka wapi. Hebu hamia kwenye *mic* ya jirani halafu ujaribu kuisimamisha. Zima kwanza hapo ulipotoka.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita katika moja ya maeneo makuu matano ya kipaumbele ambayo ni kuchochea maendeleo ya watu. Eneo hili linajumuisha utekelezaji wa miradi ambayo inajikita katika kuboresha maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mpango wa pili kumekuwepo na mafaniklo makubwa katika Sekta ya Afya. Tumeona miundombinu katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali zikijengwa, vilevile na upatikanaji wa dawa, ongezeko la watumishi pamoja na vitendea kazi. Hata hivyo, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto nyingi. Kwa hiyo, naomba katika Mpango huu wa Tatu changamoto hizi zitatuliwe ili tuweze kufikia malengo ya mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikamilishe sasa maboma ya Zahanati na Vituo vya Afya ili yaweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa. Vile vile kukamilishwa kwa maboma haya kuende sambamba na upatikanaji wa vitendea kazi, watumishi wa kutosha na dawa za kutosha. Ni ukweli usiopingika kwamba Zahanati zetu nyingi hazina watumishi wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara zangu, nimeshuhudia, baada ya mtumishi kustaaafu Zahanati inafungwa. Mojawapo ni Zahanati ya Mwabalebi. Pia katika Zahanati ya Mwabagalu kuna watumishi wawili ambaao mmoja amekwenda *maternity*, mmoja ni mgonjwa, Zahanati imefungwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke mkazo katika kuajiri wataalamu wa afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali itoe fedha za kutosha ambazo zitapaswa kutolewa katika chombo chetu cha *MSD* ili kiweze kusambaza dawa za kutosha nchini. Ni ukweli usiopingika, katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa Serikali imeongeza Bajeti kubwa ya madawa kutoka shilingi bilioni 29 mpaka shilingi milioni 250. Madawa katika hospitali zetu yaliongezeka mpaka upatikanaji wa dawa muhimu ulifikia asilimia 80 mpaka 90. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ninavyoongea, ukienda kwenye hospitali zetu, hakuna dawa. Wananchi wanaandikiwa dawa na kuhitajika kwenda kununua dawa katika maduka ya dawa. Naiomba Serikali niweke mkazo katika mauzo ya dawa. Tutategemea bajeti zitaongezwa, lakini Serikali ikiacha tu kutoa fedha, hospitali zile zinakosa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano tu. Robo tatu zilizopita za *basket fund* haikuweza kuletwa katika hospitali zetu. Kwa hiyo, ilisababisha ukosefu wa dawa katika hospitali zetu. Kwa hiyo, Serikali ikiweka mkazo katika mauzo ya dawa, itasaidia kuwa na mzunguko, kutakuwa na *revolving*. Hata hivyo, wataalam wetu wamekuwa na kisingizio kwamba madawa haya yanamalizwa na wagonjwa ambao wako kwenye makundi ya msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naishauri Serikali, ijue ni asilimia ngapi itakwenda kwenye makundi ya msamaha, ni asilimia ngapi itakuwa ni ya mzunguko na hiyo isimamiwe. Hata kama Serikali ikichelewa kupeleka fedha za ruzuku, hospitali hizo kuwe na mzunguko wa kutosha na madawa yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Elimu kumekua na mafanikio makubwa. Tumeona ongezeko la wanafunzi kutokana na Elimu Bila Malipo na miundombinu mingi imejengwa. Hata hivyo, sekta hii bado ina changamoto nyingi katika miundombinu ya kujifunzia na ya kufundishia. Kwa hiyo, kwanza naiomba Serikali itoe fedha iweze

kukamilisha maboma ya maabara katika Shule zetu za Sekondari, itoe fedha za kutosha kukamilisha maboma ya vyumba vyaa madarasa pamoja na nyumba za watumishi. Pia udahili wa wanafunzi uendane na ongezeko la vyumba vyaa madarasa pamoja na nyumba za watumishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri za vijijiini, nimeshuhudia kuwepo kwa tatizo kubwa la walimu wengi kuhama. Hivyo Serikali inapaswa ifuatilie kujua ni nini kinachosababisha walimu hawa wanahama kwa wingi? Kwa mfano, katika Halmashauri ninayotoka ya Meatu, katika robo moja walihama walimu 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili linachangiwa na ukosefu wa nyumba za walimu. Kwa mfano, katika jimbo langu, Shule ya Mabambasi miaka mitatu illyopita ilikuwa ya mwisho kitaifa. Ukipika pale, walimu wote sita wanaishi katika nyumba moja; na shule hiyo ni kilomita 30 mpaka Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, familia zao inabidi ziishi Wilayani na wenyewe mwisho wa wiki inabidi waende kwenye familia zao. Kwa hiyo, kunakuwa na gharama kubwa za nenda rudi nenda rudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule moja ya Mwanyagula yenye we ina nyumba moja ambayo sasa inavuja na yule mwalimu amehamia Wilayani. Kwa hiyo, ukipika pale, hakuna mwalimu anayeishi shulenii, inabidi walimu wasafiri kila siku kilomita 20 kwenda na kurudi na hivyo kunakuwa na gharama kubwa ya kimaisha. Naomba Serikali iwekeze zaidi katika miundombinu ya nyumba za watumishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tatizo la miundombinu ya barabara inachangia walimu kuhama kutokana na gharama kubwa ya usafiri, huduma ya maji nayo ni tatizo na umeme nao ni tatizo. Endepo Serikali itasawazisha haya, ninaamini walimu wengi hawatapenda kuomba uhamisho kwenda kwenye maeneo ambayo yana huduma kama ambazo nimezitaja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Maji, Serikali katika mpango wake imeeleza kwamba kwa ujumla miradi yote iliyotekelezwa imewezesha wananchi zaidi ya milioni 25 kupata huduma za maji, hivyo kupata wastani wa upatikanaji wa maji vijiji ni asilimia 70 na mjini asilimia 84 hadi mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoiona Serikali, haipo *serious* na changamoto na upungufu wa maji. Katika takwimu hizo walizozitoa, ukiangalia wananchi wanaopata milioni 25, na Watanzania tuko takribani milioni 50, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba asilimia 50 tu ya wananchi ndio wanaopata maji. Kwa hiyo, takwimu hizi za asilimia 70 kwa 84 haziakisi uhalsia wa upatikanaji wa maji katika maeneo yetu. Ni vyema sasa Serikali ikatafuta nini chimbuko kubwa la ukosefu wa maji ili ije na suluhu, iweke mkakati maalum wa upatikanaji wa maji hadi tutakapokuwa tunamaliza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ajiandae.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pia naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata nafasi ya kusimama mbele ya Bunge hili leo na kuweza kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, ambayo ilifanya marekebisho ya Sheria ya Madini mwaka 2017 na tukaja na sheria mpya na kanuni zake ambazo kwa ujumla zimefanya mchango wa kampuni za madini hasa kampuni kubwa ya uchimbaji wa dhahabu pale kwangu Geita *GGM*kuonekana kwa macho kwa wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia marekebisho hayo ya sheria sasa katika kipindi cha miaka mitatu tu ambayo Bunge hili lilitanya marekebisho, ukifika Geita mjini unawezza ukagundua kwamba marekebisho yale yalikuja katika kipindi sahihi na tayari kuna mabadiliko makubwa na maendeleo makubwa sana ambayo wananchi sasa yanawatoa kwenye mgogoro ambao ulikuwepo awali wa kuona hawa wachimbaji, makampuni makubwa ya madini wanakuja kuchukuba madini yetu na kutuacha watu maskini, ukifika katika Jimbo langu la Geita Mjini utaona kitu tofauti kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili liliwezekana kwa sababu lilitimamiwa vizuri na naamini katika Mpango huu wa miaka mitano ijayo, yako mambo nataka kuishauri Serikali iendelee kuyafanya kazi. Kwa mfano, tulipotunga sheria tulizungumza habari ya *local content* nimsikia Mheshimiwa Rais juzi akisema inafanyika vizuri. Naomba niseme ukweli eneo hili bado halijafanya kazi vizuri, sio kwenye *consultation peke* yake bado *local content* katika mazingira ya bidhaa zilizotajwa katika sheria, *section 102(2) na (3) tumesema* vizuri juu ya bidhaa ambazo hazipatikani Tanzania na tukasema vizuri juu ya namna ambavyo Mtanzania au kampuni ya kitanzania inatakiwa iwe na asilimia ngapi kushirikiana na kampuni ya kigeni ili kuweza kuingiza bidhaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado eneo hili halijasimamiwa vizuri, bado makampuni makubwa yanayo uza bidhaa za gari katika migodi ni makampuni ambayo yamesajiliwa nje na makampuni ambayo yanaleta bidhaa moja kwa moja kutoka nje kuingiza Tanzania. Maana yake ni nini? Kama mgodi matumizi yake makubwa ni kwenye *services*, maana yake asilimia zaidi ya sitini ya mapato ya mgodi ni kwenye *services*. Kama mgodi huo una mapato yake ya dola labda milioni 300, *sixty percent* ya dola milioni 300 ni kwenye gharama za uendeshaji, kama nusu ya hizi zinafanya manunuzi nje, maana yake Serikali inapoteza pesa nyingi sana. Kwa hiyo, ushauri wangu eneo hili lisimamiwe vizuri, ufanyike ukaguzi, sheria *ime-provide*, imetoa maelekezo migodi hii kila baada ya miezi miwili, kutangaza ni bidhaa gani ambazo inazitaka kutoka nje ili kuruhusu Watanzania

waweze kuziingiza. Hata hivyo, bado zimekuwa hazifanyi hivyo na kama zinafanya inafanya kwa kificho kiasi wafanyabia shara wengi wenyewe uwezo wanashindwa kupata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya sheria hii tulizungumza habari ya *CSSR*, inajulikana wazi, kwenye *own source* tunasema *service levy* watalipa *0.3 percent*, lakini kwenye *CSSR* sheria imebaki kimya imeacha jambo lile liko wazi; wengine wanasema *0.7*, wengine wanasema ni *discretion ya investor*. Sasa inatufanya tushindwe kuitumia vizuri hii sheria kwa sababu ni vizuri pamoja kwamba pesa hii ni ya mwekezaji *iprove* *iseme ita-range* kutoka asilimia ngapi kwenda asilimia ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna shida moja kubwa ambayo nalona pamoja na kusifla tunafanya vizuri sana kwenye mahusiano na mgodi, lakini bado shida tuliyonayo kubwa na ambayo nafikiri Serikali inabidi inatakiwa ifanyie kazi ni kwamba pesa hizi za *CSSR* zinatumika unakuta gharama zake ni kubwa kuliko gharama halisi ambazo ziko kwenye maeneo ya masoko ambayo tunanunua bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa tu mfano, sisi tunapata *CSSR* ya bilioni *10*, lakini gharama ya *CSSR* ile unaweza ukakuta mnabishana kuhusu ujenzi wa mradi ambao ungejengwa na halmashauri ungegeharimu milioni hamsini, gharama ya ujenzi wa *CSSR* kwa sababu pesa ni ya kwao utajenga kwa milioni *150*. Kwa hiyo nasema bado sheria hii haiweki wazi sana kwanza ni asilimia ngapi hii *CSSR* ambapo ni kichaka kinajificha, lakini pili ni matumizi ya *CSSR*, ni vizuri sheria ikasema wazi kwa kuwa ni pesa inakuwa *declared* kwenye kodi, basi pesa hii isimamiwe na Sheria za Manunuza za Serikali ambazo tunazifahamu sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya vizuri sana kwenye utalii kwa miaka takribani minne kabla ya *covid* na naomba ni sema kwamba kipimo kizuri cha mafanikio kwenye jambo hili kimekuja kwenye kuharibiwa na mwaka mmoja

baada ya kuingia kwa *covid*. Tunafanya nini ili tuweze kufanya ya tukio la *covid*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia *comment juzi hapa*, habari ya hasara ya *ATCL*. Kulipima shirika la ndege change lenye miaka mitatu kufikiri litapata faida hiyo sio biashara ya nyanya. Shirika la ndege lina-*indirect* vitu vingi sana ambavyo huwezi kuvipima kama unapeleka nyanya pale Soko la Karikoo kwenda kuuza unatoa gharama na vitu vingine. Kuna vitu vingi sana lazima *CAG* hapa angesema pamoja na kula hasara hapa lakini limesaidia *one, two, three, four, five*. Tunataka kuimarisha utalii dunia nzima wanayofanikiwa kwenye utalii wanafanikiwa kwenye mashirika ya ndege. Kwa hiyo maoni yangu kwenye jambo hili, kwanza tuendelee na mpango wa kuliimarisha shirika hili, lakini tujitanue vizuri Zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona tuna *weakness* moja, tunasubiri watalii wanaokuja wenyewe au wanaota futwa na watu. Kiko kitengo kimoja ambacho nchi nyingi kinawapelelea watalii wengi sana hawa wanatumia sana mashirika ya ndege ya ndani cha mikutano lazima pale *TTB*, Wizara iweke kitengo maalum cha kufanya *lobbying*, mikutano mingi duniani inata futwa hajji yenyewe. Wale ndugu zangu wa *AICC* pale wanabiri mikutano ije, mikutano ile mikutano ile ya Afrika Mashariki haiwezi ikasababisha nchi hii iweze kuonekana inafanya mikutano. Ni lazima awepo mtu anafanya *lobbying* na mashirika makubwa duniani yanayoleta mikutano ya watu zaid ya elfu nne na anazunguka duniani kuitafuta hiyo mikutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema hapa Mheshimiwa Shangazi, kuna kinaitwa *economic diplomacy*, ukienda kwenye balozi zetu, nimeenda kwenye balozi karibu nane Tanzania, unakuta *staffing* ni watu wasiozidi kumi *WTO* mikutano peke yake iliyoko Ujerumani katika kipindi cha mwaka mmoja inayotangaza utalii iko zaidi ya hamsini, wale walioko pale watu sita, watatu wameweka *brochures* na vitu vingine kwenye meza na *website* yao ipo *centralized*

Tanzania hawawezi kuleta watalii na kuongeza watalii Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubali kwamba tunatakiwa kama tunazungumzia hao wafanyakazi, tuwa-*empower* tupeleke watu wawe *equipped* na *knowledge*, wapewe pesa wazunguke kwenda kuwatafuta hao watu waje Tanzania vinginevyo tutaendelea kuzungumza habari hii na itaendelea kuwa shida kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, hapa katikati tulipata tatizo kidogo, tunao utalii wa uwindaji, watalii wa uwindaji ni matajiri sana duniani, lakini kuna gharama kubwa sana ya kuki-*manage* kitalu, tunayo sheria kila baada ya miaka mingapi unatakiwa kufanya mnada. Sasa unapofanya mnada, unakuta yule amekitunza kile kitalu kwa miaka mingi anaweza asishinde kulingana na mtu mwingine, anayekuja *interest* yake sio kutunza kile kitalu matokeo yake anapoteza wateja wale wa mwanzo, kitalu kinapoteza thamani na tayari tunandelea kupunguza idadi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu hapa, wale wanaofanya vizuri waendelee kuaminiwa na Serikali, waendee kupewa na waendelee kulindwa. Nasema hivi kwa sababu shida kubwa tullyonayo tunafikiri unataka uuze vitalu kwa mnada, sawa, utauza vitalu vinne, halafu vitalu sabini viko wazi maana yake nini, ningekuwa mimi ningeweza kuvigawa hata bure vyote, halafu ukataka utoze kodi kutoka kwenye vile vitalu kwa sababu kitendo cha kukaa wazi gharama kubwa ya Serikali ni kuvilinda na kuviedesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza hapa mara nydingi kuhusu *TRA*, nashukuru sana Serikali Sikivu ya CCCM imesikia na imetoa maelekezo. Jambo moja hapa nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mara zote wanapoona tunazungumzia Habari ya mgogoro wa walipa kodi na *TRA* inayoweza kula hasara hapa ni Serikali, *negotiation* itakayokuja ulikuwa unalipa milioni tano na hili ndio jambo ambalo nataka kumshauri lazima tuwe

waangalifu tunataka kumpa nani unafuu. Ulikuwa unalipa milioni tano unataka kulipa milioni tatu, wanaweza watu wakatumia vibaya hii *loop* aliyoisema Mheshimiwa Rais, matokeo yake watu wakawa wana-negotiate wanakwambia nipe milioni mbili halafu hapa tutaandika hela kiasi Fulani, tunapoteza pesa ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka kushauri, badala ya kila mwaka huyu mtu anakwenda kukadiriwa kodi ya kulipa *TRA* kwa nini ukikadiriwa mwaka huu usiachwe miaka mitatu unalipa *constant* ile ile halafu baadaye utakapo-*provide* zile *audited accounts* zako waweze ku-reviewhesabu. Kitendo cha kila baada ya miezi tisa unaweza kutengeneza hesabu kinafanya mazingira ya kukaa mezani kila mara kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Kengele ya kwanza Mheshimiwa.

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vuma Augustine Holle atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Saimoni Songe Lusengekile ajiandae.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai mpaka leo, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo ya Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na zao la chikichiki. Zao la chikichi kwetu Kigoma ni utambulisho wetu, ni *identity* yetu, ukitaja chikichi ama mawese Tanzania hii kwa watu inakuja ya Kigoma picha, lakini chikichi kwetu ni ajira lakini pia chikichi ni siasa. Sasa nimesoma Mpango huu wa Miaka Mitano vizuri sana, ni mzuri kwa kweli, lakini niseme tu, nchi hii mahitaji yake ya mafuta kwa mwaka ambayo tunaagiza kutoka nje ni jumla ya tani 570,000 kwa mwaka bado kwa mujibu wa takwimu ya Serikali. Watanzania wanahitaji mafuta tani laki 570,000 kwa mwaka, lakini ambayo tunazalisha sisi Tanzania ni tani 205,000 peke yake. Maana yake tunaagiza kutoka nje tani 365,000. Zaidi ya asimilia 50 ya mafuta ambayo tunatumia sisi watanzania tunaagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika huu Mpango wa Miaka Mitano, Serikali ijikite kuweka malengo ya kuhakikisha kwamba tunaweza kuzalisha mafuta ambayo tunaweza kulisha watanzania pasipo kuangiza nje na inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye matunda yanayotoa mafuta, tafiti inaonesha mchikichi ni namba moja, zao namba moja kwenye matunda yanayotoa mafuta. Ziko ripoti zinazoonesha, wapo waliokuja kwenu Tanzania wakachukua mbegu za michikichi, wakaenda kwao, leo hii wanatumia yanawatosheleza mpaka mengine wana-export kwenda nje ya nchi. Sasa ushauri wangu kwa Serikali kwanza nimshukuru Waziri Mkuu kabisa kwa moyo mkunjufu kwa namna alivyovalia njuga suala la kufufua kilimo cha michikichi na kupendeza katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja mara kadhaa kwa miaka ile ya kwanza, akasisitiza akatoa maelekezo ambapo hamasa imekuwa kubwa sasa, lakini pia kuna mbegu mpya tumepata na kuna chuo kizuri sana kwa ajili ya utafiti wa michikichi kipo. Sasa wananchi wamehamasika wamepanda chikichi kwa wingi sana. Sasa kinachofata hapo ni kwamba wataalam wanasesma inawezekana baada ya miaka mitatu minne uzalishaji wa

mafuta ya mawese uka-*triple* yaani ukawa mara tatu. Sasa hofu yangu ni moja tu, tunapoenda kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mawese, tumejipanga vipi kisaikolojia ili kuhakikisha kwamba tunaweza kuboresha au kuongeza thamani ya mawese ili yasiliwe Kigoma peke yake yaje kuliwa Dodoma pamoja na mikoa mengine na hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawese kwa asili tunatumia kwenye chakula, sisi watu wa Kigoma, lakini kwa sababu yanakuwa kama *crude oil*, watu wengine wanakuwa hawawezi kuyatumia. Sasa ukiongeza uzalishaji kama mara tatu, kama hatujajiandaa kuyatengeneza yaweze kutumiwa na watu wengi kwa maana ya kutanua soko, nina uhakika Mkoa wa Kigoma leo hii dumu moja ni Shilingi elfu kumi. Itaenda kushuka mpaka iende elfu tano elfu mbili. Kwa wale wananchi tuliokuwa tunawahamasisha walime mawese, michikichi wataanza kutupiga mawe kwa sababu mawese ni mengi, lakini hatujatanua soko la mafuta yatokanayo na michikichi ili walaji wawezi kuwa wengi. Kwa maana hiyo mengi yatakuwa Kigoma, utashangaa dumu kutoka elfu kumi itaenda mpaka elfu mbili au elfu tatu na kitakachotokea hapo wananchi wataanza kuichukuia Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu katika hili, ni lazima sasa Serikali kupitia Waziri Mkuu ambaye kwa kweli amekuwa ni rafiki yetu Mkoa wa Kigoma katika hili, tuanze kujielekeza kwenye kuwekeza kwenye teknolojia, tuanze kubuni teknolojia ndogondogo za kuweza ku-*refine* mafuta ya mawese. Kwa kufanya hivi tutaongeza soko la mawese na hata uzalishaji utakapokuwa umeongezeka, tunaamini kwamba wananchi wataendelea kuuza kwa bei ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipiga hesabu mafuta ya mawese dumu moja kama nilivyosema ni shilingi elfu kumi, lakini mafuta ya alizeti ambayo ni *refined* ni shilingi elfu 35 yaani ni sawasawa lita moja ya mawese unauza shilingi 2000 au chini ya hapo, lakini lita moja ya alizeti unauza zaidi ya Shilingi 7000, maana yake nini? Ukifanya *double refine* kwenye mafuta ya lita tano labda *let say unaondoa uchafu*

labda wa robo lita tu. Kwa hiyo unaweza ukaona namna gani ambavyo wananchi wa Kigoma bado tunanyonywa kutokana na teknolojia mbovu na duni kwenye zao la chikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana maelekezo yatoke, *SIDO* wafanye ubunifu wa teknolojia ndogo ndogo ambazo watu wanaweza kumudu hata wananchi wa kawaida. Kama viko viwanda vyta ku-refine alizeti vyta milioni kumi, milioni nane, kwa nini Kigoma ishindikane, kwa nini mawese siku zote yaonekane yana rangi nyekundu. Tunahitaji teknolojia ambayo ni ya bei nafuu ili wananchi hata wa kawaida waweze kununua milioni kumi, milioni nane, waweze ku-refine mafuta ya mawese na waweze kuuza kwa bei nzuri na rafiki kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nizungumzie kidogo kuhusu reli ya *SGR*. Nashukuru tumeona mipango ipo *clear* na kwenye bajeti tunaona *reflection* kuanzia Dar es Salaam, mpaka Mwanza. Sasa ni zamu ya Kigoma; *route* ya kutoka Tabora kwenda Kigoma, ni ukweli usiopingika ukiangalia mizigo inayopita kwenye reli ya katika kwenda Mwanza na inayopita reli ya katika kwenda Kongo, ya kwenda Kongo ni mingi zaidi na kwenda Kongo unapitia Kigoma. Kwa hiyo tunachotaka na sisi kwenye hii miaka mitano, tumeona kuna mambo mengi sana, lakini nasi tunahitaji tuone kwenye makaratasni na kwenye bajeti ni kiasi gani kinatengwa kila mwaka au ujenzi wa *SGR* kwenda Kigoma sasa uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesubiri, sasa ni zamu yetu, tunasubiri ikifika Mwanza tu na sisi tuanze kudai. Sasa Mwanza tumeona mpaka mikataba imeanza kusainiwa, juzi tumeona Waziri yupo kule, sasa na sisi Kigoma ni zamu yetu, tuone mikataba ikisainiwa, reli ijengwe kwenda Kigoma, *it is our time now*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni la umeme. Kigoma sisi hatujaunganishwa na *grid* ya Taifa, ni miongoni mwa mikoa michache sana ambayo haijaunganishwa na *grid* ya Taifa, hii miaka mitano tunahitaji kuona sio *story* tena, mama ametupa msemo mzuri, ukinizingua nakuzingua,

tunakaa humu ndani miaka mitano kwenye bajeti, Mawaziri tunawaomba wakajipange vizuri, Serikali ikajipange vizuri, tunahitaji kuona umeme wa *grid* ya Taifa unafika Kigoma sio ahadi tena, tutasubiri mpaka lini? Tunaposema viwanda vidogovidogo vije hivi, vinahitaji umeme, sasa kama hakuna *grid* ya Taifa, umeme wa jenereta wa kuwasho tu, viwanda vinakuwaje? Kwa hiyo tunaomba Serikali ijipange vizuri sana ili tupate umeme wa *grid* ya Taifa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa nimetenda haki kama sitzungumzia michezo katika nchi hii. Napenda sana michezo, licha ya kuwa Mwanayanga mzuri sana, nawapoongeza Timu ya Simba kwa ilipofika kwa kweli; imejitahidi sana. Na sisi Serikali tuna tabia ya kuvizia mafanikio binafsi ya timu, sisi tunadaka, hata kama ni mazingira mazuri ya Serikali, kwa nini Simba peke yake? Kwa nini nyingine zisifike *level* hiyo ya Simba? Tuweke vizuri mikakati yetu kwenye upande wa michezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na sehemu ya kuanzia, twende kwenye sheria za adhabu mbalimbali za *TFF*. *TFF* wana sheria kali kuliko hata za Kanuni za Bunge hili; wana sheria kali kuliko hata za ubakaji. Yaani leo hii Masau Bwire akiwa-*challenge* kidogo wanamfungia miaka mitano, sasa utafikaje kwenye nani? Uki-*challenge* kidogo, milioni tano, milioni moja, milioni ngapi; hatuwezi kwenda hivyo. Lazima waweke mazingira vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda michezo sana. Na nimekuwa Mjumbe wa *Bunge Sports Club* kwa miaka sita sasa. Na hata jana wakati Mheshimiwa Spika alivyotangaza kwamba fomu zinaweza kuchukuliwa, nilichukua fomu kabisa ya kugombea Uenyekiti wa *Bunge Sports Club*. Kwa hiyo, naamini muda ukifika hata wewe – kwasababu amesema wewe utakuwa msimamizi wa uchaguzi – muda ukifika ntaomba kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tujikite vizuri sana kwenye suala la michezo. Michezo ni ajira. Na kweli mimi

kama ntapata nafasi hiyo ntaonesha mfano kwenye michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu jambo lingine moja, nimeona kwenye ujezi wa miundombinu, hasa barabara... ya kwanza, ya pili hiyo?

NAIBU SPIKA: Ya pili.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba kura yako.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge nadhani mnahusika kwenye hivyo vilabu vya michezo lakini pia kwenye TFF. Nadhani tupeleke hayo mawazo mahususi mahali, lakini yasiwe yale ambayo wewe una maslahi fulani kwasababu unaweza ukazisema adhabu leo kwasababu si mtu wako aliyeathirika ama akiwa ameathirika ukaiona changamoto, lakini tuangalie mambo yale ambayo yanafanywa na yanakataza na kwa nini adhabu imewekwa kubwa.

Tusije tukajikuta hapa Wabunge tunaanza kujadili mambo ambayo yanafikia kwenye ubinafsi sana lakini pia pengine kwenye mpira ni ya muhimu. Najua hata huko FIFAH huwa sheria zake ni ngumu sana, nazijua kidogo. Nadhani tuangalie, kila sehemu ambayo tunaweza kushiriki na kutoa huo mchango basi tutoe mchango huko tuone mabadiliko hayo na yawe yanaielekeza nchi yetu kwenye maendeleo kimichezo na siyo yanaturudisha nyuma kwa kwenda kinyume kabisa na utaratibu ulipo duniani kwingine.

Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatia na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Kipekee kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kutukutanisha tena hapa tuzungumzie Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano,

2021/2022-2025/2026, uliobeba dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wetu sisi wote tumeletwa na watu humu ndani, na sisi wenyewe ni watu na mahitaji watu waliotutumia waliyonayo ni sawa na tuliyonayo. Naipongeza Serikali kwamba hatukuwa timesimama tukipiga *mark time* bali toka ule mpango wa miaka mitano mitano ulipoanza mambo mengi yamefanyika; barabara zimejengwa, maji yameboreshwa, elimu imekwenda mbele, lakini kiubinadamu tu jambo likishatekelezeka halina motisha tena. Alisema *guru wa management, once a need is satisfied it's no longer a motivation*. Na hilo ndiyo linatufanya kila siku tuone kwamba kuna jambo la kutendeka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza pale kwenye viwanda, na ninazungumzia kwenye viwanda katika mpango wamepanga kuzuia au kulinda viwanda ambavyo vinaagiza vitu kutoka nje ili vile vyta kwetu vinavyotengenezwa viweze kupata soko na pia viboreshwae.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitakwenda moja kwa moja kwenye viwanda vyta sukari. Sukari ni bidhaa ambayo inahitajika na kila mtu, na sasa hivi ninavyozungumza ni siku chache tu wenzetu Waislam watakwendwa kwenye Mfungo Mtukufu wa Ramadhani, na sukari ni bidhaa ambayo inahitajika sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na sukari siku zote imekuwa mfungo huu unatokea wakati ambapo viwanda viko kwenye *maintenance* na vitafungwa au vimeshafungwa kwa ajili pia ya mvua. Lakini sukari hiyo mpaka mwaka jana ikifika wakati huu sukari inaadimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyngi tumezungumza hapa; Serikali inafanya sasa kuhakikisha kwamba sukari haiadimiki tena. Kumbukumbu zangu zinanikumbusha kwamba Waziri wa Kilimo alisema mwaka huu shida hiyo haitakuwepo. Na namuomba Mungu shida hiyo isiwepo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama haitakuwepo ninachotaka kusema kuhusu viwanda vya sukari ni nini; kwa kuwa shida kubwa inayotokea ni kwamba wale wanaoagiza sukari wanasema wanaagiza sukari ya viwandani, ile sukari nyeupe nyembamba ile na siyo sukari ya kula watu, wao waagiza *industrial sugar*. Lakini unakuta kwamba wanachanganya humohumo na kuja kufanya *repacking*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, Serikali sasa ione kwenye mpango huu inaboresha au inawasukuma hao wenyewe viwanda vya sukari hiyo sukari ya viwanda itengenezewe hapa hapa nchini. Tuna viwanda vingi vya sukari vikiwemo *TPC*, Kilombero, *Mtibwa Sugar*, vingine wamesema vinakuja Bagamoyo, vingi tu. Sasa naomba kabisa kwenye mpango huu tuelezwe ni viwanda vingapi vya *industrial sugar* vinakwenda kufunguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu nimeona mambo yanayohusu utawala bora lakini sikuona utawala bora kwenye ngazi ya chini; tuna watendaji wa vijiji, tuna watendaji wa kata. Watendaji hao ni watu muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku, watendaji hao ndio wanaoishi na wananchi wetu, watendaji hao ningetaka iandikwe watapewa elimu. Na wanapewa elimu gani; elimu sasa ya kuweza kujenga kanzidata kuhusu mambo yanayofanyika kwenye maeneo husika yakiwemo yale ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila aliyesimama hapa amezungumzia kilimo, nitazungumzia kilimo kivingine, ya kwamba tuwe sasa na *database* ya kujua ni mazao gani yanayolimwa kwenye eneo fulani na ni ukubwa wa eka ngapi yanalinwa? Na ni wakulima wangapi wanalima mazao hayo, na yanavunwa kiasi gani. Wakati huo tukiwa na rekodi hiyo, Serikali inakuwa tayari ina rekodi ya kutafuta masoko. Wanatafuta masoko na tukishapata haya mazao wanakwenda sasa kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna changamoto moja; kijijini wakishavuna wanakwenda likizo. Wamevuna wanafanya sherehe, kwingine wanaweka kidogo akiba,

hakuna kuunganisha sasa nini kinafanyika, wanakaa hivyo mpaka msimu mwengine. Na ukizingatia kwamba sisi kilimo chetu kinategemea zaidi mvua za msimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali yangu sikivu iangalie sasa baada ya kilimo – na sasa hivi kuna vijana wengi ambao wako vijiji; wako waliomaliza *form six*, wako waliomaliza chuo kikuu na pia wazazi wao – watu hao wanawekwa katika zoezi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda tu nitoe mfano kidogo wa kule Libya alipokuwa, Hayati sasa, Muammar Gaddafi. Yeye alikuwa vijana wakifikia rika fulani kama anakwenda kupata mwenza basi anamzawadia dola 5,000. Sisi Tanzania hatuna hizo *petrol dollars* lakini Mungu ametubariki kuwa na eneo kubwa, tuna ardhi kubwa na vijana hawa wangeweza kabisa wakafunguliwa maeneo wakapewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo lazima kama umezaliwa kule ulikotoka hakuna maeneo, basi watoke kule waende kwenye maeneo mazuri. Hata kama watakuja Mbeya, kule Rungwe kuna maeneo mazuri tu, au Sumbawanga, wakagawiwa maeneo mazuri wakafungua mashamba ikajulikana ni *batch* gani, ni mashamba yapi wakaenda wakalima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wakishalima mashamba hayo wanafungua sasa ukurasa mpya wa kilimo cha wasomi. Ninaomba sana mpango huu uweze kufikiria namna ya kuwafungulia au kuwatawanya vijana wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposimama kuzungumza yalikuwa yanazungumziwa mambo ya michezo. Naomba niliendee vingine, naona huku ndani Waheshimiwa wanazungumza timu zile kubwa tu za watani wale wawili. Sasa hao wachezaji mnaowajua wakishaondoka - sitaki kuwataja majina maana yake mnaweza mkacheka, japo nina timu yangu fulani – ni lini sasa sisi tulio hapa ndani na

Serikali kwa ujumla, Wizara ya Habari na Utamaduni, itashuka chini kule kwenye kata tuwe na timu za kata? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na isiwe kazi ya Mbunge tu, Serikali ipeleke wataalam, tuwe na timu za wilaya, tushindanishe watu. Hapa ni mtu mmoja tu anayefahamika ikitajwa inajulikana ndiyo kule kwake, inaitwa Namungo eeh? Eeh, Namungo tu ndiyo inayofahamika hapa, labda kwa vile kiongozi huyo alikuwa refa. Sijasikia, naskia wanantajia Singida na nini lakini sijasikia Nkasi, sijasikia Mbeya. Ila nikupongeze, umewatoa Mbeya kimasomaso kuna *Tulia Marathon*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nawaomba, Waheshimiwa kila wakati wanachukua jezi kupelekea wachezaji wao, lakini hatujazisikia timu zao. Mpango huu kwa kuwa michezo ni ajira basi ishuke chini, tuandae vilana wetu toka utotoni wakue wakijua michezo na waendelee kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kumekuwa kuna shida na ugomvi mkubwa kuhusu *TARURA*, na kilio, *TARURA*, *TARURA*. Lakini kwenye mpango sikusikia Mfuko wa Barabara. *TARURA* inajenga barabara, ikishajenga inaacha, kuna Mfuko wa Barabara ambao ndiyo unaotunza barabara, ulikuja hapa Bungeni mkautungia sheria. Tutagombana hapa na *TARURA* lakini tunamgusa ambaye siye. Hebu tutafute chanzo cha ugonjwa kiko wapi. Naomba mpango huu utueleze kuhusu Mfuko wa Barabara, hela zile zimegawanywa vipi au zinakwenda kwa jinsi gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mfuko wa Maji; tumesikia ujenzi miundombinu ya maji lakini hatujui ule Mfuko wa Maji unakwenda vipi. Mtandao wa maji safi na salama unakwenda kasi, lakini mtandao wa maji takaa hatuuusikii ukitajwa. Itakuja siku, na sasa hivi hizi mvua zikituvuruga kidogo tu ukipita kule Jiji kama Dar vinyesi vinaelea juu kwenye zile barabara za halmshauri/jiji, wanachomekea kule ile mipira inatokea. Ninaomba mpango huu uelekeze sasa mnapotaja

maji mtaje maji safi/ salama na usafi wa mazingira... kengele ya ngapi?

NAIBU SPIKA: Ya pili.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuwa hapa. Lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa nchi yetu. Nimpongeze pia Mheshimiwa Vuma kwa kuitambua na kukubali mafanikio ya Timu ya Simba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite katika mambo machache sana kuchangia mpango huu ili kuendelea kuimarisha uchumi wetu. Lakini ijlilikane ya kwamba ni lazima sisi kama Wabunge tuendelee kuisimamia Serikali ili tufikie ule mpango ambao unasemwa sasa wa *per capita income* dola 1,400 katika hii miaka mitano ijayo. Kwasababu sasa ni 1,080 na *cut off* ni 1,036. Kwa hiyo, bado tuko katika eneo ambalo si salama kwa sababu tofauti yake ni dola 44. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Nchi ya Algeria mwaka 2019 *per capita income* ilikuwa 4,060 lakini 2020 ilishuka ikawa 3,970. Kwa hiyo, kushuka pia inawezekana. Kwa hiyo, sisi kama Wabunge lazima tuisimamie Serikali ili uchumi wetu uendelee kupanda kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameeleza katika mambo matano ambayo ameyazungumza yatakayokwenda *ku-reflect* uchumi wetu. Na ninaomba uchumi huu sasa uende uka-*reflect* kwa wananchi hawa waliopo huko kwenye majimbo yetu na wananchi kwa ujumla wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Simiyu ukitafuta *identity* yetu ni zao la pamba. Lakini wananchi wetu wameshapoteza *hope* na zao la pamba. Kwa nini; kwasababu ya bei ya zao la pamba. Leo ninataka kuzungumza kidogo kuiomba Serikali kutafuta namna ya kuwezesha Mkoa wa Simiyu kuupelekeea kiwanda, hasa cha kuzalisha vifaa tiba vitokanavyo na zao la pamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata kiwanda hiki maana yake zao la pamba sasa bei yake itaenda kuimarika. Na zao la pamba likiimariika maana yake sasa tutarudisha morali ya wananchi wetu kulipenda na kulima tena zao la pamba ambalo litaongeza uchumi wa wananchi wetu walioko huko kwenye Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kiwanda hiki kitasaidia nchi yetu kwa namna ya pekee sana kwasababu kitazalisha zaidi ya ajira ambazo ni rasmi 600 na ajira ambazo si za moja kwa moja zaidi ya 1,000. Wananchi watapata ajira, watalipa kodi, watapata kipato, na hii sasa itakwenda kuimarisha uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe Wizara ya Uwekezaji iendelee kuhakikisha kwamba inawekeza kiwanda hiki katika Mkoa wa Simiyu ili zao la pamba, kama nilivyosema pale awali, liweze kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitengeneza vifaa tiba vitokanavyo na pamba maana yake tunakwenda sasa kuimarisha kutokuagiza vifaa hivi nje zaidi ya asilimia 38.3. Asubuhi timesikia hapa, tunaagiza zaidi ya asilimia 80. Sasa tukiwekeza kwenye kiwanda hiki tunakwenda kupunguza uagizaji kwa asilimia zaidi ya 38.3 ambapo tunatumia zaidi ya bilioni 147 kila mwaka kuagiza vifaa tiba nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni imani yangu kwamba Waziri wa Fedha, Mawaziri wanaohusika, mtatusaidia kuhakikisha kwamba tunapata kiwanda kule Mkoa wetu wa Simiyu ili tuweze kuzalisha vifaa tiba vikiwemo

cotton gauze, cotton swab na nguo za madaktari na manesi pamoja na mashuka ambayo yanaweza kutumika katika hospitali zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe Wizara ipunguze tozo mbalimbali kwa ajili ya wawekezaji. Lakini pia mamlaka husika ziwe na lugha moja, hasa mamlaka zinazotoa vibali kwa hawa wanaokwenda kuwekeza kwenye miji yetu. Nilitaka nizungumzie sana hapo kwenye eneo la kilimo ili wananchi wetu sasa wakanufaike. (*Makof!*)

Kwenye eneo la kilimo bado hatujawekeza mahususi katika kilimo cha umwagiliaji. Bado hatujatumia Ziwa letu Victoria, hasa kwenye Mwambao wa Ziwa Victoria, bado hatujalitumia vizuri katika suala zima la kilimo cha umwagiliaji. Uktianzia kule Rarya, ukija Musoma, ukija Bunda, ukija pale Busega, ukienda Magu, Mwanza, Sengerema, Buschosa na huko mpaka Bukoba, bado hatujatumia ziwa letu katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, niombe Wizara ya Maji ijikite kuhakikisha kwamba tunaimarisha miundombinu ili tuwe na kilimo cha umwagiliaji katika sehemu zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza mradi ulioko mkubwa wa kuleta maji hapa; mzuri sana. Lakini pia niseme sisi ambaao tunazungukwa na Ziwa Victoria bado tuna shida kubwa ya maji. Mfano kwenye Wilaya ya Busega wanaotumia maji safi na salama ni asilimia 42.9; bado tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunapokuwa tunaangalia suala hili la maji pia tuone kabisa kwamba linaenda *ku-reflect* kilimo cha umwagiliaji kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kuchangia hapa ni eneo la asilimia 10 ambazo zimepangwa kisera kwenye halmashauri zetu, ambapo asilimia nne ni kwaajili ya vijana, asilimia nne kwaajili ya akina mama na asilimia mbili kwaajili ya walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ipo kisheria na imepangwa lakini cha kusikitisha ni kwamba haifuatwi na hakuna anayefuatilia. Unakuta Halmashauri imepata mapato ya ndani safi lakini asilimia ambazo zinaenda kwenye *group* hili hazifiki hata 10, na hamna anayehoji wala anayesimamia. Wakurugenzi hawaojiwi, *business as usual*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili lazima tulisimamie. Kama ni asilimia 10 itengwe kweli, kama makusanyo ya ndani ni bilioni moja asilimia 10 ni milioni 100, *no discussion* kwenye hili, ipelekwe milioni 100 sehemu husika. Lakini sasa hivi inaweza ikawa milioni 100 zikaenda milioni tano, milioni saba, hamna anayehoji, hamna anayechukua hatua, ni lazima eneo hili twende tukachukue hatua ili sasa vijana wetu tuwaimarishe na waweze kupata fedha hizi ili sasa waweze kuzitumia katika kuinua kipato chao pamoja na hawa akina mama na watu wenye ulemavu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kidogo kwenye eneo la maliasili na utalii. Nimesikia kengele ya kwanza. Ukitoka Lamadi kuelekea Bunda pale katikati ya Lamadi na Bunda kuna wanyama wa Mbuga ya Serengeti. Ningeishauri Serikali, ili kuinua pia uchumi wa maeneo yale tufungue namna ya wanyama wetu waweze kwenda hadi ziwani, ukienda pale Nyatwali wanyama waende mpaka ziwani. Nasema hivi kwasababu itafungua uwekezaji katika Miji yetu ya Lamadi na Bunda na wananchi wa pale watazidi kunafaika na hali halisi ya uwekezaji ambao utapatikana maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe Wizara ya Maliasili iliangalie hili, ni eneo mojawapo ambalo tunaweza kuwekeza na ni eneo mojawapo ambalo linaweza kuipatia fedha Serikali, na hasa hasa katika hizi sehemu ambazo nimezitaja ikiwemo na mji wa Lamadi ambao sasa ni mji mkubwa, pamoja na mji mwagine wa Bunda. Eneo hili lazima tulitazame ili liweze kuingiza kipato katika eneo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie kidogo habari ya *TARURA*, *TARURA* lazima tuitafutie fedha; kama *TANROAD*

wanapata asilimia 70 na *TARURA* asilimia 30 kuna haja ya kuzungumza hapa tena. Kuna haja ya kuendelea kuingalia *TARURA* kwa jicho la pili, kuna haja ya kulingoza fedha ili maeneo yetu sasa yatengenezwe. Kule vijijini na kwenye majimbo tatizo la *TARURA* ni kubwa, tatizo la *TARURA* linalalamikiwa kila mahali. Barabara hazipitikim ukienda pale jimboni kwangu barabara ya kutoka Mwamanyiri kwenda Badugu haipiki, barabara nyingi hazipitiki. Sasa hata kama wazalishaji wa pamba watazalisha hatimaye tutazungumza tena habari ya barabara. Kwamba sasa gari zinaendaje kuchukua pamba huko ambako pamba imezalishwa kuja hapa mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa tunazungumzia kuimarisha uchumi wa watu na kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja lazima pia tuziangalie bajeti ya *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe Wizara ya *TAMISEMI*, lazima tuje tuzungumze, na hapa lazima tuje tuone hali halisi ya namna ya kuiwezesha *TARURA* ili iweze kufanya kazi kubwa kwa ajili ya wananchi wetu. Wapo wengine ambaao wamekuwa wakisema irudi *TANROAD*, Wizara ya Ujenzi lakini hapa *issuesio* kurudi *TANROAD issue* ni kuiongezea fedha ili iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na kazi iendeleee. (*Makofii*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Festo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nipende kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri ya mpango ambaao tunaujadili kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye mpango huu naomba nizungumzie jambo moja tu ambalo linahusu sekta ya michezo; na mimi ni mdau wa michezo na nimekuwa

kiongozi wa michezo kwenye nchi hii. Kwa leo naomba niitakie kila la heri timu ya *Simba Sports Club* kwenye michezo wake pale Misri, na ninaamini kwamba hata wanayanga wenyewe wanaendelea kutuunga mkono kama ambavyo imekuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye michezo naomba nizungumzie mambo kadha wa kadha. Ninaanza na jambo suala la sheria namba moja kwenye kanuni 17, sheria 17 za mpira wa miguu ambazo zinahusu mambo ya viwanja vya mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumebahatika sana, takriban kila mkoa tunaviwanja vya mpira wa miguu. Serikali kwa muda mrefu lakini pili sisi kama Chama cha Mapinduzi kwenye ilani yetu kwa muda mrefu tumekuwa tukiweka kwamba tunauwezo na tunafursa ya kuviendeleza viwanja vyetu vya mpira wa miguu. Ukienda ukurasa namba 30, 245 kwenye ilani ya mwaka huu inazungumzia ujenzi wa viwanja kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulibahatika Mwalimu Nyerere alijenga viwanja maeneo mazuri na viwanja vikubwa ambavyo hadi leo kizazi hiki inavitumia. Hata hivyo sijaona mpango wa moja kwa moja kwa Serikali na Chama cha Mapinduzi amba ni wamiliki wa viwanja hivi kuendeleza viwanja vya mpira wa miguu. Tumeishia kulalamika kwamba viwanja sio bora, sio vizuri lakini hakuna hatua ya moja kwa moja ambayo Serikali imekuwa ikifanya na kuichukua kwa kuhakikisha kwamba inaviendeleza viwanja hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe na niishauri Serikali. Viwanja visto maeneo mengi na maeneo *potential*, viwanja kama Sokoine, CCM Kirumba, Ali Hassan Mwinyi – Tabora, vinahitaji tu fedha ya kuweka hata *carpet* tu mpira uchezwe kwa sababu majukwaa Nyerere alishatujengea, yako imara na yako vizuri, kinachohitajika ni fedha tu zitengwe kwa ajili ya kuweka hata *carpet*.

Mheshimiwa naibu Spika, niunganishe moja kwa moja, tunahitaji kuwa mpango wa moja kwa moja. Sisi wote hapa tunafurahia leo, kwamba timu zinacheza vizuri, Timu ya Simba, timu ya taifa zote zinacheza vizuri, lakini ikifungwa tunaanza kulaumu. Hata hivyo kusudi na malengo ya moja kwa moja ya Serikali kuendeleza michezo hatujaiona. Tunazungumzia viwanja hivi lakini hadi sasa hatujaona Serikali ikitoa kodi kwenye vifaa vya michezo. *For instance*, hizo carpet ambazo tunazzungumzia, ingetenga hata mwaka mmoja kwamba huu ni mwaka wa *exemption* kwenye vifaa vya michezo kwa ajili ya kutandika carpet kwenye nchi yetu; hata viwanja viwili viwili tu kwa kila mwaka, kwa muda wa miaka mitano tunaviwanja 10 vimetandikwa kapeti mpira wetu unachezwa na watoto wanaweza kupata sehemu ya kuchezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iondoe kodi au iweke *tax exemption* kwenye vifaa vya michezo; kuanzia jezi lakini pia hizo *carpet* ambazo tunaweza tukazitandika kwa ajili ya viwanja vyetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu pika, jambo linguine, zamani wakati tupo na timu ya taifa tulikuwa na shule nyingi ambazo zinazilisha wachezaji; mathalani shule kama ya Makongo, ambayo ilizalisha wachezaji wengi ambao tulikuwa tunawasifia wakina Kaseja na wachezaji wengine. Tunaomba mpango wa makusudi wa Serikali kujenga shule maalum kwa ajili ya michezo kwenye taifa hili. Shule ambazo *either* zinaweza zikawa za *zonal* kwa maana ya kanda kama Dodoma, Mbeya, Mwanza na hata Kusini wajenge shule angalau 10 au tano za michezo tu ambazo zitakuwa *zina-feed* timu yetu ya taifa na vilabu vyetu vya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu wachezaji wetu ambao tunao hapa hawana uchezaji wa mpira ambao umepitia kwenye darasa, wengi wametokea mitaani, hawana shule maalum kwa ajili ya taifa letu ambazo zinasimamiwa ama na TFF ama na Serikali. Tunahitaji kuwa mpango wa muda mrefu kuhakikisha kwamba michezo ya taifa hili inakuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha, yeye ni mdau wa michezo wa moja kwa moja. Leo hii yeye ni Waziri wa Fedha; aone haja ya moja kwa moja kuinua soka la nchi hii. Amekuwa na *club* ya *Singida United* na amewaona jinsi ambavyo ni ngumu kuiendesha; ni kwa sababu timu nydingi hazina fedha. Je? haoni sasa kuna haja ya Serikali, kama nilivyosema, kuondoa kodi kwenye hivyo vifaa? Na isiwe tu kuondoa kodi kwenye hivyo vifaa, lakini pia kampuni, kama *betting companies*, ambazo zipo ndani ya nchi hii zizonafanya kazi za *betting* nchi hii haziwezi kuijendesha kama si mpira, maana yake wananufaika moja kwa moja na mpira wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je? Serikali haioni fursa kwa sasa, kwamba kampuni zote za *betting* ziwekewe angalau sheria au utaratibu? Kwamba kila kampuni ya *betting* iwe na uwezo wa *ku-finance* au kuchangia au *ku-sponsor* timu yoyote ya ligi kuu? Ziwe za wanawake au timu ya taifa, au timu hizi ambazo tunazo kwa sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuione fursa ili *betting companies* ziweze *ku-support* kwenye mpira wa Tanzania kwa sababu nazo *existence* yake, uwepo wake hapa nchini ni kwasababu ya mpira wetu. Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali muone haja ya kuweka mazingira salama kwa ajili ya timu zetu kuweza kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendesha timu za ligi kuu ni kazi ngumu sana, vijana hawa hawana hela, hawana fedha, tunahitaji hatua za makusudi *kuwa-support*, na kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikusihii na nikuombe, *tax exemption* kwenye vifaa vyta michezo lakini pili hizi kampuni zingine za *betting*; lakini si kampuni za *betting* tu. Tuchukue hata utaratibu ule wa Zambia kipindi cha Kenneth Kaunda kwenye kampuni ya migodi; aliamua kutangaza wazi kama kuna kampuni ipo tayari *ku-finance* vilabu vyta ligi kuu vyta nchi yetu; ile KK11 ilikuwa *financed* na makampuni ya

migodi, kwamba tutawaondolea sehemu ya kodi hiyo kodi ipelekwe kwenye michezo; fanyeni hivyo ili *msa-port* michezo ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka nizungumzie, sitazungumza kwa muda mrefu sana; ni jinsi gani ambavyo tunaweza kulinda wawekezaji kwenye michezo yetu? Nataka hapa niweke *case study* ya Simba Sport Club na hata *Young African* wanatuunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Simba imepata uwekezaji ambao wanahainga nao na upo kwenye *public* na Serikali imeingilia kwamba inasimamia ule mchakato uende salama, *the same to Young African*, wana uwekezaji ambao mchakato wake wameshauanza. Sasa, je wawekezaji wetu wanalindwa? Hawalindwi, *intimidation na frustration* kwa wawekezaji wetu zimekuwa ni kubwa kwa kiwango ambacho wawekezaji wakati mwingine wanataka hata kukata tamaa. Simba leo ambao tunajivunia, kila mmoja anajikonga kifua kwamba ni Simba kwa sababu inafanya *performance* ni kwa sababu muwekezaji yule ameweke fedha pale, ameweke fedha lakini kuna watu wanajitokeza *wanawa-frustrate* kati kati ya mapambano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Simba leo ikibeba klubu bingwa Africa, Tanzania itatangazwa *all over the world*. Si hivyo tu pia tutafungua nafasi kwa mawakala wa wachezaji kuja kufuatilia soka letu la Tanzania. Je, wawekezaji wetu wanalindwa? Serikali ione haja, watu ambao *wana-frustrate* wawekezaji, kama Mheshimiwa Rais alivyosema, wawekezaji wasibughudhiwe. Yule mwekezaji si mwizi, mchakato upo *open kabisa*, uko wazi lakini amekuwa *frustrated* kwa muda mrefu. Akifanya hiki huyu anaingia anasema hivi, akifanya hiki huyu anaingia anasema tunakata bilioni 20. Bilioni 20 hasa hasa kwa *Simba Sport Club*? Kwa posho ya mwaka huu *is over one billion*, posho tu. Mwekezaji anaweka *over 1.5 billion* ruzuku, *what is* bilioni 20 kwa Simba iliyookolewa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe uwezekano wa Serikali kulinda wawekezaji ambao wanaingiliwa, hasa kipindi

kama hiki ambacho Simba inaenda kuchukua ubingwa na kuweka historia kwenye taifa letu. Kwa hiyo lazima tuwalinde.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalisema hili kimasihara, lakini niseme wazi, Simba inaenda kuandika historia nyingine. Je, hii historia inayoenda kuandikwa inalindwa? Simba inaenda kwenye robo fainali mtu mwingine anajitokeza anatoka billioni 20, billioni 20 za nini? mshahara wa Chama, mshahara wa Bernard Morrison ni zaidi ya billioni 20. Mtu kaamua kuwekeza kwa maslahi na mapenzi ya soka Tanzania, ni vema akapewa heshima na akalindwa. Serikali ione haja ya kuwaita pembedi watu ambao *wana-frustrate* na *ku-intimidate* na kuwaambia kwamba huu mchakato haujaisha na si mchakato wa wizi, ni mchakato uko wazi na wanasimba wameridhia kwenye mkutano mkuu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe, Serikali lendelee kulinda. Vilevile na Dar Young African tunawatachia kila la heri, tunajua nanyi mnaenda huko, mnatufata sisi, tunaamini mtafanikiwa. Sasa na ninyi mkiruhusu michakato hii watu kuingilia wawekezaji watakata tamaa, GSM watajitoa pale Yanga kwa sababu watu hamlinde wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kuhusu suala la kusaidiwa kwa *TFF*. *TFF* ni chombo chetu ambacho tunacho, kinafanya kazi, lakini mzigo wa *TFF* ni mkubwa. Ninaishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete aliamua kuchukua sehemu ya mishahara ya *bench* la *TFF*, akasaidia kuibeba *TFF*, kwa maana ya kulipa makocha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuisaidie *TFF*, *TFF* kwa pale walipofikia bajeti yao ni ndogo sana. Timu ya taifa tunatamani ifanya vizuri, kufanya vizuri kwa timu ya taifa ndivyo taifa letu linavyoendelea kutangaza kimichezo na kuendelea kufungua fursa. Serikali inaweza ikachukua jukumu hata la kulipa mishahara tu ya makocha ikasaidia *TFF*. *TFF* yetu pale tukiangalia ofisi zao hazina hadhi. Somalia kuna vita lakini wana ofisi nzuri kuliko hata ofisi yetu ya *TFF*. Ni kitu ambacho kinatia aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione haja ya hata kuishauri *TFF* wajenge majengo yenyé hadhi nzuri, lakini si hadhi nzuri tu bali pia muipokee mzigo, mzigo wa *TFF* ni mkubwa, wamejitahdi kwa *level* yao. Leo hii tuna timu za wanawake na tuna timu ya taifa zinafanya vizuri na vile vile kuna vilabu ambavyo vinafanya vizuri. Basi Serikali ione sasa, kwamba hawa wenzenetu wanapambana kwa *level* hii lakini kuna majukumu mengine tuwapunguzie, mionganoni ni suala la mishahara, wapunguziwe mishahara *TFF*, Serikali ione haja jinsi kuingilia na kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya hapo tuseme tu, Serikali muendeleee kuiunga mkono Simba, inaenda kuandika historia ya tofauti kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, waheshimiwa Wabunge tunamalizia na Mheshimiwa Flatei Massay, lakini nadhami mmepeata picha ya Mbunge akichagua kuchangia jambo moja anaweza kulichangia kwa uzuri zaidi kuliko ukiwa na mambo kumi unataja la kwanza, la pili, la tatu mpaka kumi yote ujataja hata sentensi haijakamilika, Mheshimiwa Flatei Massay.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipongeze Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2020/2025 ambao umeletwa hapa. Mpango huu nimeusoma vizuri sana, ni mpango mzuri sana, lakini ninayo machache ambayo napenda kuyaelezea katika mpango huo. Ukiangalia mpango uliopita wa pili utaona jinsi ambavyo uchumi ulikuwa unasogea kidogo kidogo, lakini pia uwekezaji katika mpango huu katika eneo letu la kilimo haujawa vizuri sana. Sasa naomba na kushauri kwamba; Dkt. Mwigulu Nchemba umesoma vizuri sana. Ukiangalia sasa wakulima wetu ndio walio wengi, na zaidi ya asilimia 70 ni wakulima. Sasa ni vyema tukaangalia namna gani mpango utawa-favor

watu wengi hawa ambao kimsingi uchumi wao unategemea kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia saa hizi kilimo kimekuwa kwa asilimia tatu peke yake. Kwa nini iko hivyo? Ni wazi kwamba mpango uliopita haukwenda vizuri sana katika eneo hili ili *ku-favor* Watanzania katika suala la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini? Wizara zote hizi ambazo zipo katika Serikali zinatakiwa ziende zkipangilia kuendana na mpango unaowekwa kwa kila mwaka.

Mheshimwia Naibu Spika, na sasa ukienda kuangalia Tanzania kama nchi hatuko pembedi ya dunia. Ukiangalia sisi bahati nzuri tunapata mvua za misimu na hatuwezi kabisa kulima kupitia mvua hizi kwa sababu kuna wakati unafika mvua zinalsha.

Kwa hiyo nishauri, kwenye Wizara ya Kilimo mkija na bajeti muweke bajeti ambayo itasaidia kujenga mabwawa katika maeneo yote ya nchi hii ambako utaweza kuzuia maji kwa wingi ili basi tukawa na kilimo cha uhakika, na kilimo hiki kikishakuwa cha uhakika maana yake uvunaji wa uhakika unaonekana; pale ambapo mwananchi anaweza kunyeshea mazao yake na akavuna kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia leo tuna mikopo ya wakulima, unamkopesha mkulima huyu kutoka benki aende akalime, lakini anakwenda kulima kwa kutegemea mvua za masika, mvua zikiisha au zisipofika wakati wake mvua ikawa kidogo maana yake ni kwamba yule mkulima sasa anakutana na kitu kinachoitwa deni, na hilo deni lazima alipe. Lakini kumbe Serikali ikijiandaa vizuri ikaenda kuweka mabwawa katika maeneo yetu kule vijijiini wakulima wale wakaweza kunyeshea yale mazao kwa hiyo utakuwa umemsaidia yule mkulima kwanza, atakuwa na uwezo ye ye mwenye wa kulima na atawea kuvuna na kulipa Serikali. Kwa hiyo utakuwa umemuinua mwananchi moja kwa moja kutoka chini katika mazingira ya kujenga mabwawa ya kunyeshea.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo mengi yana maeneo hayo ya kunyeshea lakini si kila mahali. Ukiangalia nchi nyingi za nje zimekopa mambo mengi toka Tanzania. Ukiangalia kilimo cha korosho ukienda Cuba utakuta walichukua mbegu kwetu. Pia ukienda katika suala la mbegu na pembejeo hizi za kilimo imekuwa tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukienda kununua mbegu ni ghali; na mbegu zote zinatoka nje ya nchi, mbegu zinazotoka nje ya nchi zinakuwa ghali zikifika kwa wakulima wetu; kwa mfano sasa hivi mbegu zinatoka Kenya. Lakini ebu tujiangalie sisi kama Watanzania, tumeshindwa kweli kuzalisha mbegu nchini? Na kwa nini tusizalishé mbegu nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna Watanzania wengi vijana wameenda shule hawana kazi, tunalia namna ya kuwatafutia ajira, lakini kumbe tunayo ajira. Ajira tuliyonayo ni ipi, ukienda ukawapatia eneo kubwa tu vijana hawa ukawawezesha wakalima mbegu, mbegu hiyo itashuka thamani, na ikishuka thamani ni wazi kwamba wakulima wetu watanunua mbegu katika hali ambayo iko chini. Leo hii mbegu ni ghali, inapotokea mbegu zinakuwa ghali vijana wetu hawawezi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya China imeendelea kwa sababu ya wingi wa watu wake, imewapa kazi ya kufanya na kazi hiyo wanayofanya inawaletea kipato katika nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe kabisa, Mheshimiwa Mwigulu nakumbuka maneno yako ulipokuja kusoma kwa mara fulani bajeti hii hapa ya kwako ulisema hivi; '*ukitaka mali utaipata shambani*', mwisho wa kunukuu hotuba yako, wakati huo ukiwa Waziri wa Kilimo na Mifugo enzi hizo. Sasa ndugu yangu leo umepewa Wizara hiyo angalia namna gani ya kusaidia kilimo moja kwa moja. Ukifanya hili utakuwa umeisaidia sana Serikali kunyanya watu wote na kuwa katika kipimo kile cha uchumi wa kati ambaao sasa tunakwenda kuinua watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wowote ukitaka upande, eneo lolote, katika nchi zozote; na katika nchi zilizoendelea waliangalia swala la miundo mbinu. Miundo mbinu ikishakuwa salama na mizuri maeneo yoyote yale inasaidia uchumi wetu kupanda. Kwa mfano ukienda moja kwa moja katika maeneo ambako uchumi umekwenda juu ni kwa sababu ya miundo mbinu. Tunapogawa rasilimali kuititia mpango huu, tuna hakika tunatakiwa kuangalia. Nimshukuru sana Hayati John Pombe Joseph Magufuli, ameangalia sana miundo mbinu na katika maeneo haya ameunganisha mikoa mingi sana kwa barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maeneo yale mambo yameenda vizuri sana. Sasa na kwasababu unajua Mheshimiwa Mwigulu kuna barabara yetu ambayo ingesaidia kuinua uchumi wa Tanzania. Barabara ya Karatu, Mbulu, Hydom, Singida, Sibiti kule mpaka Simiyu na Meatu wamekaa huko. Barabara hiyo ni barabara ya kimaendeleo. Najua *resources* au rasilimali zetu si kubwa sana, lakini barabara hii ikifunguliwa na mpango huu ukajielekeza hapo, ni wazi kwamba utakuwa umeinua sehemu hii ya uchumi wa nchi yetu kama Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikuombe sana mpango huu unaonekana namna hii, na jimboni kwako kumbuka ni kule. Kuna mtu mmoja alisema hapa hutarudi, mimi nikuombee 2025 urudi, lakini kwa masharti haya. Mpango huu uelekeze moja kwa moja kwenye barabara hii ninayoisema ambayo inapita jimboni mwako. Na bahati nzuri Mungu alivyokubariki...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatey Masey, kwani anakuja kugombea...

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina...

NAIBU SPIKA:... Maana umesema barabara hii ikitengenezwa ndio atarudi atakuja kugombea kwako kwa hiyo wewe hutarudi?

MHE. FLATE G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara hii inapita jimboni kwangu, halafu inakwenda jimboni kwake. Kwa maana hiyo basi barabara hii asipoiangalia isipopita wananchi watajua Flatey Massey Mbunge wa Mbulu Mjini kaisema barabara hii na Mwigulu Lameck Nchemba yeye ni Waziri katika Wizara hii na katika mpango uliopita barabara ilikuwepo haijatengewa fedha, sasa hivi amekuwa Waziri wa Fedha ataiwekea fedha; na kwa bahati nzuri wamewekwa pamoja. Waziri naibu wake anaitwa Masauni hawa wote ni vijana mwingine yuko yanga mwingine yuko simba unaona hiyo! Mwingine yuko bara mwingine yuko visiwani unaona hiyo! Hawa wote ni vijana. Sasa itakuwa hatari kama mpango huu hautakuja kwenye bajeti ikiwa na fedha katika barabara hii ambayo nimetaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo inapita kwenye majimbo tisa. Jimbo la Karatu, Mbulu Mjini, Mbulu Vijiji, Iramba kwake mwenyewe, inaenda Meatu, inakuja Sibiti inakutana mpaka Lalago kule, mpaka Maswa, Bariadi wanansikia kwa hapa. Kwa hiyo nimesema hii tu ili tukitoka hapa tuwe na *knowledge*; baadaye pasije pakawa na kwamba aah! Unajua katika mipango hii inayopangwa hapa, *resources* nyingine imeenda upande fulani na upande mwingine umesahaulika. Sina maana ya kujitenga katika nchi hii, napanga tu na kusema ili ninapokuja katika bajeti aje na hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na akishakuja na hiyo ni wazi kabisa mipango hii itakuwa inakwenda vizuri, kwasababu hamna uchumi wowote mahali popote unaweza kuendelea kama huna miundombinu. Mazao kutoka shambani kwenda viwandani unapelekaje? Ni lazima tuwe na miundombinu ya kutosha. Na kwasababu hiyo ukiangalia maeneo yote yale hakuna barabara ya kutosha. Hakuna barabara ambayo unaweza kusema utapeleka mazao kwenye viwanda, na ukiangalia viwanda vyetu viko mijini na kwa maana hiyo basi niombe sana sana sana sana Mheshimiwa Lameck Mwigulu Nchemba na ndugu yangu Masauni, sisi wote ni vijana na vijana wengi tumeingia humu; tuwasaidie vijana wetu kwa

kupeleka mazao yao kwenye viwanda kwa kuwawekea barabara hizi ambazo nimezisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naona kabisa muda umeondoka lakini niombe kama nchi ni vizuri kujivekeea sheria ili sheria hizi zitusaidie. Nimshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusema kabisa tunakwenda kupigilia maendeleo katika miradi mikakati iliyowekwa. Mungu ambariki sana na ninaendelea kumuombea ili tuendelee vizuri katika mipango ambayo imewekwa wote wawili wakiomba kura katika ilani ya CCM kwasababu barabara iko kwenye ilani ya CCM...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa...

MHE. FLATEI G. MASSAY: ...na nafikiri itakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii Mungu akubariki sana, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa uchangiaji kwa kipindi chetu cha kwanza. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 kamili leo.

(Saa 7.06 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Aloyce Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ighondo, Mheshimiwa Issa Mtemvu ajiandae.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kuchangia yapo mengi katika hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri lakini nitachangia zaidi tutakapoingia kwenye maeneo ya kisekta, leo nitachangia katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisje nikachelewa, nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo nitazungumzia sana maslahi ya watumishi. Nchi hii ina watumishi katika maeneo mbalimbali; wapo wakulima, walimu, madaktari na kadhalika. Hawa wanastahili zao; wanastahili kupandishwa madaraja kwa wakati, wanastahili kwenda likizo, wanastahili kwenda masomoni lakini wapo wengine ambaao wanastahili kupata malipo kutohana na kazi wanazofanya kwa muda wa ziada. Kwa bahati mbaya stahili hizi hazipatikani kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukasema kwamba bajeti yetu ipo salama bila kuzingatia hilo. Tunapokwenda kukamilisha Mpango huu, wapo watumishi ambaao wanانون'unka, wapo ambaao hawapandishwi madaraja lakini wapo ambaao hawalipwi, niombe sana zitengwe fedha maalum kwa ajili ya wale ambaao wanastahili kupandishwa madaraja hii ikiwa ni sambamba na kuwapandisha madaraja kwa wakati na walipwe stahili zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nitazungumzia ni miundombinu. Ipo miundombinu ya barabara, reli na kadhalika. Katika hilli nitazungumzia miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Mkoo wa Kigoma, lakini katika taarifa iliyotolewa ndiyo mkoo pekee ukiunganishwa na Mkoo wa Katavi haujaunganishwa katika mpango wa barabara kwa maana kwamba kufika kila mkoo. Niombe sana katika bajeti inayokwenda kukamilishwa sasa, mkoo wetu uweze kuunganishwa kwa barabara ambazo zinatosholeza kuweza kufikia kwenye ngazi ya mkoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara mfano inayotoka Mpanda – Mishamo - Uvinza – Kigoma; Tabora – Kaliua - Uvinza – Kigoma; na Mpanda – Inyonga – Koga - Ipole - Tabora. Niombe sana, barabara hizi zikamilishwe ili wananchi wa maeneo hayo kwa Mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma nao waweze kufurahia uhuru wa nchi yao kwa kupata barabara na kuweza kusafiri bila shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Kigoma ipo barabara ambayo inatoka Kabingo – Kakonko – Kibondo - - Kasulu - Manyovu – Buhigwe anakotoka Makamu wa Rais. Barabara hii imetengewa fedha sasa huu ni mwaka wa tatu, hawa ambao wanasema ni wajenzi wa barabara kasi yao ni ndogo. Niombe Wizara husika ifanye ufuatiliaji wa jumla ili barabara hii iweze kukamilishwa na wananchi waweze kupata huduma muhimu hasa hiyo ambayo nimeitaja ambayo ni barabara. Niombe sana barabara hiyo ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika Wilaya ya Kakonko, tunayo barabara ya Kakonko – Ruhuru - Nyakiyobe - Gwarama - Mpaka wa Mhange. Mpaka huu kuna soko ambalo linaunganisha Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Kakonko na nchi jirani ya Burundi. Pale limejengwa soko kubwa, soko la Kimataifa lakini halina barabara. Niombe barabara hiyo ijengwe kwa maana ya kutuunganisha na wenzetu wa Burundi ili biashara ambayo inastahili kufanyika katika eneo lile ambalo tayari kuna soko iweze kufanyika na iweze kukamilika kwa wakati na kuweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakwenda sambamba na barabara ya kutokea Gwarama - Nabibuye inakwenda kuunga kwa jirani yangu Mheshimiwa Ndaisaba Wilaya ya Ngara.

Niombe sana barabara hii nayo iweze kukamilishwa. Barabara hizi zikikamiliwa wananchi wetu watakuwa na uwezo wa kusafirisha bidhaa kutoka vijijini kwenda mjini na kwenda kule ambako soko linapatikana. Hii ni pamoja na barabara ya kutoka Kibondo kwenda mpaka Mabamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo, wananchi wetu wengi ni wakulima, hili halina ubishi. Shida inayojitokeza katika eneo hilo ni upatikanaji wa pembejeo, mbolea na matrekta tena kwa wakati. Niombe, kwa kuzingatia kwamba kilimo ni uti wa mgongo, wananchi wetu wengi wanategemea kilimo, pembejeo kwa maana ya mbolea, zipelekwe kwa wananchi wetu mapema ili ziwasaidie katika kuandaa kilimo na kulima vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mazao ya kimkakati, mwenzangu kaka yangu Mheshimiwa Vuma asubuhi alizungumzia masuala ya kilimo cha chikichi kwa upande wa Mkoa wa Kigoma. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ametumia muda mwangi sana kuja Kigoma kuhamasisha zao la chikichi. Ametumia muda mwangi na amejaribu kwa nguvu zake zote kuhamasisha jamii ile na wananchi wameamka. Niombe sana katika bajeti hii, nguvu kubwa ipelekekwe katika zao hili na hasa ikizingatiwa kwamba zao hili litaleta jibu sahihi katika tatizo ambalo linalotukabili la upatikanaji wa mafuta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba ipo mikoa mbalimbali ambayo inaweza ikalima zao hili. Mkoa wa Kigoma ukiwa mkoa wa kwanza, lakini zao hili linaweza likalimwa vizuri sana katika Mkoa wa Rukwa, Katavi na Tabora. Niwaombe sana Mawaziri hasa Waziri wa Kilimo, tafiti zifanyike, ufuatiliaji ufanyike, pembejeo zipelekwe, wataalam wapelekwe ili kuhakikisha kwamba zao hili linalimwa kwa wingi katika mikoa yetu na ikiwa katika mazingira hayo nina uhakika itatusaidia kumaliza tatizo linalotukabili la upatikanaji wa mafuta katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la chikichi kama ambavyo nimesema, ndilo jibu la tatizo la mafuta katika nchi yetu. Maeneo mengi katika nchi hii, chikichi inaweza ikalimwa. Ipo Wilaya ya Kyela katika Mkoa wa Mbeya zao hili linaweza likakubali, lakini maeneo mengine hata katika Mkoa wa Kagera, niombe tafiti zifanyike kwa ku-support Mkoa wa Kigoma kilimo hiki cha zao la chikichi kifanyike kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba kinajibu na kinatuletea matunda

katika kuhakikisha kwamba shida kubwa ya mafuta inayotukabili inakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nahitaji kuchngia ni upande wa madini. Yapo maeneo mbalimbali ambayo yamebainishwa kwamba yana madini ikiwemo Mkoa wa Kigoma, maeneo ya Mkoa wa Njombe kama ambavyo umezungumza maeneo ya Mchuchuma. Hata hivyo, yale maeneo mengine ambayo yamebainishwa bado hakuna tafiti za kutosheleza ambazo zimefanywa. Niombe maeneo yale ambayo yamebainishwa kwamba yana dhahabu, almasi na kadhalika tafiti zifanyike kwa kupeleka wataalam wa kutosha na mwisho kabisa uchimbaji uweze kufanyika kwa ajili ya manufaa ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ighondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ajiandae.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nami nianze kwanza kwa kuwapongeza Mawaziri na Naibu Waziri wote waliochaguliwa ama walioteuliwa katika awamu hii ya Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo mawili matatu, lakini naomba nianze na hili la viwanda na hapa naomba Waziri wetu wa Fedha anisikilize kwa makini kwa sababu kwanza yeye ni kijana mwenzangu lakini ni mtu ambaye amekabidhiwa jukumu la kwenda kukomboa uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye eneo la viwanda ndugu zangu wabobezi katika mausala ya uchumi watanisiaidia lakini katika pitapita zangu, uchumi wa viwanda, nchi iliyoendelea kiviwanda inatakiwa iwe na sifa

kuu chache. Kwanza, tunatakiwa tu-export manufactured goods. Pili, tunatakiwa tu-import raw materials, tu-import malighafi kutoka nje kuja kulisha viwanda vyetu huku nchini lakini tuingize teknolojia. tukirudi kwenye uhalisia wa uchumi wetu Tanzania hii kitu inaenda kinyume, yaani kichwa chini miguu juu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira haya, kweli tunaweza kufikia ule uchumi tunaosema wa viwanda? Juzi tu hapa, tena sio juzi na hilo tatizo liko hivi sasa, mahindi ya Tanzania yamezuiliwa pale mpakani Kenya. Mimi nilifikiri kama tungkuwa *smart* Watanzania tungefurahi suala lile, tunatakiwa sisi tupeleke kule nje unga siyo kupeleka malighafi. Tunatakiwa sisi tu-export manufactured goods, sisi tuzalishe, tu-process tuhakikishe tunalisha viwanda vyetu hapa nchini, kule tupeleke bidhaa zilizotengenezwa tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Ziwa wanalamika hapa kila siku, pamba, pamba, ngozi kwa nini tunatoa malighafi hivi kwenda kuwakuzia wenzetu uchumi wakati sisi wenyewe tunahitaji bidhaa hizi kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani? Ninatarajia katika Mpango huu tunazungumza hivi sasa, Mawziri wetu, Waziri wa Viwanda, Waziri wa Fedha, Waziri wa Biashara na Uwekezaji mtutoa hapa tulipo twende hatua inayofuata kwa kuhakikisha bidhaa na mazao tunayozalisha humu ndani, tunaya-process wenyewe, tunapeleka nje bidhaa zilizokwishatengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasikia tuna viwanda vya viatu vya ngozi hapa nchini, lakini nashangaa tunafurahia kweli kuvali viatu vya China. Hatuwatendei haki wakulima wetu na wazalishaji wetu wa ndani kuhakikisha kile tunachowahubiria kila siku zalisheni, kweli wanazalisha lakini kwenye eneo la *finishing* tunashindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtaalam mbobezi wa uchumi, leo tunasema upele umepata mkunaji, basi kamalize kazi ndugu yangu tunategemea matokeo makubwa sasa.

Tuwasaki die vijana wetu basi na wao wapate ajira kupitia sekta zetu za viwanda. Serikali haiwezi kuajiri ikawamaliza Watanzania wote, sasa hivi vijana wako mtaani wanashubiri ajira, utawaajiri wapi? Lazima tuanzishe viwanda vya kimkakati, lazima tuhakikishe *raw materials* zilizopo nchini zinafaidisha Watanzania hasa kwenda kwenye viwanda vya kwetu humu ndani sisi wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kwenye eneo la kilimo mashaka bado ni makubwa. Nizungumzie tu maeneo machache ambayo nina uzoefu nayo katika Jimbo langu la Singida Kaskazini. Sisi ndiyo wazazishaji wakubwa sana wa alizeti, haya mafuta mnayokula hapa yametoka Singida Kaskazini mimi ndiyo nazalisha kule pamoja ndugu zangu. Gunia la alizeti iliyozalishwa limefungwa vizuri la kilo 100 ni Sh.40,000 mpaka Sh.50,000 lakini mbegu ni Sh.60,000 au Sh.70,000, tutamkomboa lini huyu mkulima? Tuleteeni pembejeo, mbegu na ziuzwe kwa bei *affordable* kwa kila Mtanzania. Hata hizi kelele tunazopiga kwenye viwanda watu watazalisha tupapeleka viwandani. Sasa hivi ndugu zangu kule Singida Kaskazini wameiacha alizeti kwa sababu bei ya mbegu ni kubwa, tu- *subsidized* mbegu, pembejeo ili wakulima waweze ku-*afford* kwa kiwango tunachofahamu cha hali za wananchi wetu kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la tatu ambalo linaendana sasa na haya masuala viwanda na kilimo ni lazima miundombinu iwe mizuri kwenye eneo la kuzalisha mpaka *processing* kama ni viwanda. Tulizungumza sana barabara zetu sasa hivi mvua zimenyesha zimeharibu kwelikweli barabara hazipitiki. Sidhani kama kuna Waziri hapa anayetokea Dar es Salaam maeneo ya Magogoni pale, wengi mnatoka vijijini kama ninakotoka mimi, mnafahamu hali halisi ya mazingira ya mwananchi wa Tanzania, tutengenezeeni miundombinu ya barabara za vijijini hata hizi zinazounganisha mkoa na mkoa na wilaya na wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo barabara moja kubwa pale inayotoka Singida Mjini kwenda Haydom, ile ndiyo roho ya uchumi wa Singida Kaskazini. Barabara hii ni

ahadi ya viongozi wa kitaifa kuanzia Rais Mstaafu Hayati Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Hayati Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Naomba basi, tusiwadhalilishe viongozi hawa, tekelezani hizi ahadi ndugu zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo barabara inatoka Singida Mjini - Kinyeto – Kinyagigi – Meriya – Maghojo - Sagara nayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyeo madarakani hivi sasa. Naomba barabara hii nayo itengenezwe kwa kiwango cha lami kwa sababu sisi kwa uzalishaji wetu wa alizeti ninaowaambia hapa ndiyo tunaowalisha kwa mafuta, hatuwezi kuwaleta sokoni kama barabara ni mbovu. Ndiyo tunaozalisha vitunguu kwelikweli lakini hatuwezi kuvikisha sokoni kama barabara ni mbovu. Naomba kwa kupitia Mpango wetu huu wa Maendeleo tuione miundombinu ni kipaumbele na tuhakikishe tunawasaidia wakulima wetu katika eneo lao la uzalishaji.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kwenye utawala bora kidogo...

NAIBU SPIKA: Hiyo ni kengele ya pili Mheshimiwa Ramadhani.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima yako naomba nusu dakika, inanitosha, naomba kuzungumzia suala la maslahi ya Madiwani.

NAIBU SPIKA: Sasa jambo jipya tena hilo Mheshimiwa.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wakati unachangia nikawa naijuliza hiyo suti kama ameshona kijana wa Kitanzania au umeagiza mahali halafu unapiga maneno

mengi hapa. Wanawake nadhani ndiyo tunaongoza kuwa-*support* vijana, wamama na washonaji wengi, wababa wachache sana. Mjithidi jamani mshone hapa hapa, sisi si mnatuona vitenge vyetu, mambo kama haya. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea na Mheshimiwa Issa Mtemvu, tunao wageni ambaao tuko nao humu Bungeni. Kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambaao ni viongozi wa Maafisa Elimu, Kata ya Moshi Mjini, Mkoani Kilimanjaro ambaao ni Ndugu Godfrey Shirima ambaye ni Mwenyekiti na Ndugu Eva Swai ambaye ni Katibu. Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni mmoja wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambaye ni mtoto wake, anaitwa Simba William Jerry Silaa. Asimame tumuone, karibu sana, naona amesimama kijeshi sijui kama ndiyo ameambiwa hiyo ndiyo salaam ya heshima. Karibu sana, lakini naona Mheshimiwa Jerry anafukuzia jamani kama kuna wale watoa tuzo za baba bora nadhani ndiyo maana amekaa na mtoto wake kule juu, naona anatafuta tuzo ya baba bora. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji wetu Mheshimiwa Issa Mtemvu anaafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa maana ya mwaka 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri mapema kwamba mimi ni mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Bajeti, kwa hiyo, nimechangia mara nyingi katika maeneo mengi. Kwa sasa nitumie nafasi hii kuchangia eneo moja tu ambalo pia nilitumia nafasi kama hii kuchangia Mpango kwa mara kwanza mwezi Februari katika eneo la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuwasilishia Mpango mzuri. Pia, nimpongeze Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa jinsi ambavyo waliweza kutuongoza na kufikia mapendekezo hayo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu una maeneo matano ya vipaumbele, lakini binafsi nitajielekeza katika eneo moja la kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Hapa yako mambo mengi ya elimu, afya na kadhalika lakini mimi nimebeba hili la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema sana juu ya eneo la ardhi na hasa upimaji, Mpango wetu ulieleza wazi nia yake ya kupima ardhi nchi nzima. Nia hii wala si mpya sana kwenye Mpango wa Tatu, ilikuwepo pia kwenye Mpango wa Pili. Nikikumbuka sana katika Mpango wa Pili tumeendelea sana kupima ardhi na hapa niipongeze sana Wizara ya kisekta kwa kufanya kazi nzuri sana kitakwimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufahamu vizuri maana halisi ya kupima ardhi ni lazima tujue faida zake. Nitataja chache sana kwa sababu ya muda, tukipima ardhi maana yake tutatambua kisheria umiliki halali wa kipande kilichopimwa, kuongeza thamani ya ardhi, kuongeza usalama wa ardhi, kutumika kama dhamana na zaidi kuondoa migogoro kwa majirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, hizo zikiwa ni sifa chache sana lakini malengo ya upimaji katika kipindi kilichopita cha Mpango wa Pili tumepima vizuri sana. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 – 2019/2020 tumetoka katika upimaji wa karibu viwanja 74,000 mpaka kufikia viwanja 150,000 ni ongezeko zaidi ya nusu yaani mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mpango mzuri ambao upo sana ndiyo maana nina wasifia sana, katika kipindi hiki

cha Mpango wa Tatu naona sasa wanaelekea kwenye kupima ardhi katika kiwango cha 300,000 mpaka 500,000 kwa mwaka, hili ni jambo kubwa sana. Zaidi nijielekeze na nilsema Februari nchi hii ni kubwa, ina eneo la ardhi kubwa sana lakini toka Uhuru tumeshapima asilimia 25 tu na najua malengo kwa miaka mitano ijayo itakuwa labda kwa ziada ya asilimia 100 maana yake ni mara mbili kufikia asilimia 45. Ni ukweli tukijielekeza sana ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam ambaao una watu zaidi ya milioni sita katika makadirio kati ya milioni 61 kwa nchi nzima, unaweza ukaona tuna idadi kubwa na tukiwekeza pale tunaweza tukapata tija sana ya kuinua watu wetu kiuchumi. Tukiinua watu hawa kiuchumi maana yake itaenda sambamba kwa maana ya *multiplier effect* katika maeneo mengine ambayo yatatusaidia sana kuijinua kiuchumi lakini vilevile kuongeza Pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuseme ukweli, nimepongeza kwa kiasi lakini ipo kazi bado haijafanyika na mimi muda mwingu naipima kazi ya sekta hii katika Mkoa wa Dar es Salaam *vis a vis* mikoa mingine na nipongeze sana. *Trend* ya mwaka 2015/2016 – 2019/2020 na hasa miaka miwili ya mwisho utaona Mkoa wa Dodoma *vis a vis* Mkoa wa Dar es Salaam, nilijaribu kuitapita kitakwimu nikakutana na Kitabu kimoja cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri cha mwisho kwa sekta hii 2021, karibu kama ukurasa 170 unaweza ukaona viwanja vilivyopimwa 2018/2019 Dar es Salaam ni 25,490 lakini mwaka huo huo Dodoma imepima 71,571. Kwa mwaka uliofuatia 2019/2020 mpaka Aprili, Dar es Salaam tumeppima viwanja 11,125, Dodoma 76,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo ninaposhangaa. Ninashangaa kwa kuona kwamba bado hatujaamua kupima ardhi, tungeamua kupima ardhi hii haiwezekani eneo lenye watu milioni sita tunapima ardhi viwanja 14,000. Watu wenye watu takriban milioni mbili wanapima viwanja 70,000 mpaka 75,000. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni ukweli pia katika mwaka 2017/2018, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana

aliwahi kutoa kauli moja nzuri sana juu ya kurasimisha ardhi nchi nzima. Jambo hili liliikuwa ni zuri sana kwa maana katika malengo yale niliyoyasema kama faida ya kupima ardhi utaona huko kuinua wananchi kiuchumi. Alitamani kuona maeneo ambayo yameendelezwa kiholela sasa basi watu waweze kupimiwa bila kubomolewa na baadaye hati zile ziwasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfano wa kawaida sana, Mkoa wa Dar es Salaam kwenye lile jambo la urasimishaji ambayo nkinukuu kauli ya Mheshimiwa Waziri alioitoa tarehe 23 Oktoba, 2017 alisema: "*Hatutobomoa nyumba ya mtu bali tutaendelea na urasimishaji wa makazi kwa maeneo yaliyojengwa holela ili yawe makazi rasmi na wananchi wapelekewe huduma muhimu kama vile barabara, umeme na maji. Muhimu wapewe hati miliki ili ziwasaidie kiuchumi na waweze kulipa kodi ya ardhi, lakini nitazuia ujenzi mpya holela katika miji yetu kwa mujibu wa sheria. Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, tarehe 23 Oktoba, 2017*".

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme jambo hapa kwa kumalizia dakika zilizobakia. Kitakwimu, urasimishaji huu umekuwa donda kubwa Dar es Salaam kama *sample* ya nchi nzima. Dar es Salaam katika Wilaya ya Ubungo nikienda Jimbo la Kibamba kwenye Kata sita nabeba kata mbili tu, maana huko kwagine ni nyingi sana, katika kata mbili tu katika nia njema ya kupima ardhi hii ili itusaidie sana kwenda kwenye Mpango wa Tatu, katika makampuni yaliyosajiliwa, kwenye usajili, uthamini, wana mambo kama matatu hivi lakini viwanja vilivytambuliwa na kupimwa kat i ya viwanja 10,000 ndani ya kata moja ya Kibamba ni viwanja 3,000 tu ndiyo vimewekewa mawe, hati ni 20 katika kipindi cha miaka miwili na zaidi. Kata ya Mbezi, katika viwanja vilivyopimwa 33,000 hakuna hati hata moja katika kipindi cha miaka miwili na nusu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, fedha ni zipi zimechangwa? Kwenye ile Kata ya Kibamba peke yake shilingi milioni 890 wakati Kata ya Mbezi ni shilingi bilioni 2.57,

ukizijumlisha ni zaidi ya shilingi bilioni 3 zimechangwa na Watanzania maskini lakini mpaka sana hawajawahi kuona hati ndani ya kipindi cha miaka miwili, haya ni magumu hata kuyatamka. Leo tunasimama tunazungumzia Mpango uje utusaidie kwenda mbele katika kipindi cha miaka mitato 2021-2026. Kwa kweli lazima tuoneshe tuna nia njema kusema haya tunayoyasema ili tuyatende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili halijawahi kwenda sawa, tunatambua wakati tunapeleka urasimishaji upande mmoja watu wanaambiwa wachange fedha zao ili twende sawa wapate hati, kuna upande mwininge zaidi ya halmashauri 27 zimepewa zaidi ya shilingi bilioni 6 hadi 10. Tumeona Kamati ilikuwa Iringa juzi tu na ikakuta zaidi ya shilingi milioni 400 waliyopewa ile halmashauri wameshindwa hata kurejesha, ni *revolving* lakini wameshindwa kurudisha lakini hawa wallotoa hela zao zinaenda kupotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana jukumu la Wizara kwenye hili ni kutoa hati siyo makampuni...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudi kuongelea sekta hii vizuri sana. Nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimiwa Hassan Mtenga ajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupewa fursa hii ya kuchangia Mpango huu. Nitajikita kwenye maeneo mawili; nitaongelea kilimo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mpango, umeongelea kwa kina suala zima la kilimo. Kama Wabunge wengi walivyochangia, kilimo ndiyo sekta pekee ambayo inaakisi uchumi jumuishi; inaaajiri Watanzania zaidi ya asilimia 65. Kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyosema, kilimo hatujakipatia msukumo ambao kinastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea zao moja. Kama Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma wanavyosema, kwa Mkoa wa Kagera zao la kahawa ni siasa, zao la kahawa ni elimu, zao la kahawa ni kila kitu. Miaka ya 1970 Mkoa wa Kagera ulibahatika kuwa na wasomi wengi kwa sababu ya zao hili la kahawa. Leo tunapoongea, Kagera zao la kahawa limekuwa kama laana. Bei imeshuka na wanapouza hata bei kama ni ndogo, bado kupata hela zao inawachukua zaidi ya miezi mitatu kama dada yangu Mheshimiwa Conchesta alivyosema pale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la kahawa kwa Mkoa wa Kagera linahusisha kaya nyingi kama ilivyo kwa Taifa zima. Nilikuwa naangalia takwimu hapa. Zaidi ya 90 percent ya kahawa inazalishwa na wakulima wadogo wadogo. Hawa wakulima wadogo wadogo ndio wazazi wetu, kaka zetu, wadogo zetu, ambao wanahangaika usiku na mchana kuhakikisha kwamba wanapata pesa ya kusomesha watoto wao, kutunza familia zao na kuhakikisha kwamba wazazi wao wanaendelea kuishi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo liko wapi? Naishukuru Serikali, kwa miaka mitano iliyopita walifuta tozo karibia 20 kwa zao la kahawa, tunawashukuru kwa hilo, lakini walipofuta hizi tozo, hatujatafuta suluhisho la bei na mauzo ya zao la kahawa, tumeviachia vyama vyama msingi vinunue kahawa kutoka kwa wakulima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sekta binafsi, tunaihusishaje kuhakikisha kwamba na wao wanunuua kahawa kwa Mkoa wa Kagera ili kuleta ushindani? Tumeviachia vyama vyama msingi peke yao, vinafanya kazi vinavyotaka vyenyewe, vinalipa wakati vinapotaka

vyenyewe. Hata hivyo, kuna wazawa wa Tanzania ambao wamewekeza kwenye viwanda vya kusindika kahawa, tunawaambia hao kama unataka kununua kahawa, kanunue kwenye vyama vya msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atuambie, tunaoanishaje kilimo na Sekta ya Viwanda? Unapowaambia wanunue kwa vyama vya msingi, watanunua kwa bei ya juu kuliko wangekwenda moja kwa moja kununua kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna maneno hapa yanasemwa, eti watakwenda kuwalangua wakulima. Ndiyo! Wakalangue kule, lakini Serikali ihakikisha kwamba inaweka mazingira sahihi na mazingira huru kuhakikisha kwamba vyama vya msingi vinanunua na wafanyabiashara wanununua bila kuwaathiri wakulima wadogo wadogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mpango namshukuru Waziri, amesema tunakwenda kujenga uchumi shirkishi na uchumi shindani. Tunayo Sheria ya Ushindani hapa nchini, tuweke mazingira huko kwenye vijiji vyetu kuhakikisha kwamba hata huyu; vyama vya msingi na vyama vya ushirika vishindanishwe na wakulima na wanunuzi binafsi ili kuleta uwiano na ushindani kwenye masoko yetu. Tusimlinde huyu. Mnajua madhara ya uchumi hodhi? Mnajua matatizo ya *protectionism*? Tumevilinda kwa muda mrefu vyama vya ushirika na vyama vya msingi na tunajua matatizo yake kwa wakulima wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaporuhusu ushindani, tunakaribisha ubunifu, tunakaribisha teknolojia na tunakaribisha wakulima wapate *a fair deal* kwa mazao yao wanayoyalima huko kwenye majimbo yetu. Nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kuhakikisha kwamba baadhi ya sheria na Mashirika ambayo hayatuongezei ufanisi kwenye maeneo yetu tunakotoka, aidha, sheria zao wazilete hapa tuzipitie upya kuona kama zinatuongezea ufanisi au tufute. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nilikuwa nasoma kitabu kimoja wachumi wanakifahamu vizuri sana, " *Why Nations Fail? The Origins of Power, Prosperity and Poverty.*" Mwandishi anatuambia na kutushauri, kama tuna mashirika ambayo hayana ufanisi, tunakaribisha umasikini kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nishauri kwenye hili, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi tuhakikishe suala la zao la kahawa Mkoa wa Kagera lipatitive ufumbuzi wa haraka, watu wapate bei nzuri na sekta binafsi ihusishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, tatizo tulilonalo kwenye hili zao lenyewe la kahawa kutoroshwa kuuzwa nchi za nje litakwisha. Pia, tutakuwa tumeboresha Sekta ya Viwanda; kwenye jimbo langu tunavyo viwanda viwili vinasindika mazao ya kahawa, lakini wanalazimika kununua tu kwenye vyama vyaya msingi kwa bei ya juu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni uvuvi. Tunalo Ziwa Victoria ambalo linazalisha, lakini ukiangalia takwimu za uvuvi na faida tunayoipata kutoka katika ziwa hili ni aibu. Sisi kama Tanzania, niliwahi kulisema hapa mwezi wa Pili. Tunamiliki eneo kubwa zaidi ya kilomita za mraba 35,000 ambazo ni sawa sawa na asilimia 51 na wenzetu asilimia 43; lakini ukiangalia tunachokipata na tunachokiuza nje, hakuna uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa nilikuwa nasoma ripoti moja, tumeambiwa sisi tunauza nje kwa asilimia 51 ukilinganisha na majirani. Kwa uchumi wetu tunachangia *only two percent* ya GDP, Uganda 3%, Kenya 2% na wenye. Ukiangalia viwanda ambavyo vimejengwa, Uganda wanaongoza, wana viwanda zaidi ya 20; sisi ambao tuna asilimia 51 tuna viwanda vinane tu na Kenya wana viwanda vitano. Tunaambiwa viwanda vinazidi kuperomoka kwa upande wetu na vinazidi kuongezeka Kenya na Uganda wenye eneo dogo tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunafanya hayo na sisi tuko hapa? Kazi kubwa tunayopaswa kuifanya kama

tunataka kuchochaea uchumi, ni kuhakikisha tunavuna hizi fursa ili wananchi wetu waweze kuchangamkia uchumi wetu. Hata mazao tunayoyapata kutokana na uvuvi ili yasafishwe kupelekwa kwenye masoko ya nje, yanapitishwa Uganda na Kenya; *Entebbe na Jomo Kenyatta International Airport.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma tulifanya maamuzi mabaya, tuliweka *a five percent surcharge* kwa *total consignment* ya minofu ya samaki kutoka Mwanza. Ilifikia mashirika yote ya ndege yakakimbia. Mpaka leo ili tusafishe minofu ya Samaki, lazima twende *Entebbe au Jomo Kenyatta International Airport*. Kwa nini, Mheshimiwa Naibu Waziri? Ukiangalia chanzo chake ni tozo tulizojiwekea sisi wenyewe na tulizipitisha hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea tu, mabondo; ili usafishe mabondo tuna tozo ya shilingi 7,500/= kwa upande wa Tanzania; Uganda ni shilingi 436/= na Kenya ni shilingi 34/=. Ukipitia tozo zote kwa upande wa samaki na mazao ya uvuvi, sisi tuna tozo ambazo hazibebeki na hazihimili na matokeo yake tunapoteza uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitachangia zaidi kwenye sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Mtenga na Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi nitaongelea jambo moja tu kuhusiana na urasimu katika utekelezaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba nitoe mfano mmoja ambao uliwahi kutokea hapa kwetu, inaweza kuwa

siyo hadithi nzuri sana, lakini itatusaidia kukumbuka. Kuna wakati fulani ilitokea hadithi ya mafuta ya upako; yalimwagwa kwenye *carpet* na watu wakapita wakiwa na malengo ya kupona pale, huzuni zitabaki pale, wakiwa na malengo kwamba kama wallingia na mawazo, yataisha pale na kwamba wataondoka hawana *stress*. Sasa basi, Mpango huu naufananisha kama mafuta ya upako, kumbe ndani ya yale mafuta ya upako kulikuwa kuna utelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya watu kutoka wamepona pale, wakawa wanakatana mitama mle, wanalaliana, wanakanyagana, wengine wakatoka wamekufa, tukapata majeruhi na wengine ambao walikuwa mahututi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango ni mzuri na mambo yamekaa vizuri. Wasiwasi mkubwa ni urasimu ambao hauna maana katika utekelezaji wa Mpango. Lazima tukubaliane sasa kama tunakwenda kama nchi, tushirikiane mihimili yetu yote mitatu, Wizara zetu zote, pamoja na Idara zetu zote, tushirikiane na vyombo. Kwa sababu kuna wakati fulani tunaweka mipango mizuri lakini unaweza kukuta kuna mahali tunaweka vitu ambavyo vinasababisha tusiende mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumeongea kwenye Mpango kwamba tuna miradi ya kimkakati. Miradi hii mingine imeanza siku nyingi, bado inahitaji garama ndogo sana. Sasa kwa sababu ya urasimu usiokuwa na maana, utakuta kuna vikwazo vinatokea tu ama kutoka katika Idara moja ama kutoka katika Idara nyingine au kutoka katika Wizara fulani au kutoka katika chombo fulani tunakuwa hatuendi mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna miradi kwa mfano ya utalii, tayari tuna *capital* kule kwa sababu tayari tuna Wanyama, tuna Mbuga za Wanyama, tuna kila kitu. Kuna miundombinu tu kuielekeza kufika kule kwenye utalii ili sisi tuanze kukamua dola, kunaanza kutokea urasimu usiokuwa na maana. Halafu wakati mwингine *ku-connect* sasa; tumeboresha viwanja vyatundege, tumenunua ndege,

zinafika kwenye viwanja vya ndege. Kutoka pale kwenye kiwanja cha ndege kufika kwenye Mbuga ya Wanyama hapaingilili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu ndiyo tunasema utelezi kwenye upako. Utelezi ndani ya Mpango, kwa nini sasa? Hii miradi ya kimkakati kama ya utalii ambayo inaweza ikatengenezewa tu miundombinu na tukaanza kupata fedha, isitolewe hiyo fedha tukafanya mambo haya na tukatekeleza ili tuanze kukamua hela huku wakati huo huo tukiboresha huduma zetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna Wizara ya Viwanda na Biashara, tuna Wizara ya Vijana na Ajira, wanafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba wanatengeneza ajira kwa vijana wetu. Tuna Wizara zinafanya juhudil kubwa au Idara zinafanya juhudil kubwa kuua vyanzo hivyo vya ajira. Ndiyo maana hapa unakuta Waheshimiwa Wabunge tunakuja kulalamika, ni kwa nini bodaboda ziae kwenye Vituo vya Polisi na vijana wetu wakati wamejiajiri na tumeruhusu kama sehemu ya ajira? Huo ndiyo unakuwa utelezi sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumekubaliana kwamba tunavutia wawekezaji kwenye Taifa hili. Tuna Wizara ya Uwekezaji kwenye nchi yetu, tulikuwa na *TIC* wakati ule inavutia wawekezaji kwa kuweka mazingira mazuri. Kuna Idara nydingine wanapofika ndani ya hii nchi, wanazuiliwa vibali, wanaanza kuwekewa urasimu wa vibali kibao, sijui kodi, vitu kama hivyo. Huo ndiyo utelezi sasa kwenye Mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka uchumi shindanishi kikanda na Kimataifa. Leo hii tunataka Watanzania wakauze bidhaa kwenye Soko la Afrika Mashariki, Soko la *SADC* na Soko la *AGOA*. Rudi sasa kwenye utelezi; namna ya kupata *Passport*, namna ya kupata Hati tu ya Uraia, namna ya kupata cheti cha *TBS*, utelez! Kina Mama wanatengeneza *products* zao, kuwekewa tu alama ya *TBS*

kuna milolongo mirefu, akina mama wanashindwa kwenda mbele, tunashindwa kufanya biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwengine tunadanganyana humu. Unapofuatilia kibali kwa ajili ya wawekezaji au kuleta wawekezaji, utasikia kuna vyombo, kuna vyombo, kuna vyombo; sasa sijui ni bakuli, sijui ni *thermos*, sijui ni chupa! Vinazuia! Hapa vyombo vinafanya utafiti, uongo mtupu! Tunadanganyana, tunaweka utelezi kwenye Mpango. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna miradi mikubwa ya umeme hapa imeanzishwa, kama Julius Nyerere *Stiegler's Gorge*. Ule ni mradi ambao utatusaidia. Wapo Watanzania wanaubeza, zipo Idara nyngine ni utelezi. Wapo Watanzania wengine hawaoni umuhimu. Mradi ule utatuongezea nguvu ya umeme, utatupunguzia *production costs*, utasababisha bidhaa zetu kushuka bei. Hivyo utasababisha nasi tuweze *ku-compete* kwenye soko la *East Africa* na Kikanda. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ule ukiwekwa maji pale, umeshatengewa tena hekta zaidi ya 150,000 kwa ajili ya *irrigation scheme* unakwenda kwenye ile *irrigation*, utakutana na watu wa bonde. utelezi hutuzuua sasa tushindwe kufanya *irrigation schemes*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna vitu ambavyo nasema kama hatutashughulika na utelezi kwenye mafuta ya upako, tutaondoka tumekufa, tutaondoka majeruhi. Lazima Serikali yenye kazi iipange. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilikuwa nasoma taarifa ya CAG, anaongelea kuhusu kukusanya mapato na *TRA* jinsi ilivyokusanya, lakini moja ya mapendekezo ya CAG, aliwapa mapendekezo kama 338; ni asilimia 19 tu wameyafanya kazi, mapendekezo 266 wameshindwa kuyafanya kazi. Asilimia 38 ya mapendekezo 266 ni kwa sababu yako Idara nyngine, kwa hiyo, yameshindwa kutatuliwa, Idara nyngine imeleta utelezi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu kama hatutaangalia haya na kuangalia urasimu tuliuweka ambao unatukata mtama wenye kwenye upako, hatuwezi kufika mbali. Lazima sasa Serikali iamue kwa nia ya dhati kuondoa urasimu usiokuwa na maana. Kama tumeamua tunajenga ajira kwa vijana wetu, walindwe; machinga walindwe; bodaboda walindwe; na mama ntilie walindwe. Wale hawajaenda shule lakini tuna wasomi, Maafisa Biashara wetu, siyo kazi yao kuingia kuwasumbua wale, ni kwenda kuwaelimisha wafuate taratibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kazi ya Jeshi la Polisi tu kukamata bodaboda peke yake, ni kutoa na elimu. *TRA* leo ni chombo kinachokusanya mapato, siyo kazi yao kuwa *innovator* wa kesi kwenye nchi hii. Zipo kesi za biashara kwenye Mahakama ya Rufani 1,097 ambazo ziko *created* na *TRA*, wamehama kwenye lengo lao la msingi, wamehamia kwenye *ku-create* kesi. *TRA* wana kitengo cha kutoa elimu kwa wafanyabiashara, watoe elimu kwa wafanyabiashara na sio kuwavizia wafanyabiashara wamekosea ili wao wapate mazingira ya kuwashtaki. Kwa hiyo lazima tuondoe utelezi na urasimu usiokuwa na maana, twende tukatekeleze hii miradi ya kimkakati. Tujenge barabara kwenda kwenye *National Parks* zetu. Kwa mfano sisi tuna barabara ya kutoka Iringa - Ruaha *National Park*, ni *park* ambayo ni ya pili kwa ukubwa duniani. Ina tembo wakubwa kuliko *National Park* yoyote lakini miaka yote barabara iko kwenye Ilani lakini haitekelezeki mahali ambako tungekwenda kuchukua *dollar* bure. Unaona watu wanaingia Serengeti wanakwama kule ndani, wakati vitu tayari viko pale. Tuache, twende tukaamue sasa kufanya kazi kwa ajili ya ku-*implement* Mpango huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo tutakwenda vizuri. Tukiangalia hawa watu wa chini, ameongea Mheshimiwa Mbunge mmoja kama tukiangalia hii *micro enterprise* ya wafanyabiashara wadogo tukaielimisha, leo tunaongelea ujuzi, kutoa elimu ya ujasiriamali. Tuna mkakati gani wa kuwapa hiyo elimu? Tunawapa mafunzo ya ujasiriamali kwa mtindo gani? Au tumeweka tu

tunatengeneza mifuko ya wajasiriamali, sijui ya wafanyabiashara wadogo wadogo, hiyo mifuko inaishia juu. Kuna mmoja amesema hapa kuna Benki ya Kilimo ina majengo mazuri Dar es Salaam, Dar es Salaam kuna kilimo gani? Haya ndiyo mambo ya utelezi, yaani vitu ambavyo watu wanatengeneza dili ambazo hazieleweki! Twende kwenye *grassroot* tukatatue matatizo ya wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaongelea akinamama wajengewe vituo vya afya, zahanati na hospitali, huduma za uzazi ziwe bure, wewe unakaa unazuia fedha ya matibabu kwa akinamama wasitibiwe, una hila gani? Utelezi huu. Sisi tunataka kuongeza wapigakura kwenye nchi hii, tunataka kuongeza raia bora kwenye nchi hii, wazaliwe watoto bora kwenye nchi hii, unazuia fedha bila sababu, huo ni utelezi. Tunataka sasa urasimu na Wizara zijione kama kila Wizara ina heshima, maana ipo ile kuona kwamba labda Wizara hii kwa sababu sisi ni Fedha, basi ni wa muhimu sana, samahani kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, wewe ni rafiki yangu sana. Labda wewe ndiyo wa maana zaidi kuliko yule Waziri wa Wizara ya Kilimo au Waziri yejote, hapana! Kwa sababu ili Waziri wa Fedha awe na fedha, ni lazima kilimo kichangie mapato, ili awe na fedha, lazima mama ntilie wachangie. Leo hii tuna vitu vya ajabu, tunatakiwa kuangalia mambo ya utelezi, urasimu wa kijinga. Kwa nini tusifikirie Watanzania wetu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa...

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: ... wanaofanya vizuri tukawatumia sisi wanaanza kuonekana kutumika kwanzza Afrika Kusini.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja lakini utelezi uondolewe. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nadhani Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu, mama Samia Suluhu Hassan amesisitiza hilo. Serikali ni moja, safari hii haiyumkiniki kwamba kutakuwa na mtu anasema kibali kimekwama hapa, pale, wote zungumzeni lugha moja.

Mheshimiwa Hassan Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao ajiandae.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Fedha kwa kutuletea Mpango ambao umekaa vizuri sana. Nina mambo ambayo nitayachangia kwenye maeneo zaidi ya matatu hasa tukianza kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunahitaji tuvuke na tupambane kuondoka kwenye umaskini kuingia kwenye suala zima la kimaendeleo hasa kwenye uchumi mkubwa tunapozungumza miundombinu hasa kwenye maunganisho ya nchi yetu Kusini mwa Tanzania, kule Mtwara, naishukuru sana Serikali kwa kutujengea daraja la Mtambaswala. Nataka nitoe angalizo, daraja hili limetengenezwa kwa gharama kubwa sana, lakini kwenye utengenezaji wake na matumizi ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze uhalisia kutoka Mtwara kuelekea Masasi kuna kilometra zaidi ya 230, lakini kutoka Masasi kuelekea kwenye daraja la Mtambaswala kuna kilometra 130 lakini kutoka Mtambaswala kwenda *border* kuna kilometra 75. Ukitoka *border* kuelekea Beira Nampura pana kilometra zaidi ya 788. Hoja ni vipi? Ukitoka Mtwara kuelekea Ruvuma pana kilometra 70, kutoka Ruvuma Mpakani unaelekea Msimbwa Naplaya mpaka

Nampura unatumia kilometa 445. Kama tungejenga daraja hili kuititia pale Mto Ruvuma tungeweza kufungua mawasiliano kati ya Msumbiji na Tanzania na Afrika Kusini kuititia Msumbiji kuja Tanzania. Sasa hivi wenzetu Afrika Kusini wakitaka kwenda kuuza magari wanapitia Zambia ambapo wanatumia zaidi ya kilometa 2,800 kuja Tanzania. Kwa hiyo nataka niseme hapa hapahitaji watu wenye *degree* wala maprofesa, ni suala la uamuzi sasa kwa Waziri mwenye dhamana alishughulikie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nataka nimpongeze mdogo wangu Mheshimiwa Bashe. Mimi nasema Bashe ana akili kubwa sana. Pia nataka nishauri, kule kwetu Mtwara liko eneo moja linaitwa Kitele. Toka nazaliwa napata umri mpaka leo naingia uzeeni, liko eneo linamwaga maji chemchem, maji ya kutosha sana na eneo lile wakazi wa pale wanalima mpunga. Kwa kuwa mpunga ule unalimwa tofauti na viwango, hatuna *scheme* za umwagiliaji mpunga ule ni mzuri sana, lakini haukidhi mahitaji ya kibiashara. Sasa naiomba Wizara yenye dhamana, twende pale wakaangalie wajivekeze ili tuweze sasa kuleta kilimo cha kisasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango nimeangalia kwenye suala la elimu. Kwanza niipongeze Serikali, imeweza kuwekeza kwenye mfumo wa elimu bila malipo tukisema elimu bure, hongera sana kwa Serikali yetu. Hata hivyo, bado kuna tatizo, shule za msingi katika kila pato la kichwa cha mwanafunzi tunapeleka shilingi 6,000, lakini kwenye shule za sekondari kila kichwa cha mwanafunzi tunapeleka shilingi 10,000, lakini fedha hizo tayari Wizara zinapeleka kukiwa na mgawanyiko wa matumizi. Utawala wana asilimia 10 kwenye fedha hiyo, michezo kuna asilimia 20 inagawanyika kwenye fedha hiyo, mitihani kuna asilimia 20 kwenye fedha hiyo, ukarabati kuna asilimia 20 kwenye fedha hiyo, vifaa kuna asilimia 30 kwenye fedha hiyo. Niombi fedha hii ni ndogo mno na fedha hii inasababisha sasa hivi Walimu wetu kufanya njia mbadala ya kuwafaaulisha watoto ilimradi tu wasionekane kwamba wao hawana mafunzo kwenye zile shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi zimekuwa sasa wazazi wakiwa wanachangia, lakini kwenye uchangiaji wazazi wamefika mahali wanagoma. Wanasema Serikali inaleta fedha nyingi sana kwa sababu mnyumbulisho huu wazazi hawauelewi. Kwa hiyo niiombe Wizara yenye dhamana twende tujiwekeze sasa kwenye Sekta hii ya Elimu, kama tumekubali sasa Serikali kubeba mzigo wa elimu bila malipo basi twendeni sasa tuongeze ruzuku hii ambayo inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nataka niguse kwenye suala la viwanda. Kusini tuna Kiwanda kikubwa sana cha Saruji cha Dangote. Kiwanda hiki kina wafanyakazi zaidi ya 6,000. Kimetoa ajira ya kutosha, lakini kiwanda hiki kinashindwa ku-move kwa sababu ya kodi za *TRA*. hHpa karibuni mlikuwa mnasikia kwamba Kiwanda cha Dangote kinataka kufungwa, lakini Kiwanda cha Dangote wamefika mahali sasa wamechoka wanataka kuondoka. Kwa mfuko wa saruji mmoja *TRA* wanachukua shilingi 3,000, mfuko unaouzwa shilingi 11,000 kwa bei ya jumla. Ukienda ndani ya kiwanda kile, *maintenance* ya kiwanda, mkanda mmoja unavyokatika wa mashine unatumia zaidi ya milioni 180 kuagiza mkanda mmoja wa mashine. Twendeni sasa tuangalie kama tunahitaji kuboresha uchumi huu wa Tanzania lazima tufike mahali sasa viwanda vyetu tuvisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wawekezaji, kila tunapozungumza, sasa hivi nimeshazungumza na wawekezaji zaidi ya sita kutoka nje (*investors*) lakini wanasema kwamba Mtenga, hili suala kwenu haliwezekani. Ukitaka kufungua kiwanda, kuwa mwekezaji, shughuli yake ni kubwa mno. Mle kuna watu wapo zaidi ya nane au tisa, ukitaka kiwanda unamkuta *NEMC*, ukienda hapo *NEMC* mambo ya *NEMC* Mwenyezi Mungu mwenyewe anayafahamu. Pia kuna mtu anaitwa *TBS*, ndani ya kiwanda hicho hicho kimoja. Yuko mtu mmoja anaitwa *TRA*, lakini kuna janga kubwa la Kitaifa linaitwa *NIDA*, leo mwekezaji ametoka nje kadi ya *NIDA* anaipata wapi hapa Tanzania? Hili lazima tuliangalie, lakini kuna mtu anaitwa *OSHA*, pia mtu mwingine anaitwa Zimamoto. Vile vile Kuna kibali cha kuishi, hili nalo ni shughuli

nyingine. Vibali nya kuishi leo kama kuna wawekezaji ambao tayari wana wafanyakazi wao wako wanafanya kazi, kwenda ku-renew kibali tu cha miaka miwili au mwaka mmoja wanachukua takriban zaidi ya miezi nane au tisa. Hebu tufike mahali kama kweli tunahitaji sasa, tufike mahali tubadilike ili tuingie kwenye uchumi mkubwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri hawa *OSHA*, *NIDA* na kadhalika kwenye Sekta hii ya Uwekezaji hebu wakae sehemu moja ili shughuli ile iwezekane kupatikana. Yuko hapa mtu mmoja anaitwa Mkurugenzi wa *NEMC*, yaani afadhali leo unaweza kumtafuta Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukampata kuliko Mkurugenzi wa *NEMC*. Tunakwenda wapi? Leo tunazungumza kwamba nchi yetu tunataka iwe nchi ya uchumi, lakini uchumi wetu tunazungumza viwanda, ni kitu ambacho hakiwezekani. Ukiangalia kwenye viwanda vyetu, wafanyakazi ambao wanafanya kazi kwenye viwanda hivyo, mishahara yao wanayolipwa ni midogo. Serikali kama Serikali wanasema kuna viwango nya kima cha chini vimepangwa, sasa viwango vinavyopangwa nya kima cha chini tuangalie na kodi tunazowatoza wale watu na service za viwanda vyao wanavyofanya ili tufike mamlaka ya kuwabana wale juu ya mishahara yao ambao inalipwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshamaliza? Loh, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Toufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao na Mheshimiwa Ally Yahya Mhata ajiandae.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru

sana Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai wa kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Sambamba na hilo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa kuandaa Mpango huu. Niwapongeze pia ndugu zetu wa Kamati ya Bajeti kwa kuandaa taarifa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja ambayo ningependa kuizungumzia leo, mionganoni mwa hoja hiyo ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji. Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia hili suala la kilimo cha umwagiliaji nami pia naomba nichangie kwenye suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kujengwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji kulingana na Taarifa ya Mpango kwamba kutoka hekta 461,372 mwaka 2015 hadi kufikia hekta 694,715 mwaka 2020 bado kilimo cha umwagiliaji kinahitaji kufanyiwa kazi ya ziada. Nilitamani tungepata maelezo kwamba hizi hekta 694,713 zilifikiwa kwa lengo lipi, kwamba je, Serikali ilikuwa imepanga kufikia lengo kiasi gani katika suala zima la kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu ambazo nimezifuatilia inabainisha kwamba tuna zaidi ya hekari milioni 29 ambazo zinatafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, hadi sasa ambazo zimeweza kufanyiwa kazi yaani katika kilimo cha umwagiliaji ni hizi hekta 694,715. Leo ni miaka 50 na zaidi ya uhuru, kwa kweli kiwango hiki cha hekta hizi bado tuna safari ndefu sana kama tunahitaji mapinduzi ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomb nitoe rai kwamba tuone jinsi gani Serikali inajipanga vizuri kuhakikisha kwamba

kilimo cha umwagiliaji kinawekewa uwekezaji mkubwa ili kusudi tuweze kupata chakula cha ndani ziada, mazao ya biashara na ili kusudi tuweze kuza katika masoko ya nje. Leo nakumbuka asubuhi wakati Mheshimiwa Bashe akijibu swali la Mheshimiwa Timotheo Mnzava alizungumzia kwamba katika Mpango huu wana-*plan* kufikia hekta 1,200,000 za umwagiliaji. Maana yake ni kwamba hii labda inawezekana katika miaka mitano, lakini bado ina maana kwamba zitabakia hekta 27,800,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa bado naomba nitoe msisitizo kwamba hatuna budi sasa tuone mipango yetu ya Serikali tunafanyaje ili angalau tufikie hatua nzuri tuweze kujikomboa katika kilimo hasa kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, Serikali haina budi kuona jinsi gani tunaweza tukaboresha hii miundombinu ya umwagiliaji lakini pia uhamasishaji wa Sekta Binafsi na wadau mbalimbali waweze kushiriki katika hili suala la kilimo cha umwagiliaji ili mwisho wa siku sasa tuweze kuwa na mapinduzi ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa sita wa Taarifa hii imezungumziwa kuhusu maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo Morogoro. Hili jambo naipongeza sana Serikali, lakini pamoja na pongezi hizo nina ushauri kwamba, Serikali ione umuhimu kwamba kuna hii maabara ya mbegu lakini kuna kila sababu ya kuwa na maabara ya kupima udongo katika maeneo mbalimbali ya nchi hii. Kama tutaweza kupima udongo, ina maana kwamba zile mbegu ambazo zitakazosiwa zitaendana na ule udongo kulingana na rutuba yake. Kwa hiyo mwisho wa siku ina maana kwamba mazao yatakayopatikana yatakuwa ni mazao ambayo yataleta tija. Kwa hiyo, naomba nitoe ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilisoma mahali nikaona kwamba, wenzetu Mkoani Kigoma walikuwa na mradi wa FAO, mradi ule ulikuwa ukiwaelekeza wakulima jinsi ya kupima

afya na ubora wa ardhi. Sasa basi hebu Serikali ione itawezaje kuendesha huu mradi katika maeneo mengine ili wakulima waweze kupima ardhi na hatimaye waweze kulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sitazungumzia suala la zabibu. Sisi katika Mkoa wa Dodoma zao letu ambalo ni mkombozi ni zao la zabibu, lakini katika mpango huu sijaona sehemu yoyote ambayo Serikali, imezungumzia kidogo sana katika taarifa ya kamati, lakini bado sijaona mkakati wa Serikali wa kuendeleza zao la zabibu katika Mkoa wa Dodoma. Jamani zao la zabibu ni siasa katika Dodoma, lakini tatizo ni kwamba, zao la zabibu bado halina pembejeo. Mbegu ambazo zinatumika ni zile za miaka nenda miaka rudi kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ione jinsi gani itakavyoweza kusaidia kukuza hili zao la zabibu ili ndugu zetu wa Mkoa wa Dodoma waweze kuondokana na suala zima la umasikini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wamezungumzia kuhusu suala la mafuta. Na hasa wamezungumzia jinsi gani ya kuweza kuboresha mbegu za alizeti, mbegu za mchikichi, na kadhalika. Lakini basi hebu tuone kwamba, Serikali ijaribu kuangalia zaidi; kuna mafuta ya karanga, kuna mafuta ya ufuta, kuna mafuta yanayotokana na mifugo, vyote hivi najaribu kuona ili kusudi tuweze kupunguza utegemezi wa kupata mafuta kutoka nje.

Ninakumbuka miaka ya nyuma tulikuwa tuna mafuta ya pamba. Je, kwa nini Serikali isifikirie kuona umuhimu wa kuanzisha tena zile *ginnery* za mafuta ya pamba, ili kusudi tuweze kupunguza upungufu wa mafuta? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri sana hebu Wizara ione hilo, lakini jambo jingine kama muda utaniruhusu nilikuwa naomba nizungumzie kuhusu suala la afya. Kwenye suala la afya katika ule mpango wamezungumzia kwamba, vifo vimepungua kutoka 432 kwa vizazi hai laki moja. hadi sasa vifo vimeduwa 321,000 kwa vizazi hai laki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba, pamoja na kupunguza lakini hii namba bado ni kubwa. Tunatamani, yaani ndoto yangu natamani kama mwanamke nione wanawake hawafi kutokana na uzazi na hili jambo linawezekana. Kwamba, tukiwa na mipango kabambe ya kuhakikisha kwamba, wanawake hawa hawapotezi maisha yao tutapunguza mayatima na tutapunguza na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, wenzetu nchi ya Rwanda wameweza sana kujitahidi kupunguza vifo vya akinamama na watoto kwa kuwafuatilia kuona kuhakikisha kwamba, mwanamke au mama lazima kumfuatilia mpaka mwisho kuona anajifungua na anajifungua salama. Kwa hiyo, kama itawezekana na sisi tungeweza tukaweka program au kwa kufanya *field visit*, jinsi utakavyoilita, illi kusudi wataalamu wetu waweze kwenda kule, waweze kwenda kujifunza, kuona jinsi gani wenzetu wameweza kufanikiwa. Na naamini kabisa kujifunza ni jambo jema kabisa, mwisho wa siku na sisi inaweza ikawa vifo vya akinamama na watoto ikawa ni historia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa uchache niliona nichangie hayo. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, asante sana, nashukuru kwa kunipa fursa. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Simon Fiayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Yahaya Mhata, Mheshimiwa Neema Lugangira ajiandae.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Mpango wa Tatu wa Bajti ya Taifa letu. Nijikite moja kwa moja katika sekta ya kilimo, ni Dhahiri kuwa sekta ya kilimo imekuwa ikichangia kwa asilimia kubwa katika pato la Taifa. Lakini kwa bahati mbaya bajeti ya sekta ya kilimo imekuwa haitekelezeki. Imekuwa kilimo kikipewa bajeti ndogo sana na kusababisha mambo mengi kukwama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sekta hii kuchangia katika pato la Taifa letu wakulima wetu wamekuwa wakikutana na changamoto nydingi sana na kubwa katika suala zima la pembejeo za kilimo. Na changamoto hii inasababishwa na mlundikano mkubwa wa kodi uliopo kwa wafanyabiashara na umesbabisha wakulima wetu kuumia sana, lakini kwa kuwa ni jukumu letu sisi kama Waheshimiwa Wabunge, kuhakikisha tunaishauri Serikali ili tuweze kuzipitia sheria za kodi na kuzifanya marekebisho. Tuna jukumu kubwa la kufanya maana sheria zilizopo zinawaumiza sana wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili pia liendane sambamba na kutafuta soko. Kumekuwa na changamoto kubwa ya masoko ya mazao, hususan katika Mkoa wa Songwe wananchi wetu wamekuwa wakijishughulisha sana na zao la kahawa, zao la mahindi, zao la mpunga na maharage na mambo mengine. Lakini kwa sasa ukienda Songwe mahindi gunia linauzwa kwa shilingi 30,000/= tu wakati huo mkulima nanunua mbolea kwa bei ya 65,000/= mpaka 70,000/= mbolea aina na *DAP*, kitu ambacho kinasababisha wakulima wetu kuumia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linawatesa sana wakulima wetu na kuwakatisha tamaa sana katika suala zima la kilimo. Kwa nini nasema tuangalie masoko? Asilimia kubwa wananchi wa Mkoa wa Songwe na Rukwa walikuwa wanategemea sana kuwauzia Wakongo mahindi na Wakenya, lakini leo hii biashara imekufa, Wakongo hawawezi kununua tena mahindi kwasababu, watu wa Afrika Kusini wameliteka soko la mahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkulima wa Tanzania akibeba mahindi kwenda kuyapeleka Kongo kutoka Tanzania kwenda kufika Kongo ni kilometra zaidi ya 1,000 lakini mtu wa Afrika Kusini akitoka na mahindi kutoka Afrika Kusini kwenda kufika Kongo ni kilometra zaidi ya 2,000 lakini mtu wa Afrika Kusini anauza mahindi kwa kilo 250/= na Mtanzania anauza kwa 360/= lakini bado haimlipi. Jambo hili linawakatisha sana tamaa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sababu ya kuweka uhusiano mzuri na mataifa ambayo yanatusaidia katika suala zima la soko, ili tuweze kuwanufaisha pia wakulima wetu na kutokuwakatisha tamaa. Lakini pia Serikali ituambie ni kwa namna gani kilimo ambacho ndicho uti wa mgongo wa Taifa letu kinaweza kuinua pato la Taifa. Ikiwa tu bajeti inayotengwa haitekelezeki kwa mwaka 2019/2020 utaona bajeti iliyotekelvezeka ni asilimia 15 tu. Sasa tutawezaje kuinua wakulima kama bajeti tunayopanga ndani ya Bunge hili haiwezi kutekelezeka kabisa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo tuna haja kubwa ya kutunga sheria za kusimamia utekelezaji wa bajeti ambazo tunazipitisha ndani ya Bunge hili, ili ziweze kutekelezeka. Na kuwepo nidhamu katika kutekeleza bajeti ambazo tunakuwa tunazipitisha ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la umeme. Tumeendelea kuzungumzia suala la viwanda ndani ya Taifa letu. Ni dhahiri kabisa kwamba, viwanda asilimia kubwa vinategemea umeme. Lakini leo ukienda katika Mkoa wa Songwe limekuwa ni jambo la kawaida umeme kukatika siku mbili mpaka tatu bila sababu za msingi. Sasa hawa watu ambaao tunataka wawekeze katika Taifa letu, wawekezaji wa ndani nan je tunawakatisha tamaa. Mtu hawesi kuweka kiwanda akitegemea kutegemea nguvu ya *solar* ama *generator* kuendesha kiwanda chake. Ni lazima ategemee umeme ili uweze kumsaidia kwenye kiwanda, sasa tusifike mahali kuwakatisha tamaa wawekezaji ambaao wanakuja kuwekeza katika Taifa letu kwa njia ya umeme tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii umeme Mkoa wa Songwe umekuwa ni kawaida kukatikakatika, lakini ukikaa Dodoma hapa unaweza ukajisahau kwamba, Songwe na Dodoma ni nchi mbili tofauti, lakini kumbe mikoa yote iko ndani ya Taifa moja. Umeme Dodoma mimi sijawahi kushuhudia umeme ukiwa umekatika ndani ya Jiji la Dodoma, lakini Songwe ni kawaida umeme kukatika. Tunawahamasisha vijana wetu kujivekeza, tunahamasisha vijana wetu kujiajiri, hivi leo kijana ame�iajiri katika kazi

anachomelea, wengine wana saluni, umeme unakatika siku mbili-tatu maisha yake atayaendeshaje kwa namna hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawakatisha tamaa pia vijana wetu. Tuombe suala la umeme pia lichukuliwe ili tuweze kuwatia moyo wawekezaji na vijana wetu ambao wameamua kujajiri ndani ya Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa mpango huu uendane na kuzipa nguvu halmashauri zetu ikiwa ni pamoja na kurejesha baadhi ya vyanzo ambavyo vimechukuliwa na Serikali kuu. Mfano chanzo cha *property tax*, chanzo hiki tuliona tu kwenye vyombo vy'a Habari kwamba, Waziri ametangaza kwamba, halmashauri watakusanya, lakini uhalisia ni kwamba, fedha hizo zitakusanya na halmashauri na zitapelekwa Serikali Kuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pengine tuone tunaona kwamba, inaonekana Serikali Kuu tumekosa watu wa kutukusanya tunataka halmashauri sasa itusaidie halafu mwisho wa siku fedha hizi zinakuja kwenye Serikali kuu. Tunaomba kama Serikali kuu imedhamiria kukirudisha chanzo hiki kwenye halmashauri, halmashauri wakusanye wao na fedha hizo ziingie katika mfuko wa halmashauri, jambo hili litatusaidia sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tunajua kwa asilimia kubwa ukiangalia kwenye masuala ya barabara leo hii tunazungumzia mambo ya barabara ambazo zinaendeshwa na *TARURA*. Tumekuwa tukifeli sana kwasababu, aslimia kubwa *TARURA* wanategemea chanzo cha ndani cha halmashauri na halmashauri tumekuwa tukipata fedha kidogo kwasababu ya vyanzo vingi kuchukuliwa na Serikali kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe sasa kama itawezekana vyanzo ambavyo vinawezekanika halmashauri kukusanya turidishe mikononi mwa halmashauri na

halmashauri iendelee kukusanya, ili iweze kujidesha pia. Kwasababu, kuna wakati tunapata hata hati zisizoridhisha kwenye halmashauri zetu kwasababu ya miradi kuchelewa kutekelezeka yote ni kwasababu ya Serikali kuu kutopeleka fedha kwa wakati na kutopeleka fedha za kutosha kulingana na bajeti inavyokuwa imetengwa na halmashauri. Tuweze kuzipa miguu halmashauri, ili ziweze kutembea na ziepukane na kupata hati chafu na hati zisizoridhisha. Vyanzo vingi ambavyo halmashauri inaweza kuvirejesha tuweze kuvirudisha halmashauri iweze kukusanya. Nashukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Justine Nyamoga ajiandae.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Naibu wake kwa kazi nzuri waliyoifanya kuwasilisha mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano, mpango wa tatu. Naomba nijielekeze katika njia gani ambazo nazipendekeza zinaweza zikaongeza mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi ya India kabla ya mwaka 2005 ilikumbana na changamoto ya wananchi wake kuhitaji kuwa na uraia pacha. Tatizo hili lilikuwa kubwa, lakini Serikali ya India ilikaa chini na kufikiria jinsi gani inaweza ikatatua tatizo hili na wananchi wake wakaendelea na maisha yao hivyo, wakaanzisha, wakawapatia kitu kinachoitwa *Over Seas Citizen of India Card*. Kadi ile iliwawezesha raia wote ambao ni wahindi by original/kuweza kuingia India kwa wakati wowote na muda wowote wanaotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivi waliweza kutatua matatizo matatu. Kwanza lile takwa la wananchi wa India kuwa na uraia pacha liliondoka kwasababu, lengo lao lilikuwa kuingia India na kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Kwa hiyo, kwa kuwapatia hizi kadi za *Over Seas Citizen of*

India raia wa India wanaoishi nchi mbalimbali waliweza kuja India bila matatizo yoyote na *ku-maintain* uraia wao. Kwa hiyo, Watanzania wengi wenyewe asili ya India ambao wako hapa Tanzania wanazo kadi hizi *Over Seas Citizen of India*. Hata raia wanaoishi Uingereza, Marekani, n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, na wahindi hawa wanapofika India wanapata *privilege* zifuatazo, kwanza wanaweza kushiriki katuika shughuli za uchumi ndani ya nchi ile. Kwa hiyo, wahindi wameweza kuwekeza, wameweza kupeleka uchumi, kupeleka mitaji India kwasababu sasahivi wamekuwa hawana tena pingamizi la kwenda India. Muda wowote na wakati wowote wanaweza kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili. Raia wa India na huyo ambaye haishi India wana haki sawa. Haki ambazo zinamuwezesha rala wa India, mfano haki za kushiriki katika shughuli za maendeleo, raia wa India na huyo ambaye anakaa nje ya India anafanya wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini waliweka utaratibu wa kuwazua hawa wenye *Over Seas Citizen of India* wasifanye mambo yafuatayo; kwanza waliwaambia tunawapatia hizi kadi, hizi sio *passport* kwa hiyo, wewe sio raia wa India ila tunakutambua kama muhindi mwenzetu. Kwa hiyo, hutaweza kupiga kura katika nchi yetu, hutaweza kushiriki katika shughuli za kiserikali au hautakuwa kiongozi wa kuchaguliwa. Na hautakuwa ukafanya shughuli za kununua ardhi ndani ya India, lakini unaweza ukawekeza katika nchi yetu. Kwa hiyo, India waliweza kuvutia mitaji mingi sana ndani ya nchi yao ndani ya utaratibu huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba tujaribu kuiga utaratibu wa India. Tunao Watanzania wengi ambao wako nje ya nchi yetu wana uwezo na wana pesa za kuja kuwekeza ndani ya nchi yetu. Lakini hawataki kuukana uraia wa hizo nchi. Na sisi hatuna utaratibu wa raia pacha, tuwapatie kadi tuwaite *Over Seas Citizen of Tanzania*. Wakija hapa waje kwenye shughuli za kiuchumi tu, hata ruhusiwa kupiga kura, hata ruhusiwa kuchaguliwa, hata ruhusiwa

kununua ardhi, lakini ataweba kuwekeza ndani ya nchi yetu. Nina imani kabisa tutakuwa na uwezo wa kuwawutia wahindi wengi, waingereza wengi, wajerumani wengi, ambaao walikuwa raia wa nchi hii, wamarekani wengi wakaja na wakawekeza ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umewezesha nchi ya India kuinua sana uchumi na vijana wengi wameajiriwa, lakini pamoja na hivyo India waliweza kuvutia teknolojia kwasababu, nchi mbalimbali zilikwenda na wakaweza kuleta teknolojia mbalimbali. Kwa hiyo, halikadhalika kwa nchi yetu nina uhakika kabisa tutakapotumia utaratibu huu tutapata *knowledge* za mataifa mengine ndani ya nchi yetu; madaktari watakuja kwetu, *ma-engineer* watakuja kwetu na wataalamu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa pili ambaao naupendekeza, sisi nchi yetu ya Tanzania, natoka Wilaya ya Nanyumbu. Wilaya yangu inapakanwa na nchi ya Msumbiji. Mheshimiwa Mtenga alipokuwa anaelezea daraja la Mtamba Swala liko ndani ya wilaya yangu. Amezungumzia kutokuwa umuhimu wa lile daraja katika maeneo yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lile daraja liliengwa *purposely* kwa ajili ya kuinua uchumi wa watu wa Kusini, tati zo ambalo lipo upende wa pili wa lile daraja miundombinu ni mibovu. Naomba sana Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje watumie nafasi hii waishauri Serikali ya Msumbiji wawewe kuimarisha barabara kutoka Mtamba Swala kwenda mkoa unaofuata ambaao hauko kilometra nydingi. Sasa hivi ninavyozungumza mbaao zote zinazokuja Dar-es-Salaam, mbaao ngumu, zinatoka Msumbiji zinapitia Daraja la Mtamba Swala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunanufaika sana kuwepo kwa lile daraja. Vijana wa Mtwara, vijana wa wilaya yangu wanafanya biashara na mkoa wa jirani wanapeleka mahindi, wanapeleka mchele, wanapeleka samaki, wanapeleka dagaa. Nina imani kabisa endapo

miundombinu itaboreshwa upande wa pili wa lile daraja hali ya kiuchumi wa wananchi wetu itaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu naomba sana ndugu zangu viongozi wetu Mawaziri, hawa wawekezaji tulionao tuendelee kuwa-*maintain*. Kuna tabia ambayo sasa hivi imejengeka, hawa wawekezaji tulionao tunawakatisha tamaa. Tunao wawekezaji wanaofanya biashara ya kuingiza faida, lakini pia tunao wawekezaji wanaotoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu tuna Hospitali ya Ndanda tuna Hospitali ya Nanyangao na majirani zetu pale Tunduru wana Hospitali ya Mbesa. Kuna watu wa *foreigners* wanaoendesha zile hospitali wanapata tabu sana ku-renew vibali vyao. Unashangaa mtu anamkatalia daktari ku-renew mkataba wake; unajiliza huyu anatafuta nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nawaomba; hawa watu wanao-renew mikataba ni watalam, na kitendo cha hawa kuwepo wanaongeza utaalam kwa *local staffs* wetu. Leo unamwambia muda wako umekwisha ondoka aje mwengine. Uapomfukuza yule mtaalam maana yake unaiua ile Hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ningeomba, Mheshimiwa Waziri, mama yangu, shemeji yangu, Mama Jenista; hawa wataalam wetu wanatuangusha. Haiwezekani leo unamnyima daktari kuongeza mkataba. Daktari anakataa kuongezewa mkataba wanatutakia mema watu hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, unapomkatalia daktari hata wagonjwa hawaendi tena. Kuna watu wanakuja kwa sababu *Doctor Yahya* yupo pale. Leo unamwambia rudi kwenu halafu ile hospitali unamuachia nani? Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, wataalam wetu wanakotupeleka siko, waangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini linguine, kuna baadhi ya *missions*, mashirika ya dini wanatoa huduma za uchimbaji

wa visima. Kuna mashirika kule kwetu wanachimba visima kwenye shule bure. Yule m-*mission* mkataba umekwisha amekataliwa kuongezwa, anachimbia shule kumi, kumi na tano bure, unamkatalia unapata nini? Amekuja na pesa zake, amekuja na utaalam wake amekuja na vyombo vyake unamwambia muda wako umekwisha rudi kwenu, maana yake wewe hutaki wananchi wetu wapate maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana wataam hawa waangaliwe; hasa hawa ambao wanatoa huduma. Mashirika yetu ya dini wana watu wa namna ile wanaanza kufukuzwa eti kwasababu muda umekwisha, jambo hili kwakweli halikubaliki katika uchumi wetu...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, muda umeisha, ...

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Mheshimiwa Neema Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ajiandae.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nami ningependa nijielekeze katika kuhakikisha namna ya kuipunguzia Serikali gharama; kwasababu kwa siku mbili hizi tumesikia michango mingi sana ya Waheshimiwa Wabunge ambayo yote inalenga kuboresha hali ya uchumi wetu na kuboresha pia hali ya maendeleo ya Taifa. Lakini ili Serikali iweze kutimiza yote hayo Serikali inahitaji fedha, Serikali inahitaji Bajeti. Kwa hiyo mimi ningependa kuishauri Serikali, ifike mahala sasa iangalie suala zima la idadi kubwa ya mahabusu walio gerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwasababu hivi sasa Tanzania ina takribani wafungwa 16,836, lakini vivyo hivyo ina maabusu 16,703 ambapo Jeshi la Magereza kila mwezi linatumia takribani milioni 900 kwa ajili ya kuwalisha hawa wafungwa pamoja na mahabusu; sasa hii ni gharama

kubwa sana kwa Serikali. Nasema ni gharama kubwa sana kwa Serikali kwasababu Jeshi la Magereza halina vyanzo vya mapato ilhalii linajitegemea. Kwa hiyo binafsi kwanza ninafarijika sana kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa hiyo jambo hili analifahamu fika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile hata katika hotuba za hivi karibuni za Mheshimiwa Rais Mama yetu mpendwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameongelea pia suala la idadi kubwa ya mahabusu gerezani. Sasa tupate picha kidogo ikiwa tutaweza kupunguza idadi ya mahabusu gerezani, ina maana kati ya ile milioni 900 kila mwezi...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ni taarifa ndogo tu. Katika mchango wake amesema Waziri wa Fedha alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda tu kumjulisha kwamba alikuwa pia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwenye hilo eneo u-concentrate vizuri kuishauri Serikali, ahsante (*Makofii*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema endelea na mchango wako.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru lakini pia naomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mantiki hiyo ile milioni 900 ambayo Jeshi la Magereza inatumia kila mwezi kwa ajili ya kulisha chakula wafunga na mahabusu tukiweza

kupunguza idadi ya hawa mahabusu ina maana kuna kiasi kikubwa cha fedha ambayo tutaweza kuokoa; na kiasi hicho kila mwezi kitaweza kwenda kufidia kiasi kikubwa cha fedha ambacho kinahitajika ili kutekeleza mipango mbalimbali na ushauri mbalimbali ambao wametoa Waheshimiwa Wabunge ndani ya hizi siku mbili.

Kwa hiyo mimi ningependa kuchukua fursa hii kuishauri Serikalichukue maamuzi madhubuti kabisa ya kuona namna gani tutapunguza idadi ya mahabusu kule gerezani kwa lengo kubwa la kuchangia kupunguza gharama kwa Serikali. Kwasababu mimi ninaamini tunavyochangia mpango lazima pia tuangalie tunaipunguziaje mzigo Serikali, tunaokoaje fedha za Serikali ili zielekezwe huko kunakostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi naona huu ni upotevu wa fedha usio wa lazima. Kwa hiyo pamoja na ushauri huo pengine njia nyininge ambayo tunaweza tukafanya Mahakama ibebe jukumu la kugharamia hii bajeti ya kulisha hawa mahabusu wako gerezani kwasababu kimsingi wako kutokana na ucheleweshaji wa wao kuhakikisha kwamba kesi zote hizi zinafikia kupata hukumu. Na kwa mantiki hiyo hiyo pengine hata na Jeshi la Polisi pia linajukumu katika hili; kwasababu ni kuendelea kuionea Jeshi la Magereza ilhali Serikali imesema ijitegemee na Jeshi la Magereza halina mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi binafsi nina imani kubwa sana atakapokuja kuwasilisha hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ukizingatia, kama alivyosema dada yangu pale kwamba alikuwa ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alikuwa pia ni Waziri wa Katiba na Sheria basi atatueleza ni namna gani Serikali inapanga kwenda kupunguza idadi ya mahabusu ili ile bajeti ambayo inatumika hivi sasa iende kwenye mambo ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba kuunga mkono hoja, nashukuru sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika ajiandae.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujielekeza zaidi kwenye masuala mawili. La kwanza nitazungumzia suala ambalo linahusu asilimia 10 ambayo imekuwa ikitengwa kwa ajili ya akina mama, vijana na watu wenyewe ulemavu na suala la pili nitazungumzia kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kulizungumzia hili suala la asilimia 10 kwanza kwa kuanza kwa kupongeza sana Mabunge yaliyopita ambayo yaliona umuhimu wa kuwepo na mfuko huu. Nimebahatika kuwa kwenye Kamati ambayo inahusika na Utawala na Serikali za Mitaa, kwa hiyo nilipata nafasi ya kutosha ya kutathmini mikoa mingi jinsi ambavyo mwenendo wa mfuko huu unavyoendelea; na hiyo ndio imenipelekea kuona kwamba nielekeze mchango wangu huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia wakati mfuko huu unapoanzishwa ulilenga kuunga mkono vikundi vyatvijana, akina mama na watu wenyewe ulemavu kujihusisha na shughuli za ujasiriamali, na umekuwa na mafanikio makubwa; na mpaka kufikia taarifa zilipotolewa inaonekana vikundi vingi vinafanikiwa na kumekuwa na marejesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoangalia na nilivyofanya tathmini nikagundua kwama kwa sasa, tayari kuna fedha nyangi; na hapa ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa TAMISEMI na Waziri anayehusika na Vijana na Maendeleo, kwamba yale marejesho tu ambayo yapo na yamezuiliwa kwenye *account* kwenye Halmashauri mbalimbali yanatosha kuanzisha mfuko wa vijana kwa ajili ya miradi ya kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwasababu ule mfuko bado ile asilimia 10 inatolewa; kwa hiyo akina mama, vijana na wenyе ulemavu hawata kosa ile mikopo; na kwa wale wanaopata mikopo, miradi mingi inayoanzishwa inaanzishwa kwa ajili ya mitaji ya milioni mbili, milioni tatu nakadhalika ambayo inatosheleza kwa hiyo asilimia 10. Hata hivyo, kwasababu kuna marejesho ambayo halmashauri nyingi zimeiweka kwenye *account* na hazitumiki, kama leo yangetolewa maelekezo kila mkoa ukusanye yale marejesho tu yote, kila mkoa ungeweza kuanzisha mradi mmoja mkubwa wa kimkakati kwa vijana akina mama au wenyе ulemavu. Maana yake ni kwamba tusingehitaji kusema tunataka mtaji, tungkuwa nao kutokana na hela ambazo tayari zilitengwa, zimetumika na zimerejeshwa na haya marejesho yataendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninapendekeza kwamba, sawa tumeanzisha kwenye ngazi ya halmashauri tumekuwa na hiyo mikopo inatolewa, sasa twende hatua nyingine. Tunao vijana wenyе mawazo mapana wanahitaji milioni 50 wanahitaji milioni 100, wanahitaji milioni 200 ili kuanzisha viwanda, wanahitaji *ku-export* ili tuweze kufanya Kilimo kikubwa (*estate farming*); tufanye *Industrialization* wakilima mabarachichi walime mashamba makubwa. Hao ambao wanahitim uvyo vikuu ambao ni wengi basi sasa uanzishwe mfuko kutokana na marejesho yale. Hata kama si marejesho yote ila kutokana na yale marejesho uanzishwe mfuko ambao utatoa mikopo bila riba kwa hawa vijana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na huo mikopo maana yake ni kwamba tutakuwa tumezalisha ajira na wakati huo huo ule mzunguko wa ile fedha utaendelea huku halmashauri zikiendelea kutoa ile asilimia 10 na vile vikundi vyा akina mama, vijana na watu wenyе ulemavu vikiendelea kunufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti ya CAG inaonesha kiasi ambacho kilikuwa hakijarejeshwa mpaka kufikia Juni 2020 ambayo ni bilioni 27. Lakini ripoti ile inasema

jumlah ya shilingi bilioni tatu zilikuwa zimetumika kwa matumizi mengine; jumlah hizo tu peke yake ni Shilingi bilioni 30. Hizi fedha zote kama zingerejeshwa zikawekezwa kwenye hiyo miradi ya kimkakati ya vijana na akina mama tusingekuwa tunazungumzia kutengeneza *crisp* peke yake, kutengeneza batiki peke yake na kutengeneza karanga peke yake. Tungeanza kuzungumzia viwanda vikubwa vitakavyoleta changamoto nzuri kwa akina mama kwa vijana na kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hatuwezi kuishia kusema kwamba, akina mama wa Tanzania watatajirika kwa kukaanga karanga peke yake, hatuwezi kusema watatajirika kwa kutengeneza batiki peke yake; lazima wasonge mbele kushona suti; na hata hii mimi nimeshona hapa hapa Tanzania; lazima wasonge mbele kwa lengo la kuboresha. Na tayari hawahitaji kutafuta fedha mahali pengine, wanafanya kazi na wanarudisha kwenye mzunguko ule na hiyo hiyo hela inaweza kutosha kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama watu wanataka kufanya mararibio mimi nipo tayari kuwakaribisha kwenye Jimbo langu la Kilolo tufanye majoribio. Jimbo hilo linakusanya zaidi ya Shillingi bilioni nne na kwa hiyo hatuwezi kukosa zaidi ya Shillingi milioni 200 za kuanza mpango wa Kimkakati kama huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hoja hiyo ambayo kwakweli nina *passion* nayo sana na ninafikiri kwamba ni jambo ambalo kama tukilifanya kwa umakini linaweza kututoa hapa tulipo bila kumsumbuwa Waziri, ili hizo fedha nytingine ziende kwenye kujenga reli ile ikamilike, ziende kwenye Mradi wa Maji wa Mwalimu Nyerere ambayo mimi nina imani nayo sana; basi hii za akinamama na vijana tuziwekeze ili zizunguke vijana wetu wawe na hela kwenye mifuko yao, akina mama wawe na hela kwenye mifuko yao na watu wenye ulemavu wawe na hela kwenye mifuko yao. Kama ambavyo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu amesema, kwamba mifuko kidogo haina hela basi hizi zinaweza kusaidia kuongeza mapato ya vijana hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nigusie kidogo kwenye suala la Kilimo. Kilimo kinakwamishwa, na watu wengi wameshasema, na suala zima la pembejeo. Mimi ninatambua kwamba kuna mfuko unaitwa mfuko wa pembejeo. Na kwenye sehemu nyingi, hata mimi nilipozunguka kwenye jimbo langu shinda kubwa ni mbolea, shida kubwa ni mbegu. Imefikia wakati hadi kuna mikopo umiza ya mbolea. Kwenye baadhi ya maeneo kule, mtu anakopesha mbolea kwa Shilingi 50,000 wakati wa mavuno anakuja kuchukua Shilingi 150,000 kwa sababu wakulima hawana mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu mfuko wa Pembejeo makusudi yake ulioanzishwa unatakiwa ufanyiwe mapitio ili wakulima wapate pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika wakati Fulani ilijaribiwa mbolea ya ruzuku, na hapa katikati zikajitokeza hata baadhi ya kampuni; moja inaitwa *YARA* tena ilifanya hivyo hata Jimboni kwangu kule Kilolo, kwa kuwaandikisha watu kwa kupitia matandao wa simu kwamba watapewa mbolea ya ruzuku na baadaye niliwakuta pale kwenye Maonesho ya Nanenae pale Iringa mjini; nikawauliza nyie vipi? Wakasema ilikuwa ni bahati nasibu, kwa hiyo waliopata wamepata na wengine hawakupata. Sasa tukienda huko tunauliza maswali wale watu ya *YARA* wako wapi? Kwasababu hawakusema mwanzoni kwamba ile ilikuwa ni bahati nasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii yote ni kutokana na kero kubwa ya pembejeo ambayo tusipoitatu kwa njia sahihi kama ilivyo vitu vingine kama ambavyo tumefanyikiwa kwenye vitu vya *force account* hiyo Wizara ya Kilimo itafutiwe kitu kinachofanana na hicho ili mbolea iweze kwenda kwa wananchi ili mbegu ziweze kwenda kwa wananchi na wale wananchi waweze kuendelea kufanya kilimo chao kwa mafanikio makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nigusie jambo la mwisho kidogo tu, ambalo nimeamua tu kulichomekea kwasababu nafikiri ni la muhimu sana kwa

Watanzania. Jambo hili linahusu huu mkopo wa elimu ya juu ambayo inawaumiza watu wengi ambao ni walimu na wafanyakazi wa kada mbalimbali ambao wapo kwenye kulipa. Ninaomba wahusika wakasome ukurasa wa 61 na wa 62 wa Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Serikali ya ile ya Idara za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inayozungumza kwamba kuna watumishi 3,038 wanakatwa mishahara yao wanacholipwa ni chini ya $\frac{1}{3}$ na maoni yake ni kwamba hiyo imetokana na malipo ya Mkopo wa Elimu ya juu. Ushauri wake yeye mwenyewe amesema pale, Wizara husika iangalie kwanza mikopo yenyele lakini jinsi ya ulipaji wa ile mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu muundo wa mikopo yenyele mpaka ulipaji wake upo watu unaowaumiza. Kwenye miundo ya mkopo watu wamesema sana hapa kuhusu wananchi wengi tulionao huko ambao kwakweli ni maskini.

Mimi nina barua za wanafunzi wawili ambao wameahirisha masomo yao, mmoja wa pale *SUA*, kwa kushindwa kulipa na huyu mwanafunzi nimejiridhisha ni mtoto wa maskini na ameahirisha mwaka kwasababu ya mfumo wa ukopeshaji. Lakini hapo hapo kwenye kulipa hao watu wanaokatwa mkopo mpaka wanalipwa chini ya $\frac{1}{3}$ ni kwasababu ya kukatwa hii asilimia 15 na walikuwa na mikopo mingine. Hawa tunataka waendelee kujandikisha kwenye madaftari ya kwenye maduka ili wanunue chakula cha mwezi mzima kwasababu tumekata asilimia 15, wanatutumikia kwa miaka 30. Wanaweza kukatwa zaidi ya hayo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kengele ya pili imeshagongwa Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde atafutaiwa na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mheshimiwa Nicodemas Maganga ajlandae.

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyetuwezesha kufika siku ya leo na kuniruhusu mimi kusimama hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwama utekelezaji wa Mpango unahitaji fedha, na viko vyanzo vingi ambavyo vimeainishwa lakini moja kati ya chanzo ni mapato yetu ya ndani. Hivyo kwasababu dhima ya mpango inasema vyema kabisa, ni kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Kwa hiyo imani hapa ni kwamba fedha zilkipatikana za kutosha za kutekeleza mpango huu tutakwenda kuifikia dhima hii. Nataka nichukue fursa hii kipekee kabisa kuuenzi mchango mzuri sana wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwenye suala zima la upatikanaji wa mapato ambayo naamini pia Rais wetu mpandwa Mama Samia Suluhu Hassan pia atauendeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika kuishauri Serikali kuongeza wigo wa kodi (*tax base*). Duniani kote hivi sasa nchi nyingi zinaelekeza katika mfumo wa kodi ya huduma za kidigitali, wanaita DST ni *Digital Service Tax*. Kwa mujibu wa Jarida la Statista la mwaka 2019 hivi sasa duniani kuna watumiaji wa mitandao ya kijamii zaidi ya bilioni 3.6 ambaao katika nchi zinazoendelea kule Ulaya wameanza na utaratibu huu, wameanza kuweka miundombinu ya kuwafanya walipe kodi na kodi hii imeanza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana katika uchumi wa nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ninavyozungumza hivi sasa nchi ya Ufaransa wameshakamilisha taratibu zote na sheria ya kutoza 3% halikadhalika Hispania na yenyewe wanatoza 3% na Uingereza 2%, huu ni utaratibu ambapo kama nchi pia lazima

tuangalie hili eneo halijaguswa kabisa. Kwa Afrika nchi ambayo imeanza kulifanya kazi jambo hili ni nchi ya Afrika ya Kusini. Afrika ya Kusini wameunda mpaka Tume chini ya *PBO* (*Parliamentary Budget Office*) ya Bunge la Afrika ya Kusini ya kuhakikisha kwamba wanapitia na kuona namna ambavyo watawatoza kodi hasa hawa *main players* wa kwenye *social networks*. Hapa nazungumzia *search engines* kama *Google*, *Amazon*, *Spotify*, huku kuna hela nydingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), kifungu cha 47 kimetoa ruhusa ya nchi yetu pia kutengeneza mifumo ya kukusanya kodi kupitia utaratibu huu. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mwigulu Nchemba twendeni tukaliangalie eneo hili, lina hela nydingi sana, badala ya kuendelea kuhangai na bodaboda na vyanzo vingine twendeni huku kuna hela nydingi ambayo imelala. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni maeneo mawili; la kwanza, tutengeneze *payment platform* ambayo itaifanya *TRA* iweze kutoza kodi. Hivi sasa tukinunua vitu kupitia kadi yetu ya *Visa*, *Mastercard* au *PayPal* pale *TRA* wana uwezo wa *ku-capture tax* wakifanya *integration*. Kwa hiyo, mfumo huu uwekwe vizuri na naamini kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu una uwezo wa kulisimamia hili likaongeza wigo wa mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka niwapongeze wameanza kulifanya, tukae na *main players* hawa *Facebook*, *YouTube*. Najua mmeanza na *Facebook* na *Facebook* kwa takwimu za mwezi Februari wana watumiaji zaidi ya bilioni 3.1 ulimwengu mzima na sisi Tanzania pia tukiwemo humo ndani. Mimi naamini kabisa hili liko ndani ya uwezo na tukilisimamia vizuri tutaongeza mapato kwa kiwango kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye kilimo, bado naendelea kuamini kwamba sekta hii ina mchango mkubwa sana kwenye uchumi wetu hasa katika

kilimo cha umwagiliaji. Hivi kwa nini tusiwe tuna miradi ya mkakati kwenye kilimo pia kama ilivyo katika maeneo ya miundombinu na uchukuzi, twendeni tukafanye haya kwa sababu naamini kabisa kilimo kina uwezo wa kutupeleka mbele zaidi kama sekta kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyavalia njuga sana yale mazao ya kimkakati lakini tumuongezee nguvu pia katika eneo hili. Rai yangu ni kumuomba kaka yangu Mheshimiwa Prof. Kitila na rafiki yangu Mheshimiwa Mwambe mkae pamoja na sekta binafsi ili tutengeneze soko la uhakika la wakulima wetu, kuwepo na *backward and forward linkage*, mkulima anayelima nyanya aunganishwe na kiwanda moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru na kumpungeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Hussein Bashe amewahi kufanya kikao na Bakhresa nafahamu lakini tulikaa naye pamoja pia kwenye suala la ukwaju tu kwa sababu Bakhresa hivi sasa anaingiza mtambo wa kiasi cha shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ukwaju tu lakini ukwaju huu ni wa kuutafuta. Sasa Serikali ndiyo sehemu ya *ku-take advantage* hapa kwa wakulima wetu, twendeni tukaweke mkazo hapo kwenye eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kuhusu zabibu, zabibu ndiyo dhahabu yetu Dodoma. Zabibu ya Dodoma nitaomba Wizara ya Kilimo itusaidie kufanya utafiti lakini inasemekana hakuna nchi yoyote duniani yenye uwezo wa kuvuna zabibu mara mbili isipokuwa Tanzania na yenywewe ni Dodoma tu. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iweke mpango mkakati madhubuti kulisaidia zao hili la zabibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatamani kuwatua akina mama wa Dodoma mabeseni yao ya zabibu ambayo wanauzia stendi wakatengeneze mchuzi wa zabibu badala ya kuhangaika kukaa kwenye jua Serikali ikawasaidia wakatengeneze mchuzi wa zabibu. Tunaishukuru sana Serikali imeshusha tozo ya mchuzi wa zabibu kutoka Sh.3,655 kwa

lita mpaka Sh.450 hali ambayo imechochea sana ulimaji wa zao la zabibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikuombe Mheshimiwa Bashe, najua unafanya kazi nzuri sana, umeshaunda Kamati ya watu 12 kuhusiana na zao hili la zabibu twendeni mbele Zaidi. Natamani kuiona Tanzania inasifika kwa zabibu maana ndiyo zao pekee linavunwa mara mbili duniani unalikuta Dodoma. Nikuombe Mheshimiwa Naibu Waziri kazi ambayo umeianza naomba tuimalizie tuwatue mzigo wakulima wa Dodoma tupate soko la uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa najua tayari wanaendelea na masuala ya tafiti na mnakuja na mbegu mpya, mbegu ya *Beauty, Georgina* na *Alphonse Lavalleé* ambazo naamini kabisa zitaongeza tija. Nikuombe sana ndugu yangu na kaka yangu Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Waziri katika eneo hili tuwasaidie wakulima wa zabibu wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu sisi tunataka tuanze sasa kuifanya Afrika Mashariki na Kati hasa Watanzania hapa tuache kuagiza St. Anne na *wine* zingine kutoka nje ya nchi, zabibu yetu ya Dodoma ndiyo zabibu nzuri na tamu kuliko zote pia ukiacha Italia. Hivyo niwaombe sana Wizara katika eneo hili twendeni tukawasakiidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini twende mbele Zaidi, Afrika Kusini hivi sasa kupitia zabibu inafanya utalii na imetengeneza ajira zaidi ya 450,000 kupitia mashamba ya zabibu. Mashamba ya zabibu hivi sasa ni utalii na uzuri katika Jiji la Dodoma kwenye *masterplan* yetu tumetenga maeneo ya kilimo cha mijini (*urban farming*), tunaomba msukumo wa Serikali. Tunataka tuifanye zabibu iwe sehemu ya kivutio cha utalii, watu waje washangae mashamba ya zabibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akija Dodoma hapa akutane na kaulimbiu ile ya maneno makubwa kabisa ya Kilatini wanasema: "*In vino veritas*", kwamba kwenye wine/

mvinyo kuna ukweli, waje waukutie ukweli huo Dodoma. Naamini kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Hussein Bashe na Prof. Mkenda mna uwezo wa kulisukuma hili. Tukifanya hili tutakuwa tumewasaidia sana wakulima wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumza kuhusu mamlaka ya kilimo bustani (*horticulture*), alitoa maelekezo hayo. Wizara ya Kilimo anzisheni mamlaka hii, *horticulture* inakuwa kwa kasi sana hivi sasa, mamlaka ikiwepo itatusaidia sana. Wakulima wa kilimo cha bustani amebaki mtu mmoja mmoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa inabidi kuwa na masikio manne manne hivi, mmeona namna Mbunge akisikia kengele ye ye mwenyewe anakaa kabla ya kuambiwa. Kwa hiyo, ni jambo jema badala ya kukatishakatisha mazungumzo unayokuwa unazungumza.

Tunaendelea na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi ajiandae.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Mpango huu wa Tatu wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie maeneo machache; eneo la kwanza ni sekta binafsi kwa ujumla. Ni ukweli usiopingika kwamba kwa kweli kama tunataka kufanya uchumi ukue sekta binafsi haikwepeki. Sekta binafsi ni muhimu, kwa hiyo, tuiwezeshe ili iweze kusaidia kwenye kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachojitokeza kwa kiasi kikubwa sana kwa miaka hii ya karibuni, nachelea kusema kwamba sekta binafsi imeingia katika *challenge* kubwa sana na kwa kiasi kikubwa tumesikia kwamba baadhi ya

wawekezaji katika sekta binafsi na hapa tunaongelea ngazi mbalimbali hatuongelei wakubwa peke yao, tunaongelea wakubwa wa kati na wadogo wamefika mahali wamekatishwa tamaa na baadhi yao wamefunga biashara au wamekaa pembedi wakiangalia kitachoendelea kama watazamaji. Hii haina afya kwa uchumi wetu na haina afya kwa mpango wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri jambo hili limeshapewa mwelekeo na Serikali. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutoa kauli ambayo imetoa mwanga mpya kwa nchi yetu. Mkubwa akishasema watendaji tunatakiwa tuwe tumeshaelewa, *this is the tone from the top*. Kwa hiyo, tunatakiwa sasa watendaji wajipange wakijua mwelekeo wa nchi yetu inavyoiangalia sekta binafsi ni tofauti na ilivyokuwa miaka ya jirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusishwaji wa sekta binafsi uko katika maeneo mengi, uko katika ngazi ya sera lakini uko katika ngazi ya mambo ya kikodi. Sekta binafsi ina vyombo ambavyo ndivyo maalum kwa ajili ya kufanya *dialog* na Serikali. Vyombo hivyo viro, kazi imekuwa ikifanyika lakini wote tunafahamu mwisho wa siku *challenges* ambazo sekta binafsi inazipata wengi tunaambiwa hapa zimefikia mahali ambapo wote tunangoja kitu kinaitwa *blue print* mkakati ambao ndiyo unaenda kujaribu kushughulikia masuala mengi ambayo dada yangu pale Jesca amezungumzia, ametamka neno pale nisingependa kulirudia lakini urasimu ambao ndiyo upo umeonyesha kwa kiasi kikubwa unaua sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe tu angalizo hii *blue print* inayoongelewa ni karatasi tu tunahitaji kuwa na *mindset change* kwa viongozi wa Serikali. Tunahitaji kuwa na *mindset change* katika taasisi mbalimbali zinazosimamia mambo yote ya kiuchumi kuanzia Benki Kuu, *TRA* na vyombo vyote vya udhibiti kwa maana ya *regulators*. Hawa watu wasipobadilisha *mindset* ya kuionna sekta binafsi kama *engine* ya kusaidia kukuza uchumi tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu, hatutapata matokeo tunayoyokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa sekta binafsi ni pamoja na kuifanya sekta binafsi ishiriki kwenye uchumi. Serikali ndiyo mtumiaji mkubwa wa rasilimali fedha ambazo mwisho wa siku zinaishia kwenye mikono ya Watanzania kwa kupitia shughuli zao mbalimbali. Tulichokiona ambacho mimi naamini kinadumisha uchumi wetu ni Serikali kuona kwamba inaweza ikafanya mambo mengine mengi yenye ya kibiashara. Tumeona Serikali wakati mwingine inajenga yenye, tumeona maeneo ambayo hata kazi za kawaida ndogo ndogo taasisi za kibiashara za umma ndiyo zinapewa zifanye kazi hizo, hii haisaidii kuinua uchumi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetunga sheria hapa za *local content* ambazo zinatakiwa zisaidie Watanzania ili waweze kushiriki kwenye uchumi. Napenda kusema sheria hizi zitabakia kuwa makaratasi tu kama Serikali yenye haitakuwa na *initiative* ya kuhakikisha mambo haya yanatokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee eneo lingine la kilimo. Ndugu yangu pale ameshaongelea eneo la kilimo na maeneo ambayo ameyaongea mimi sitaongelea lakini ni ukweli usiopingika kwamba bado sekta ya kilimo itabakia kuwa ndiyo sekta kiongozi ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kupeleka mbele uchumi wa nchi yetu. Sekta hii tunafahamu ina matatizo mengi na makubwa, inahitaji vichochoeo vya kila aina na kikubwa kuliko vyote ni miundombinu wezeshi. Tumeshaongea kwa kiasi kikubwa hapa sitapenda kulirudia lakini kwa kweli tukubaliane kwa wakulima hasa wa mazao fulani fulani mkakati kama tutaendelea kutokuwa na utaratibu wa kuwa na umwagiliaji wa mazao yetu, nina uhakika sekta ya kilimo bado itaendelea kubakia nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia Mpango ulivyoandikwa unaona bado umwagiliaji ni chini ya 20%. Mazao kama chai ambalo ni zao kubwa sana maeneo ya Nyanda za Juu Kusini, ili uweze kupata mavuno hasa unahitaji kuwa na miundombinu ya umwagiliaji. Kuna makampuni makubwa yanafanya uzalishaji wa chai lakini makampuni

hayo sisi tunasema yana mchango wake tunahitaji kwenda sasa kuwa na wakulima wadogo wadogo wa chai walio wengi ambao watatoa mchango wa moja kwa moja katika sekta ya chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujifunze kwa waliofanikiwa ukienda Bangladesh, sisi tuna viwanda 21 vya chai lakini Bangladesh wana viwanda vidogo vidogo vya chai 700. Wao Serikali imechukua jukumu kubwa la kuhakikisha hili linatokea kwa sababu chai inaa jiri watu wengi sana katika uchumi hivyo una uhakika wa kupata kodi nyingi katika uchumi wako. Siyo hilo tu unasa idia kuinua maisha ya watu na hii inaendana na dhana nzima ya uchumi shindani na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme moja ambalo limekuwa ni kikwazo kwa sekta ya chai. Chai ni zao la mkakati na la *export* lakini ukiangalia kuna tatizo kubwa sana la VAT. Kinachojionyesha ni wazi kabisa kwamba urejeshaji wa VAT katika maeneo mengi ya mazao ambayo yanapelekwa nje ya nchi umekuwa ni hafifu sana. Hii inawaondolea wawekezaji na wafanyabiashara mbalimbali uwezo wa kuweza kuwa na mtaji wa kuendeleza biashara zao na hiyo inaondoa na inapunguza ulipaji wao wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kwa kifupi madini. Eneo la madini tumeona na tumeshuhudia mafanikio makubwa lakini naomba niseme wazi kwamba kama ambavyo Prof. Muhongo alituambia asubuhi na mimi nikazie tusijidanganye, tusipime *success* ya sekta hii kwa kuangalia mapato ambayo tumeyapata mpaka leo kwani hayatokani na kuongezeka kwa uzalishaji. Inawezekana kuna ongezeko la uzalishaji lakini sehemu kubwa ya ongezeko hilo limetokana na kazi nzuri ya Serikali ya kuzuia utoroshaji hasa uliokuwa unafanyika kwa kutumia njia za panya. Kwa hiyo, inaonekana kama kuna ongezeko lakini kwa kweli uzalishaji haujaongezeka, hakuna migodi mipya mikubwa iliyojitokeza au iliyojengwa katika miaka mitano mpaka sita toka tumebadili sheria zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inabidi tuwe makini kwa sababu tunapoangalia Mpango tuangalie na *threats* za wapi tunaweza tukashindwa kuendelea. Mimi nalionna hili bei ya dhahabu siku zote huwa inakwenda juu na chini, wakubwa wameshaanza kukaa na tunaweza tukaona hali ya *stability* katika ulimwengu ambayo itasababisha bei ya dhahabu pengine, hatuombe, ianze kwenda chini na mara moja tutapata *impact* kubwa negative kwenye Mpango wetu, hili tulielewe na tulitilie maanani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tufanyeje sasa? Tufanye yale ambayo tumeshayasaki, twende kwenye maeneo ya madini mengine ambayo ni muhimu na tusichelee kuona kwamba Liganga na Mchuchuma ni eneo ambalo hatuna sababu kwa nini mpaka leo hatujaweza kuanza kuzalisha pale mawe pamoja na chuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kama hiyo ni kengele ya pili. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ni kengele ya pili. Shukrani sana. Mheshimiwa Nicodemas Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi na Mheshimiwa Abdulwakil Ahmed, ajiandae.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kupata nafasi ya kuchangia Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea mpango huu tuujadili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nipo kwenye Kamati ya Nishati na Madini, tarehe 12 tulifanya ziara kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere Rufiji, ule mradi unaenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia, huu maradi umeanza mwaka 1970. Nitumie tu muda huu kuishauri Seikali. Kweli tuna miradi mingi katika Mpango huu wa Taifa, lakini

ipo miradi ya kuipa kipaumbele ikaweza kwisha kabla nasi tukiwa hai duniani tukafaidi matunda yake. Simaanishi kwamba labda miradi mingine ninaipinga, hata yenewe ni mizuri, ila nikiangalia pato letu kwa Taifa la Tanzania, kwa mfano hii *SGR*ina gharama kubwa sana. Tunaweza tukajikita kule tukafeli kufikisha malengo na mwishoni tukaonekana tu, watu wa ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aliyewasilisha huu mpango, kwa kuwa wewe ni mzoefu sana ndani ya hii Serikali, leo tunajadili huu mpango, tunapitisha mabilioni na matirioni yaende tena kwenye mipango, ila nikiangalia ripoti ya *CAG* hapa kwenye usafiri wa anga kwamba tuna *short* ya shilingi bilioni 150, kiukweli kwa mtu mwenye akili timamu, yaani inatia uchungu na inaumiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwenye ili Taifa kuna watu wengine wanafanya kazi bure. Tukishuka chini huku Serikali inapoanzia kwa maana ya Vitongoji pamoja na Wenyeviti wa Serikali wa Kijiji, mimi Pasaka hii sikuila, nilikuwa nafanya ziara kwenye jimbo langu. Ukikaa nao wale watu, madai yao ni ya msingi sana. Hawalipwi mshahara, hawana posho yoyote, wanafanya kazi kubwa za Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye huu mpango nimeangalia, Mheshimiwa kaka yangu Waziri wa Fedha ni vema ungewaingiza hawa watu ili nao wapate haki yao ya msingi maana wanafanya kazi kubwa sana na wanaumia sana. Japokuwa hawana uwezo wa kuingia ndani ya hili Bunge Tukufu na kuzungumza mawazo yao, wanapoona watu wakubwa wanaleta hasara kwenye hili Taifa, kwa mfano shilingi milioni 150 wakati Watanzania wote tunafurahia sana uwepo wa usafiri wa anga, lakini pale inapoonekana *loss* yaani hapa ni lazima tukae vizuri tujiulize.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeze sana *CAG* huyu aliyetao hii ripoti, maana imetupa dira. Ninamwomba au nawaomba ma-*CAG* wote, hata tunapopitisha haya mabilioni yaweze kuwa na udhibiti. Nawapongeze Baraza

la Mawaziri kwa kuaminiwa tena na Mheshimiwa Rais, maana wengi walikuwa wana-vibrate baada ya hili tukio kubwa tuliyolipata Kitaifa kwamba wengi labda wanaweza wakakosa nafasi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri, sisi Wabunge tuna kazi ngumu sana. Tunapofanya ziara kwenye majimbo yetu tunabaini changamoto na tunawaleteeni, kuna baadhi ya Mawaziri hawatujali vile, tunabaki sasa hatuna majibu na ukiangalia watu wanahitaji kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sehemu nyingi ambazo zinachangamoto kwa mfano Wizara ya TAMISEMI; nampongeza tu dada yangu kwa kuteuliwa, lakini ile sekta ni muhimu sana kwenye jamii, maana vitu vingi vinalenga TAMISEMI. Zipo changamoto Serikali kabla ya mimi kuwa Mbunge ilikaa ikapitisha bajeti kama leo tunavyopitisha mpango huu. Fedha zilienda zikaliwa, watu hawajawahi kuchukuliwa hatua hata siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naiomba tu Serikali, hilo iliangularie kwa umakini sana na ichukue hatua haraka iwezekanavyo. Siyo sifa nzuri, wala siyo Uislamu wala Ukristo; kwa mfano, mtu anaonekana kabisa amehujumu fedha za walipa kodi ambao ni wafanyabishara wadogo wadogo, wanachangia kwenye pato hili la Taifa, wanajibana kununua hata nguo, halafu mtu mmoja tu au wawili wanakula pesa za wananchi wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huko mitaani kiukweli kuna shida kubwa sana. Hata kusema kwamba tuko katika uchumi wa katи, yaani mpaka inafikia wakati mwingine ukiangalia hali iliyoko mitaani jinsi ilivyo mbaya, unaona dhahiri kabisa kwamba sijui walitumia takwimu gani? Unashindwa kujua kwa vile hunu elimu ya kuweza kudadavua mambo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu siyo wakati wa kampeni, naiomba Serikali, nawe Mheshimiwa Mwigulu

Nchemba ni mzoefu na haya mambo ya uongozi, ufanye sasa ile *gear* uliyokuwa unatumia hata miaka yote ili kusudi hata wenzetu hawa wa maisha ya kawaida waweze kupata maisha rahisi mifukoni. Mshauri Mheshimiwa Rais ili kusudi wananchi wetu wadogo wadogo wawe na pesa kwenye mifuko yao. Sasa hivi huko mitaani hali ni mbaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongelea viwanda; tuna viwanda 4,460 na kitu, lakini kiukweli hali ni mbaya. Hata wapiga kura wetu waliotupigia kura wana hali mbaya. Tuliahidi barabara; naishauri Serikali tuelekeze nguvu nyingi kwenye miundombinu za barabara na kwenye miundombinu za maji. Kwa mfano mimi natoka Jimbo la Mbogwe. Kutoka ziwa Victoria kufika pale kwenye jimbo langu ni kilomita 80. Nimeangalia huu mpango, hakuna mahali panaonekana kwamba ni lini wananchi wa Mbogwe watapata maji kutoka pale kwenye Ziwa Victoria kwenda pale kwenye jimbo langu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shida kubwa sana ya maji, hasa Mbunge unapokuwa msibani, unalazimika unywe maji na baada ya kumaliza kuyanya, unaenda tena unaugua na unatumia ghamama kubwa kutibiwa *typhoid* pamoja na magonjwa mengine. Kwa hiyo, naiomba Serikali, yaani mpango huu, sawa tunauunga mkono, lakini i-sort vipaumbele muhimu kama vile maji ni kitu cha muhimu na afya. Kuna upungufu mkubwa sana kwenye hospitali, dawa hakuna kabisa kiuhalisia pamoja na vipimo. Kwa mfano pale Mbogwe kwangu, ninamshukuru Waziri wa Afya amefika amejionea hali iliyopo pale Masumbwe. Akina mama kila siku wanajifungua, lakini hakuna *X-Ray*, hakuna vipimo vya kumpima mtu kubaini kwamba ana shida gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vyema sasa tunapopitisha huu mpango, lazima vitu vingine tuvipe vipaumbele, maana ni muhimu kulika hii *SGR* pamoja na mambo mengine ya matrillioni na matrillioni ambayo hayana sababu kwa wananchi wetu wale wa kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi nyingine ni hii ya kilimo. Toka mwaka 1992 nikiwa mdogo, Serikali ya

Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, wakulima walikuwa wakipewa mbegu za pamba. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ukifanya huo mpango kwa wakati huu, wakulima wakapata pamba, tutakuwa tumelisaidia hili Taifa. Waheshimiwa Mawaziri mwangalie, unajua sasa hivi tuna nafasi hizi, lakini ipo siku tunaweza tukafungwa pengine kwa kupitisha hii mipango halafu inakuwa haina mafanikio. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeshuhudia Serikali ya Rwanda, kuna Mawaziri wamefungwa pale. Walikuwa wakipitisha hizi bajeti zinaenda ndani ya watumishi wa Serikali zinaliwa, hawafuatilii, wanarudi Bungeni tena kujadili, wanatuma tena mabilioni mengine yanaenda, lakini baadaye ufuatilaji unakuwa haupo, halafu mnarudi Bungeni hapa hapa kupitisha tena bajeti nytingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mwaka 2015 mlipitisha bajeti, lakini ile miradi hajakamilika na haina kiwango, lakini fedha zilienda na hakuna majibu. Namwomba Mheshimiwa Rais, kasi aliyoanza nayo asilegeze, aendelee hivyo hivyo. Japokuwa anashabikiwa sana na watu, wengine sio wazuri sana kuwaongelea hata hapa.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ukiona unashabikiwa sana hata jimboni, lazima usimame ufikirie, ni kwa nini wananihabikia sana kila mtu? Kuna wengine wanakushabikia ili ukosee kusudi wapate pa kupitia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua tuko kwenye siku za mwisho, lipo hili janga la *corona*, watu wanapata shida. Ukiangalia Kenya pale, wananchi sasa hivi wanalia, Serikali ilikopa matrillioni na mabilioni, kumbe sijui hata ugonjwa haukuwepo, sasa hivi wananchi hata wale wa kawaida wanachangia lile deni kulilipa. (*Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Rais aangalie kwa umakini sana, anapoona anashabikiwa sana na watu, lazima afikirie kwamba hawa watu wanaomshangilia wana heri au wanataka kutuingiza kwenye matatizo kabisa ambayo hatutayamaliza tena?

Afuate tu nyayo za Mheshimiwa Rais, siyo lazima afuate zote, ni kuchambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua Marehemu akifufuka hata leo akakuta hii ripoti kwanza iliyotolewa juzi hii ya ndege, siyo kweli Marehemu alinunua ndege hizi kusudi zile *short*, alinunua ili afanye biashara. Hawa watu waliosababisha hiki, wanatakiwa kuchukuliwa hatua. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, msicheke. Sisi tunaolipa kodi wenye mitaji ya kuungaunga hatukubahatika hata kuwa na elimu za juu sana, tunajua uchungu na tuna uchungu mkubwa sana na tumekuja humu ndani ili kusudi kuweza kukabana nao hawa wanaojiita wana *cv* na *degree*. *CV* zisitumike kwa ajili ya kuibia watu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waendesha bodaboda wana veparata wanalipa shilingi 20,000. Ina maana vyote vinaingia huku Serikalini, halafu inapoonekana shilingi bilioni 150 amekula mtu mmoja, halafu anabaki tu ana- *survive*, yaani tuwe *serious* ili nchi yetu iletu mabadiliko makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ilishaletwa hapa Bungeni, kwa hiyo, maana yake ni Taarifa ya wazi kabisa. Ni muhimu kuipitia hasa katika yale maeneo ambayo Wabunge mnataka kuchangia ili muwe na uhakika na zile taarifa. Kwa sababu kuna taarifa ambayo imetolewa kwa kifupi, halafu mtu akachukua hiyo sentensi, lakini kuna maelezo yaliyopo kwenye ile taarifa kubwa yenyewe; inawezekana yale ya kifupi, ama mtu kachomoa maneno mahali fulani yakawa hayatupeleki kwa namna iliyo bora.

Kwa hiyo, naomba mkaisome ile Waheshimiwa Wabunge, maana tutaitumia sana katika mwaka huu wakati tunasubiria Kamati zetu zitakapopata fursa ya kuziangalia hizo taarifa halafu watazileta humu ndani, lakini sisi kama Wabunge tumeshaletewa hapa na kama Wawakilishi wa Wananchi tunatarajiwa kuzisoma zile na tutumie zile taarifa kuishauri vizuri Serikali kwa sababu ndiyo kazi yetu kuishauri Serikali na kuismamia pale inapoenda vile ambavyo sheria haisemi na pia makusudio ya wananchi.

Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi atafatiwa na Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil Ahmed na Mheshimiwa Joseph Kamonga aijandae.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mpango huu wa Tatu wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa wasilisho zuri sana walilotoa hapo jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Maendeleo ambao Waziri aliwasilisha jana, una vipengele vitano ambavyo wanalenga kuvitekeleza. Nami nitajikita kwenye eneo la tano katika ule mpango na eneo hili ni lile linalozungumzia kuendeleza rasilimali watu ambapo Serikali inategemea kuanzisha Program za kuendeleza maarifa na ujuzi kwa kuwasaidia vijana wetu kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali mpaka Vyuo Vikuu. Kuna tatizo hapo. Kwa hiyo, nitalenga kwenye hili na nitaangalia mchango wa vijana kwenye kuchangia pato la Taifa, kwenye Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha kwamba kilimo ni kitu muhimu sana; mifugo na uvuvi ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na karibia kila Mbunge aliyesimama hapa leo hii amelisema hilo. Nafasi ya vijana kwenye kilimo sasa hivi siyo nzuri sana, vijana wengi hawashiriki kwenye kilimo. Wanaoshiriki kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo

na Uvuvi ni wazee ambao wameshachoka na hawajaacha urithi mzuri kwa vijana wetu kushiriki katika hizi sekta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, program hii ya Serikali nilitaka nishauri kwamba ni program muhimu sana kama tutashirikisha vijana na kama tutasaidia vijana, tuwafunze vizuri ili waweze kushiriki kikamilifu kwenye kuboresha Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi waweze kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanaomaliza Darasa la Saba, Kidato cha Nne, sekondari Kitado cha Sita, Vyuo vya Kati na Vyuo vya Juu, wengi wao pamoja na kwamba ni watoto wa wakulima, wafugaji na wavuvi wakimaliza masomo hawaendi kwenye kilimo. Wanakimbilia mijini, wanakwenda kuendesha bodaboda, wanakwenda kuwa machinga, wanakwenda kuajiriwa. Kwa nini wanafanya hivyo? Wanafikiria kabisa kwamba kilimo, ufugaji na uvuvi ni kazi duni kitu ambacho sio sawa kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itawekeza na kufuata ushauri ambao nitatoa leo hii hapa, nina hakika tunaweza kuwahusisha vijana wetu katika hizi sekta ambazo nimezitaja na watatoa mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Sasa nitoe ushauri kwa Wizara ya Elimu na TAMISEMI ikiwezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais alivyokuwa anawaapisha Makatibu Wakuu na Viongozi wa Taasisi za Serikali alielekeza tubadilishe mitaala. Alisema mitaala ibadilishwe, tuwafundishe vijana wetu, tuwape stadi ambazo watakwenda wakitoka pale wajajiri, wafanye vitu vinavyoonekana, yaani mtu akimaliza Darasa la Saba awe na *skills* za kumsaidia kwenda kuzalisha. Akimaliza *Form Four* iwe hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niishauri Wizara ya Elimu ibadilishe mitaala ifanye kilimo; kikijumuisha, kilimo, mifugo na uvuvi; liwe ni somo la lazima kuanzia Darasa la Kwanza mpaka Kidato cha Nne. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivi tutawafundisha hawa vijana kwa vitendo, tutaweka *components* nyingi. Nimesema kwenye hiki kilimo kitakuwa na hivyo vitu ambavyo nimevitaja, tutawafundisha ujasiriamali na ubunifu wa miradi ya kilimo kwa vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mtaalam wa kilimo. Ni kwa nini nilienda kilimo? Hiki kitu nilikipata Shule ya Msingi. Kuna siku tulikwenda kwenye *study tour*, kwenye Kituo kimoja cha Utafiti wa Kahawa kule Lyamungo, nikaona walivyopanda kahawa kwenye mistari, mahindi kwenye mistari, maharage kwenye mistari, nikasema hapa hapa, mimi nakwenda kusoma kilimo. Leo hii nami ni mtaalam wa kilimo na nimeshatoa mchango mkubwa sana kwenye nchi hii, kwenye hiyo sekta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama tutabadiilisha mitaala yetu tuhakikishe kuanzia Elimu za Awali, hii program ya Serikali ambayo Mheshimiwa Waziri *amepresent* hapa; kuanzia zile *programs* za awali tunafundisha vijana wetu kilimo, nakuhakikishia watakapotoka pale watakwenda kujajiri na watafanya vizuri, watachukua urithi wa wazee ambaa sasa hivi wengi wamechoka na hawawezi kulima tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo masoko yapo. Mahali pa kuanzia; kijana akijiingiza kwenye kilimo, akilima mahindi, mboga, mpunga, akazalisha mchele, *Fuso* huwa zinakwenda mpaka kijijini kuchukua haya mazao kule. Kwa hiyo, mahali pa kuza kwa kuanzia sidhani kama ni shida kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ushauri wangu kwa Wizara ya Elimu mlizingatie hili, tuwafundishe vijana wetu kilimo, ambapo nimeshasema kinabeba vitu vingi tu, ili waweze kujajiri watakapotoma Darasa la Saba na waachane na yale mambo ya kwenda kufanya umachinga, kuendesha bodaboda ama kuajiriwa kwa watu wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, nafikiri ni wakati sasa wa Serikali kuanzisha program maalum kila Wilaya kwa ajili ya vijana wetu na hizi Wilaya zitenge maeneo ya kutosha kwa ajili ya vijana. Haya maeneo yatatumika kama *block farm* zile ambazo Mheshimiwa Bashe amekuwa anasema, tuwapatie maeneo ya kulima, kufuga, maeneo ya kuanzisha visima vya kufugia Samaki. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wamejajiri baada ya kupata *study* hizi kule Shule ya Msingi na Sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishatengeneza hizi *block farms*, kwa mfano tukienda kule Kilimanjaro, wale wazee wangu kule kuna mashamba mengi yametaifinishwa, mashamba ya ushirika, nawashauri ikiwezekana yale mashamba badala ya kupiga kelele wanayatumia vibaya tuwape vijana walime kwenye hizi *block farms*, vijana walime kwenye haya mashamba ili wazalishe na waweze kuondokana na umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hizi *block farms* zitakuwa, tukishakuwa nazo itakuwa ni rahisi kuweka miundombinu ya umwagiliaji, kitakuwa ni kitu kirahisi sana, tutaweka miundombinu ya umwagiliaji na vijana wanaweza wakavuna mara mbili hadi tatu kwa mwaka. Nitatoa mfano kidogo tu, kijana akilima mboga ekari moja, tuseme amelima nyanya ana uhakika wa kupata milioni 22 kama amewekeza. Nisikilizeni vizuri jamani, ekari moja ya nyanya unaweza ukapata milioni 22 na hapo ukitoa milioni moja ya kununua pembejeo, mbegu na vitu vingine unabaki na milioni 21. Kuna kijana atakayekwenda kuwa Mmachinga kweli, huo ni msimu mmoja na ukilima misimu miwilli, ni pesa nyingi zimekaa, zimelala ambazo naomba tusaidiane ili vijana wetu wajijingize kwenye hii miradi ya kilimo na waweze kujipatia pesa ili waoe. Vijana wengi sasa hivi ukimwambia aoe anakwambia hapana maisha magumu bwana, nioe nitampa nini, lakini pesa zipo kwenye kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wakiwa kwenye hizi *block farms* wanaweza wakapatiwa huduma za ugani, watafundishwa namna ya kuzalisha vizuri, wanaweza

wakapatiwa mitaji na mikopo itakuwa ni rahisi sana kuwasaidia hawa vijana wapatiwe mitaji na mikopo. Nitatoa mfano tu, kuna maeneo mengi ambayo yana pesa ambazo vijana wanaweza *wakazi-access* na wakafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ule Mfuko wa Halmashauri, asilimia nne ambazo huwa zinatolewa, vijana wanaweza wakazipata. Kuna Benki ya Kilimo ya Taifa inaweza ikawasaidia hawa vijana, kuna mfuko wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo, unaitwa *SELF Microfinance Fund*, kuna Mfuko wa Pembejeo wa Taifa, wenzangu wameshausemea hapa, kuna Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali, kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (*Youth Development Fund*), kuna Mfuko wa Mheshimiwa Rais wa Kujitegemea (*Presidential Trust Fund*). Tukiweza kuwaunganisha vijana wetu na hii Mifuko, tukiwapa maeneo Mungu atupe ni? Nina hakika vijana watazalisha kwa hakika na tutawatoa kutoka hatua moja waende hatua nyingine, haya mambo ya kwenda kuwa Wamachinga, bodaboda yatakuwa ni historia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishafanikisha hilo, pia ni rahisi kuwaunganisha na masoko ya ndani. Tumeshona jitihada za Wizara ya Kilimo kwenye kutafuta masoko kwa mfano sasa hivi wanaotaka kulima soya soko lipo China, wanaotaka kulima mihogo Serikali imeshatafuta soko China. Kwa hiyo sidhani kama kutakuwa na shida kubwa sana ya soko na wakishaanza kuzalisha ni rahisi kuwaelekeza pia wafungue viwanda vidogo vidogo, waongeze thamani kwenye mazao watakayolima pale, kwa mfano wanaolima mpunga, wakishakoboa mchele badala ya kuuza *raw rice* wanaweza wakafanya *packaging*; wanaolima mahindi wanaweza wakasaga wakapaki; wanaolima nyanya wanaweza wakasaga wakakausha wakapaki, wakawa wameongeza thamani; *TBS* ikawasaidia vijana watakuwa wameanzisha viwanda vidogo vidogo kwa kusaidiana na *SIDO* na tutachangia kikamilifu kwenye uchumi wa Taifa hili.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil Ahmed, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kamonga, tutamalizia na Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Mpango huu ambao ni dira kubwa, mimi naita ni jahazi litakalotuvusha kama kuna upepo au hakuna upepo kama alivyosema Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Wabunge wengi walipokuwa wanachangia walizungumzia habari za *markets* yaani masoko, kwamba uzalishaji ni mkubwa lakini tuna upungufu wa masoko katika kuza bidhaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Naibu kwamba duniani au Serikali ya Marekani imetoa fursa kwa nchi za kiafrika ambao Mpango huu unaoitwa AGOA (*African Growth and Opportunity Act*) nadhani katika utawala wa Bush ameamua Afrika iweze kuuza bidhaa zaidi bila ushuru wa aina yoyote. Sasa ni vema zaidi tukajikita na masoko ya nje, nchi yetu ina utajiri wa bidhaa mbalimbali tunazalisha, kuna maparachichi, kuna aina ya bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nikifuatilia kwa karibu sana, kila Mbunge anayesimama anasema kwamba soko hatuna bidhaa zinaharibika, kwa hiyo naishauri Serikali kwamba soko la AGOA nalo likapiga hodi Marekani. Hili ni soko zuri na halina ushuru maadamu tu ile bidhaa iliyozalishwa iwe *brandyake made in Tanzania* na iko katika hali ya ubora. Tusiwe waoga, wakati umefika tutumie fursa za ulimwengu, tutumie madirisha ya ulimwengu kusudi na sisi tuweze kuuza bidhaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ipite. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kamonga tutamalizia na Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa maoni yangu kwenye Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa wasilisho zuri la Mpango na hasa vipaumbele sita vyta Taifa letu kwa ajili ya kuleta maendeleo. Wananchi wa Ludewa wanaipongeza sana Serikali ingawa wana mashaka bado sababu wakati wa awamu ya nne hii miradi ya Mchuchuma na Liganga walishaandaa hadi eneo kwa ajili ya uzinduzi. Mheshimiwa aliyekuwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alishaandaliwa kwa ajili ya kwenda kuzindua Miradi ya Mchuchuma na Liganga lakini bahati mbaya mpaka sasa muda mrefu umepita.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuwa Serikali imeingiza miradi hiyo kwenye kipaumbele na imeweka mpango, lakini bado wananchi wana mashaka na hilo. Mimi kama kiongozi wao nimeendelea kuwapa moyo na kuwaaminisha kwamba Serikali ya sasa ni Serikali ya vitendo, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri tuwe pamoja kwenye hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo wananchi ambao wameathirika na Mradi wa Mchuchuma na Liganga nao wamesubiria fidia kwa muda mrefu sana takribani bilioni 11 ni pesa chache sana kwa Serikali iwapo dhamira ya kuwafuta machozi wananchi hawa ili wawewe kuondoka kwenye maeneo haya wakafanye shughuli zao katika maeneo mengine. Toka miaka ya sabini wamezuiwa kabisa kuendeleza maeneo haya na fidia hawalipwi, kwa hiyo wananchi wanaona kama Serikali imekuwa katili kwao, hawa ni wananchi wa Nkomang'ombe na wananchi wa Mundindi na Amani ambao wanalinda mali hizi kwa muda

mrefu sana. Kwa hiyo naomba hili la fidia litekelezwe, kwa sababu tunavyozidi kuchelewa thamani ya ardhi inazidi kupanda, tutaingia mgogoro mkubwa sana na wananchi iwapo hatutachukua hatua mapema. Kwa hiyo, hil ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa kuwa Wilaya hii ina miradi mikubwa miundombinu yake bado ni changamoto kubwa. Barabara inayoanzia Itoni kwa Mheshimiwa Deo Mwanyika, Lusitu mpaka Ludewa na kwenda Manda takribani kilometra 211.44. Tunashukuru Serikali imetutengenezea lami kwa kiwango cha zege, lazima tuwe waungwana tukubali na tushukuru, kilometra hamsini ambapo thelathini zimekwisha kukamilika. Kwa hiyo tunaomba barabara hii ikamilike yote kwa sababu Serikali hii imetuletea meli kule Ziwa Nyasa ambazo zinatoa mchango mkubwa sana kuinua uchumi wa mwambao, lakini bahati mbaya meli zile zinakosa mzigo wa kutosha kwa sababu barabara hizi hazijaunganishwa. Kwa hiyo uchumi huu na miundombinu yake lazima viwe na mawasiliano kwa sababu sekta moja ya uchumi inaweza kutoa mchango kwenye sekta nyingine. Sambamba na hilo wananchi wa mwambao wanaomba kuwe na kituo cha meli kwenye Kata ya Makonde ili iweze kusaidia hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wabunge wengi hapa wamechangia kwamba wananchi wengi Watanzania ni maskini sana na wanaishi vijijini zaidi ya asilimia 75. Kwa hiyo tukijitahidi kutafuta masoko ya mazao kwa maeneo ya vijijini, tunavyosema uchumi jumuishi, uchumi shirikishi tutawagusa wananchi ambao wanaajiriwa kwenye sekta ya kilimo. Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wanatoka maeneo vijijini kama mimi ambako kuna wakulima wengi, wamezungumzia mazao yanakosa masoko. Kwa mfano wilaya yangu wanaongoza kwa kulima mahindi, nitatoa takwimu chache, kwa mwaka 2019/2020 tani zilizozalishwa zilikuwa 110,800 lakini ambazo kwa makisio zinatosha kwa matumizi ya chakula ni tani 46,852, tani za ziada ni 63,239 na ambazo mnunuzi mkuu wa mahindi kwa kule ni hawa wanaitwa *NFRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NFRA* walikwenda wakanunua tani 709 tu. Kwa hiyo unakuta tani zaidi ya 62,000, mahindi ya wananchi yalioza kwa kukosa soko, kwa hiyo ni muhimu Serikali ikaona haja sasa ya kutafuta wawekezaji waweze kufungua viwanda kwa ajili ya kuzalisha vyakula vya mifugo, viwanda kwa ajili ya kusaga nafaka na kwenda kuuza katika maeneo mbalimbali ili kuweza kuongeza soko kwa wakulima.

Mhehimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa Jimbo la Ludewa na maeneo mengine wanalamikia sana changamoto ya vijana kuhitimu vyuo vikuu na kukosa ajira. Kwa hiyo, tunavyozungumzia katika llani ya Uchaguzi kuzalisha ajira 8,000,000 wanaona kama ni chache sana, kwa hiyo wanaamini sekta mbalimbali hizi kama zitaanzishwa za viwanda na mikopo ya vijana kama ambavyo Mheshimiwa Nyamoga amezungumzia, tunaweza tukafungua soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye utumishi wa umma kuna pengo kubwa sana katika ile *Seniority*, kwa hiyo unakuta wako *Principal Officer* lakini wale *Juniors* hakuna, kwa hiyo kuna kupindi fulani tutazalisha tatizo kwenye utumishi wa umma na tutalazimika wakati mwingine kutengua baadhi ya kanuni za utumishi wa umma na sheria. Kwa mfano inakwambia ili mtu awe Mkuu wa Idara lazima awe amefanya kazi miaka saba, sasa itafika kipindi tutawakosa hawa watu, kwa hiyo lazima tuangalie na athari ambazo zinaweza kutoka hapo mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili watumishi wa umma muda mrefu kidogo hawajapandishiwa mishahara yao. Bahati nzuri aliyekuwa Rais wetu Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli apumzike kwa amani huko aliko, wakati akiomba kura aliahidi kwamba awamu hii anakwenda kutatua tatizo la ajira. Kwa hiyo ili kumuenzi, tumsaidie mama yetu mama Samia Suluhu Hassan kuweza kuajiri vijana ambao wengi hawana kazi. Hapa kwa kwakweli tutakuwa tumeongeza tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile na hii hoja ya kupandisha mishahara, nayo Mheshimiwa Rais wetu alikuwa ameshaahidi kwamba safari hii atapandisha mishahara na hili ni kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma, Sheria ya mwaka 2002 inasema mtumishi wa umma atapanda daraja kila baada ya miaka minne wengine, wengine miaka mitatu, kwa hiyo kupuuza sheria wakati ipo wakati mwingine sio hekima sana, ni heri kuifuta.

Kwa hiyo tuangalie hiyo, tuweze kuangalia watumishi wa umma kama ambavyo alama za Chama Cha Mapinduzi ni jembe na nyundo; jembe ni wakulima na nyundo ni wafanyakazi. Kwa hiyo tuwaenzi kwa sababu hata kwenye alama ya Chama cha Mapinduzi watumishi wa umma wamo na hawa wafanyakazi wamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hata wafanyabiashara kero zao bahati nzuri mama ameanza kuzishughulikia...

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, sijui ni kengele ya pili, au ya kwanza?

NAIBU SPIKA: Ya kwanza, malizia mchango wako.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nimshukuru Mheshimiwa Waziri William Lukuvi na Mama Mabula, walezi wangu hawa, wamenilea vizuri na nawaheshimu sana, walitoa ufanuzi kwa swali alilouliza jirani yangu Mbunge wa Nyasa, Mheshimiwa Stella Manyanya kuhusiana na ile *capital gain tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri na wewe ni Mwalimu wangu pale *Law School*, sheria inayoanzisha kodi hii ni Sheria ya Kodi ya mwaka 2004, Sura 332 na kuna sheria

nyingine ambazo zinasimamia ambayo ni Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334, rejeo la mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambazo zipo kwenye kodi hizi ni kwamba ili mwananchi aweze kuhamisha umiliki wa ardhi yake ambayo amenunua au amepewa kama zawadi, anakwenda Ofisi zaidi ya moja, Ofisi za Ardhi zinahusika katika kufanya uthamini, *TRA* wanakwenda kukadiria kodi. Kwa hiyo ile ya mwananchi nenda hapa, nenda hapa imekuwa kama usumbufu, kwa hiyo kama wangeachiwa Wizara ya Ardhi kwa sababu Serikali ni moja, hii kodi wangeweza kuisimamia vizuri, nina imani sana na Mheshimiwa Lukuvi na Mama Mabula.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamishna wa *TRA* amepewa mamlaka makubwa sana kwenye hii kodi, kwa hiyo hii nayo inachanganya sana wananchi. Pia ina mlolongo mrefu na kupoteza muda wa mlipakodi, ile nenda sijui kafanye *valuation*, kwa hiyo wananchi wengi wanabaki na nyaraka wanajenga bila kubadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo hayajapimwa vile vile kodi hii haitozwi, kwa hiyo kuna maeneo mengine katika miji mikubwa ambayo hayajapimwa *transaction* kubwa zinafanyika, lakini watu hawalipi kodi. Kwa hiyo kuna maeneo ya kuangalia na hata asilimia yenyewe kumi ni asilimia kubwa sana. Mtu ameaza nyumba milioni 100, asilimia kubwa, akiambia asilimia 10 anaondoka anaenda nyumbani na nyaraka. Kwa hiyo hapa tunaweza tukaangalia kuna mambo ambayo yanaweza yakarekebishwa ikiwa ni pamoja na elimu kwa mlipa kodi na vilevile kuboresha namna ya ukusanyaji. Mwananchi asisumbuliwe kuambiwa nenda hapa, nenda hapa, nenda pale, kuwe na mtu mmoja anasimamia kama ni wa Wizara ya Ardhi, afanye uthamini yeze kwa sababu ana watalaam, akusanye yeze kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono pia Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia ile kodi ya majengo

(*Proper tax*) ile wangerejeshewa halmashauri ili kuweza kuongeza mapato. Kwa sababu wana wataalam wa *G/S* wanaweza wakaweka vizuri mifumo ya ukusanyaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tutamalizia na Mheshimiwa Jacqueline Kainja atakayechangia kwa dakika tano.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ili niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa. Kwa kuanza kuchangia moja kwa moja niende kugusia upande wa upatikanaji na uongezaji wa uchumi katika Taifa letu kutokana na mpango huu na hatutoweza kukwepa suala la kuongeza uchumi wetu bila kuongelea wafanyabiashara. Suala la wafanyabiashara na Serikali, kuweka mahusiano mazuri kati ya mfanyabiashara na Serikali, lakini vile vile kuna malalamiko kati ya wafanyabiashara, haya tuweze kuyaangalia kama Serikali, kwamba mfanyabiashara anakuwa na kodi nydingi, lakini vilevile makadirio yake ni makubwa sana ambayo wakati mwingine hayana uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nitaenda kuongelea kwamba tunafanyeje, kwa hiyo naanza kwamba na hizo ambazo ni kama changamoto. Pamoja na hayo lakini mfanyabiashara huyu anapata changamoto nydingize za wachuuzi ambao wanafanya ujasiriamali au tunaita *Machinga's mbele* ya maeneo ya wafanyabiashara hawa. Simaanishi kwamba Wamachinga au wachuuzi watolewe, lakini kuwepo na utaratibu mzuri kama Serikali kuweza kuwezesha hawa vijana ambao ni wengi wanajikita kuweka biashara barabarani kuna wengine ni akinamama wana-risk hata maisha yao kwa kukaa karibu kabisa na barabara, wakati mwingine magari yanapita na vijana wetu ambao ni wengi wameenda kujajiri kwenye kazi ya uchuuzi ambayo ukiangalia haina tija kwenye Taifa kwa namna nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nishauri Serikali iweze kuangalia ni namna gani tunaweza tukaboresha upande wa kilimo kama ambavyo Wabunge wengine waliopita wameongelea suala la kilimo kwa aina mbalimbali ili tuweze kuwa na kilimo ambacho kina tija na kinamnyanyua mwananchi mkulima wa chini kabisa huyu aweze kuwa na maisha mazuri. Hawa vijana wote na akinamama watatoka huku kwenye kuchuuza hizi biashara ambazo hazina tija kwa Taifa na kwenda kuwekeza kwenye kilimo ambacho kitakuwa na maslahi katika maisha hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna suala la hizi kodi zinakuwa ni nyingi; kuna biashara inaweza ikawa biashara moja lakini mtu ana kodi kama kumi. Ukiziangalia zile kodi zinalandana, kuna kodi ya mabango, biashara bila matangazo ambayo tunataka huyu mfanyakabiashara tupate kodi kutoka kwake ni sawasawa na bure. Naongelea mabango yale mfanyakabiashara anaweka kwenye duka lake au kwenye jengo lake. Yale mabango yapo upande wa *TRA*, kwa hilo bango mfanyakabiashara anatakiwa achajiwe, bado napata shida kidogo, kama mfanyakabiashara huyu anatangaza tu biashara yake labda Neema Saluni ili mtu aweze kujua mle ndani kunatolewa hiyo huduma, aingie ili kupata ile huduma nayo anatakiwa akatwe kodi. Sasa tunategemea huyu mfanyakabiashara atangaze vipi ile biashara yake ili aweze kutuletea sisi kodi. Kwa hiyo kama Serikali, naomba iweze kuangalia upande huu, kuna vitu vingine ni vya kuondoa tu ili sasa huyu mfanyakabiashara ajitangaze vizuri na aweze kufanya biashara yake na kodi ije kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali iweze kuangalia sheria za kodi ambazo pengine inakuwa ni changamoto kubwa sana kwa wafanyakibishara hawa. Hata Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, shemeji yangu, naomba aweze kufuatilia Bodi ya Rufaa za Kodi ambako kule kuna malalamiko mengi ya wafanyakibashara hawa, wakiwa wanalalamika ili wakate rufaa kwa ajili ya zile kodi zimekuwa tofauti na jinsi ambavyo walitakiwa kukadiriwa. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri

wa Fedha aweze kwenda kuangalia bodi hii ili aweze kujua malalamiko haya ya wafanyabiashara ni yepi ili tuone je, tunayaboresha kwa namna gani ili sasa kama Taifa tuweze kuangalia upande huo wa wafanyabiashara tunaweza tukapata vipi kuinua uchumi wetu na pato la Taifa, maana wafanyabiashara bado ni kiini kizuri katika ukuaji wa uchumi wetu. Vilevile naomba pia Serikali iweze kuangalia *investors* ambao ni wa nje na wa ndani, waweze kukaa kuangalia ni namna gani wataweza kuweka mazingira mazuri ili watu waweze ku-*invest*, watu waweze kuwekeza katika nchi yetu, kuangalia sheria kanuni na taratibu ambazo zingine zinaweza zikawa zinamfunga sana *investor* ambaye anashindwa ku-*invest* kwa kadri ambavyo alikuwa anategemea na akaamua kuondoka na tukakwama kwenye kuingiza mapato kwa ajili ya kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo kama tutaweza kuruhusu wawekezaji wa nje na wa ndani tunaangalia kabisa tunaweza tukainua pato la vijana pamoja na akinamama, wakapata ajira katika makampuni ambayo yatakuwa yamefunguliwa na viwanda mbalimbali, akinamama hawa ambao wengi wanajitoa kufanya biashara za uchuuzi, wakati mwengine zinahatarisha maisha yao barabarani. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Fedha aweze kuliangalia kwa upana huo kwa ajili ya kuweza kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa siku ya leo. Niwashukuru wote kwa uvumilivu wenu maana muda wetu umekwenda kidogo.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 12 Aprili, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.03 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 12 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*